*Hekima, Umoja, Amani, Ni ngao Zetu!*

Jarida Maalum la

# NCHI YETU

**Tanzania imara, Kazi Iendelee**

www.maelezo.go.tz Toleo la 235 | Machi 2022 | Idara ya Habari MAELEZO | TANZANIA




## MWAKA MMOJA WA RAIS SAMIA

#Samia365

scan kusoma jarida kidijitali

HALIUZWI


Maelezo
2022.MAELEZO PODCASTS.
SIKILIZA PODCASTS ZA KISWAHILI KUTOKA IDARA YA HABARI MAELEZO.
2022.MAELEZO PODCASTS.
MAELEZO PODCASTS
Tunapatikana: Spotify, Apple Podcasts, Google Podcasts, Amazon music, Stitcher iHeartRadio, Pandora, TuneIn + Alexa, Podcast Addict, Podchaser, Pocket Casts, Overcast, Castro, Castbox, Podfriend, Deezer, Listen Notes, Player FM, Podcast Index Podcast Index, AudioMack, Soundcloud
MSEMAJIMKUUWASERIKALI/MAELEZONEWS/
WWW.MAELEZO.GO.TZ

## BODI YA WAHARIRI:

**Mwenyekiti**
Gerson Msigwa
Mkurugenzi wa Idara ya Habari
(MAELEZO) na Msemaji Mkuu wa Serikali.

**Wajumbe**
Rodney Thadeus
Zamaradi Kawawa
Jonas Kamaleki

**Msanifu**
Abubakari W. Kafumba

**Mchapishaji**
Imaging Africa Communication Ltd



Idara ya Habari MAELEZO
S.L.P. 25,
**Dodoma, Tanzania.**

Simu: +255 22 292192
Barua pepe: maelezo@mawasiliano.go.tz
www.maelezo.go.tz



Tufuatilie katika kurasa zetu
kwenye mitandao ya jamii

/Msemaji Mkuu wa Serikali
/Maelezo News


scan kusoma
jarida kidijitali

# TAHARIRI

Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inatimiza mwaka mmoja tarehe 19 Machi, 2022.

Naomba kuchukua fursa hii kumpongeza kwa dhati Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan kwa kuiongoza nchi yetu kwa umahiri mkubwa na kudumisha amani, upendo, utulivu na mshikamano kwa Watanzania katika kipindi chote cha mwaka mmoja wa tangu aingie madarakani tarehe 19 Machi, 2021.

Umekuwa ni mwaka mmoja wa mafanikio, matumaini, faraja na matarajio makubwa kwa Watanzania kutokana na kazi kubwa na nzuri iliyofanywa na Serikali na ushirikiano mkubwa ambao Serikali imeupata kutoka kwa wananchi.

Katika kipindi hiki Watanzania wameshuhudia utekelezaji wa kasi wa miradi ya maendeleo ikiwemo miradi ya kimkakati kwa Taifa letu inayojumuisha ujenzi wa reli kwa kiwango cha kisasa (standard gauge railway-SGR), ujenzi wa barabara na madaraja, ujenzi wa Bwawa la Umeme la Julius Nyerere, ujenzi wa bandari, uimarishaji wa shirika la ndege la Taifa (ATCL), ujenzi wa Ofisi za Serikali katika Makao Makuu Dodoma na uwekezaji katika teknolojia ya habari na mawasiliani (TEHAMA).

Ndani ya mwaka mmoja pia Watanzania wameshuhudia kuimarishwa kwa huduma za afya kutokana na ujenzi wa zahanati, vituo vya afya na hospitali, ujenzi wa miundombinu ya elimu ukiwemo ujenzi wa madarasa, maabara na nyumba za walimu, ujenzi wa miradi ya maji, ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya umeme na kuimarisha kwa maeneo ya kutolea huduma.

Pamoja na hayo yote, Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan amefanya kazi kubwa ya kuimarisha uhusiano na ushirikiano wa Tanzania na Mataifa mengine Duniani kote hali ambayo imeiwezesha nchi kunufaika na fursa mbalimbali za uhusiano huo ikiwemo kukuwa kwa biashara, kupata misaada katika maeneo mbalimbali, kupata mikopo yenye masharti nafuu na kukuza teknolojia na ujuzi.

Idara ya Habari (MAELEZO) imetoa jarida hili la Nchi Yetu ambalo ni maalum kwa ajili ya mwaka mmoja wa Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan. Jarida hili lina mkusanyiko wa makala kuhusu kazi kubwa iliyofanywa na Serikali ya Awamu ya Sita kwa mwaka mmoja.

Ni matarajio yetu kuwa kupitia jarida hili, utafurahia makala na picha mbalimbali zinazohusu kazi kubwa na nzuri iliyofanywa na Serikali japo yaliyomo humu ni kwa uchache ikilinganishwa mambo mengi na makubwa yaliyofanyika katika sekta mbalimbali.

Nawatakia usomaji mwema wa Jarida la Nchi Yetu, maalum kwa ajili ya mwaka mmoja wa Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.



**Gerson Partinus Msigwa**
**Mkurugenzi wa Idara ya Habari (MAELEZO) &**
**Msemaji Mkuu wa Serikali.**

# NDANI *ya* JARIDA







## YALIYOMO


| | |
|---|---|
| 01 | Maslahi ya watumishi juu, huduma bora kwa Umma |
| 03 | Uwekezaji kwenye Elimu mafanikio yaonekana |
| 05 | Changamoto za Muungano 11 zapatiwa ufumbuzi |
| 09 | Vijana watengenezewa mfumo maalum wa kupata ujuzi |
| 11 | Ziara za kimataifa zapaisha biashara na uwekezaji nchini |

**015** Watanzania Wanufaika Kiteknolojia na Anwani za Makazi na Postikodi

**019** Sekta ya Ujenzi Yazidi Kuimarika

**023** Mwaka Mmoja Awamu ya Sita Utekelezaji Miradi ya Nishati Washika Kasi

**027** Mwaka wa matokeo Sekta ya Madini

**031** Upekee wa Tanzania mapambano dhidi ya Uviko-19

**035** Mwaka mmoja wa mageuzi Sekta ya Elimu

**037** Utalii waing'arisha Tanzania kimataifa mwaka mmoja

**041** Mwaka Mmoja Awamu ya Sita Tanzania Yaendelea Kuimarisha Amani na Utulivu

**043** Awamu ya Sita Siku 365 za kishindo cha Rais Samia Sekta ya Uchumi

**047** Mwaka mmoja wa Rais Samia, Upatikanaji wa Maji waongezeka

**049** Rais Samia aimarisha usawa wa kijinsia, ustawi na maendeleo ya jamii

**051** Serikali ya Awamu ya Sita yaipaisha Sekta ya Uvuvi

**053** Mwaka Mmoja wa Serikali ya Awamu ya Sita, Amani, Usalama Vyatawala

**057** Serikali ya Awamu ya Sita yaupiga mwingi Sekta ya Uchukuzi

**061** Mwaka mmoja wa Rais Samia Mapinduzi ya Utamaduni, Sanaa na Michezo Yadhihirika

**063** Mwaka Mmoja wa Rais Samia Waongeza Kasi ya Upangaji, Upimaji Ardhi Nchini

**067** Awamu ya Sita: Mafanikio makubwa ujenzi wa uchumi shindani

**071** Rais Samia Afuata Nyayo za Nyerere, Karume Kuulinda Muungano

**073** Mwaka Mmoja wa Rais Samia Madarakani: Wawekezaji Madini Wampongeza

**075** Mama Samia Umetufaa Sana Kiuchumi, Kijamii - Mchambuzi

**077** Tanzania Kichocheo cha Utengenezaji Betri za Umeme za Magari Duniani

**079** Sekta Binafsi Yampongeza Rais Samia Kuweka Mazingira Mazuri ya Biashara, Uwekezaji














## NCHI YETU

**Toleo Maalum la Jarida la Nchi Yetu tukiwa tunatimiza mwaka mmoja tangu Rais wa Awamu ya Sita Mhe. Samia Suluhu Hassan aingie madarakani.**



# Serikali ya Awamu ya Sita - Maslahi ya watumishi juu, huduma bora kwa Umma

## Madai ya watumishi 85,012 Yenye Thamani ya zaidi ya Shilingi Bilioni 123.7 Yalipwa

Na **Mary Mwakapenda**
**UTUMISHI**

Wafanyakazi katika sekta zote za umma na binafsi wamekuwa na mchango mkubwa katika kukuza uchumi wa nchi na kuongeza Pato la Taifa. Mchango wa Wafanyakazi hawa katika kukuza uchumi wa nchi unatambulika sehemu zote duniani ikiwemo kwa Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mhe. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Kwa kutambua mchango mkubwa wa wafanyakazi, mara tu baada ya Serikali ya Awamu ya Sita kuingia madarakani, pamoja na malengo mengine, ilidhamiria kwa dhati kuboresha maslahi ya Watumishi wa Umma ili kuwaongezea ari ya kazi pamoja na kuwawezesha kutoa huduma bora kwa wananchi ambao ndio wadau wakuu wa Serikali.

Dhamira ya Serikali ya kuboresha maslahi ya Watumishi wa Umma inajidhihirisha wazi katika matamko na maelekezo mbalimbali ambayo Mhe. Rais Samia Suluhu Hassan amekuwa akiyatoa kwa viongozi na watendaji katika Taasisi za Umma.

Akizungumza na wafanyakazi kwenye kilele cha Maadhimisho ya Siku ya Wafanyakazi Duniani (Mei Mosi) ya mwaka 2021 jijini Mwanza, Rais Samia Suluhu Hassan alitoa maelekezo mbalimbali kwa lengo la kuwajali watumishi kutokana na mchango wao mkubwa kwa maendeleo ya taifa.

Mojawapo ya maelekezo aliyoyatoa ni pamoja na kupunguzwa kwa asilimia moja (1%) ya makato ya PAYE kutoka asilimia 9 ya sasa kufikia asilimia 8 ili kuwapunguzia watumishi mzigo mkubwa wa kodi na kuongeza kiwango cha mshahara kinachobaki (Net salary) kutokana na kupungua kwa kodi ya PAYE.

Vilevile Mhe. Rais Samia Suluhu Hassan alielekeza kulipwa kwa madeni na madai mbalimbali ya Watumishi wa Umma ambapo tangu ameingia madarakani hadi kufikia Februari, 2022, madai ya watumishi 85,012 yenye thamani ya shilingi 123,775,134,536 yaliyohakikiwa na kubainika kuwa ni sahihi yamelipwa.

Aidha, katika kuhakikisha ajira zinatolewa kwa wananchi kwa lengo la kupunguza tatizo la ajira kwa vijana, Serikali ya Awamu ya Sita tangu iingie madarakani, jumla ya vibali vya watumishi 11,667 wa ajira mpya na mbadala na walioajiriwa wameingizwa katika orodha ya malipo ya mishahara (Payroll) ili kuhaikisha watumishi hao wanapata mishahara yao kwa wakati na kuepuka changamoto ya malimbikizo ya watumishi.

Eneo jingine ambalo Serikali ya Awamu ya Sita imeliwekea msisitizo ni nidhamu na uwajibikaji serikalini. Akilihutubia Bunge la 12 la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Rais Samia Suluhu Hassan aliahidi kuendeleza jitihada za kuimarisha nidhamu na uwajibikaji kwenye utumishi wa umma kwa kuimarisha taasisi za umma na pia kuweka mifumo ya uwajibikaji ili kutoa huduma bora kwa umma.

Ili kufanikisha dhamira ya Serikali ya Awamu ya Sita ya utoaji wa huduma bora kwa umma, Serikali imetengeneza mifumo mbalimbali ya TEHAMA kwa lengo la kurahisisha utendaji kazi na utoaji wa huduma. Mifumo hiyo ni pamoja na:-

Mfumo wa eMrejesho ambao unapatikana kwa anuani ya emrejesho.gov.go.tz ambayo hupokea malalamiko, pongezi na maoni kutoka kwa watumishi na wananchi kwa Serikali yao. Kupitia Mfumo huu, Taasisi zote za umma hupokea malalamiko, pongezi na maoni kutoka kwa watumishi na wananchi kwa ujumla na kufanyia kazi. Katika Mfumo huu, mwananchi anajisajili na kuweza kufuatilia kila hatua ya lalamiko lake na pia kuweza kupata mrejesho.

Mfumo mwingine ni wa Dawati la Huduma la OR-MUUUB (UTUMISHI Call Centre) ambao unawawezesha wananchi kupiga











simu moja kwa moja kupitia namba 0734986508 au 0262160240 na kuelezea changamoto/lalamiko walilonalo. Baada ya kupokea lalamiko mtumishi husika hufuatilia kuhusu lalamiko husika na kumpatia Mwananchi/Mtumishi mrejesho wa suala alilowasilisha. Mfumo hurekodi na kutunza kila suala lililowasilishwa.

Huduma zinazotolewa na Call Centre ni pamoja na masuala ya upandishwaji vyeo, ubadilishwaji vyeo, uhamisho au uteuzi, mishahara, vibali vya ajira, uidhinishaji wa makato na uhakiki wa vyeti; miundo ya maendeleo ya utumishi, maadili na fursa za mafunzo ya wadau wa maendeleo.

Mfumo wa Sema na Waziri wa UTUMISHI ni mfumo mwingine uliobuniwa na Serikali ya Awamu ya Sita kwa lengo la kuwawezesha watumishi na wananchi kuwasiliana moja kwa moja na Waziri wa Nchi, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kuhusu masuala mbalimbali ya Utumishi na Utawala.

Aidha, mfumo huo unampa fursa Waziri wa Utumishi na Utawala Bora kushiriki moja kwa moja kufuatilia mrejesho unaotolewa na watumishi na wananchi wanaopata huduma katika taasisi za umma kwani unaweza kumsaidia kufuatilia hali ya uadilifu na uwajibikaji wa watumishi kwani unamsaidia kujua muda ambao lalamiko limeingia mtumishi gani aliyelipokea na kulifanyia kazi. Mfumo huu pia unamuwezesha Waziri wa Utumishi na Utawala Bora kuongea moja kwa moja na mlalamikaji ili kujua ni kwa namna gani tatizo lake limefanyiwa kazi na kuweza kuchukua hatua stahiki pale ambapo halijafanyiwa kazi pasipokuwa na sababu za msingi, hivyo kuongeza uwajibikaji na uadilifu kwa watumishi wa umma.

Pia kuna Mfumo wa Huduma Mtandao kwa Watumishi (Watumishi Portal) ambao ni sehemu ya Mfumo wa Taarifa za Kiutumishi na Mishahara (HCMIS). Mfumo huu ni mahsusi kwa Watumishi wa Umma kuweza kupata huduma mbalimbali za kiutumishi moja kwa moja bila kulazimika kwenda kwenye ofisi za waajiri wao.

Mfumo huo pia unawezesha watumishi wa umma kuomba imkopo kutoka kwenye Taasisi za kifedha kwa njia ya mtandao. Pia watumishi wanaweza kutafuta watumishi wa kubadilishana vituo vya kazi kwenye mfumo, kuomba uhamisho kutoka kituo kimoja kwenda kingine au Taasisi moja kwenda nyingine.

Aidha, kuna Mfumo wa Uhakiki wa Rasilimaliwatu (Staff Audit) ambao unakusudia kukusanya, kuhakiki na kuainisha mahitaji halisi ya watumishi kwenye Taasisi zote za Umma. Mfumo huu unatumika pia kuchakata na kuainisha mahitaji ya watumishi kwa kila taasisi ya Umma pale taasisi zitakapokuwa zikihuisha orodha ya mahitaji ya watumishi (Joblist).

Kutokana na uboreshaji huo mkubwa wa mifumo mbalimbali serikalini, ni dhahiri kuwa, Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mhe. Rais Samia Suluhu Hassan ina dhamira ya dhati ya kuboresha utoaji wa huduma bora kwa umma na ndio maana pamoja na mambo mengine imejikita zaidi katika kuwajali Watumishi wa Umma ili waweze kutoa huduma kwa wananchi ambao ndio wadau wakuu wa Serikali na hatimaye kukuza pato la taifa.




# Mwaka Mmoja Awamu ya Sita Uwekezaji kwenye Elimu mafanikio yaonekana

## Fedha za Elimu bure zaongezwa kutoka Bilioni 20.5 hadi Bilioni 26 kwa Mwezi

- Madarasa bora Yajengwa

Na **Angela Msimbira**
**TAMISEMI**

Serikali imetekeleza kwa vitendo kwa kuhakikisha inaboresha miundombinu ya elimu nchini kwa kuhakikisha kila mtoto wa kitanzania anapata elimu bila kikwazo cha umbali, upungufu wa walimu, lakini pia imeongeza fedha za uendeshaji wa shule (Capitation Grants) ili kuboresha mazingira ya ujifunzaji na ufundishaji.

Serikali yetu ilianza kutekeleza Elimu bila ada tangu mwaka 2016 na kwa kipindi chote hicho Serikali ilikua inatoa shilingi Bil 20.8 kwa kila mwezi na kiwango hicho kilidumu kwa muda wa miaka mitano bila kuongezeka.

Rais wa Awamu ya Sita, Mhe. Rais Samia Suluhu Hassan tangu alipoingia madarakani ameongeza kiwango cha fedha za Elimu bila Ada kutoka shilingi bilioni 20.8 iliyokuwa inatolewa kwa mwezi hadi kufikia bilioni 26 kwa mwezi.

Haya ni mafanikio katika Sekta ya elimu kwani fedha hizo zimeboresha upatikanaji wa chakula kwa wanafunzi wa shule za bweni na ruzuku ya uendeshaji wa shule kwa kuwa sasa kila mwanafunzi anagharamiwa shilingi 890 tofauti na shilingi 700 aliyokuwa anafidiwa hapo awali.

Haya na mengine mengi yamewezesha watoto wakitanzania na wasio kuwa na uwezo wa kulipia gharama za elimu kupata elimu kupitia mpango huu wa Eimu bila Ada.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Mhe. Innocent Bashungwa amesema kuwa katika miaka iliyopita, nchi yetu ilikuwa na changamoto ya fursa ya upatikanaji wa elimu, kutokana na ada na michango mbalimbali hivyo Serikali iliamua kuanzisha Mpango wa utoaji wa Elimumsingi bila Malipo na tangu Serikali ilipoanzisha mpango huu idadi ya wanafunzi imeongezeka kuanzia darasa la awali, darasa la kwanza na hata wale wanaojiunga na Kidato cha kwanza.

Amesema mpango wa Elimumsingi bila malipo umeleta fursa ya upatikanaji wa elimu kwa kuongeza uandikishaji wa wanafunzi, ambapo kwa elimu ya awali walioandikishwa ni 1,160,580 wakiwemo wanafunzi wenye mahitaji maalum 2,347. Wanafunzi wa awali walioandikishwa ni sawa na asilimia 85 ya kuandikisha wanafunzi wa awali 1,363,834 wanaotarajiwa kuandikishwa

Waziri Bashungwa anaendelea kufafanua kuwa walioandikishwa kujiunga na darasa la saba ni 1,472,517 wakiwemo wenye mahitaji maalum




2,914 ambapo walioandikishwa ni sawa na asilimia 92.3 ya kuandikisha wanafunzi 1,592,375 wanaotarajiwa kuandikishwa

Kwa wanafunzi wanaojiunga na kidato cha kwanza Waziri Bashungwa anasema kuwa wanafunzi 751,946 wakiwemo wanafunzi wenye mahitaji maalum 922, ambapo wanafunzi walioripoti ni sawa na asilimia 83 ya wanafunzi waliochaguliwa na Wanafunzi walioandikishwa MEMKWA ni 8,592 wakiwemo wanafunzi wenye mahitaji maalum 87.

Akielezea kuhusu ujenzi wa miundombinu ya elimu nchini Waziri Bashungwa amesema Serikali kupitia fedha za Mpango wa Maendeleo kwa Ustawi wa Taifa Dhidi ya UVIKO - 19 ilitoa kiasi cha shilingi bilioni 240 kwa ajili ya ujenzi wa vyumba vya madarasa 12,000 lengo likiwa ni kupunguza msongamano wa wanafunzi mashuleni.

Hata hivyo, shilingi bilioni 60 zilitolewa kwa ajili ya ujenzi wa vituo shikizi 3000 ili kuwapunguazia wanafunzi adha ya kutembea umbali mrefu kufuata shule na shilingi bilioni 50 ilitolewa kwa ajili ya ujenzi wa mabweni kwa wanafunzi wenye mahitaji maalum nchini. Ujenzi huo umekamilika na kuwawezesha wanafunzi wote waliochaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza mwaka 2022 kuingia wote kwa awamu mmoja.

Waziri Bashungwa amesema kupitia mradi wa Uboreshaji wa Elimu ya Sekondari (SEQUIP) Serikali imetoa kiasi cha shilingi Bilioni 110 kwa ajili ya ujenzi wa shule za Sekondari za Kata kwenye kata 232 ambazo hazina shule za Sekondari na ujenzi umeshaanza na wengine wapo katika hatua ya ukamilishaji wa shule hizo.

Vilevile, kutoka katika mradi huo Serikali imepeleka shilingi bilioni 30 kwenye Mikoa 10 ambapo kila mkoa umepokea shilingi bilioni 3 kwa ajili ya ujenzi wa shule maalum za sayansi kwa ajili ya wanafunzi wa kike.

Kwa upande wa ujenzi wa miundombinu ya shule za Msingi na Sekondari Waziri Bashungwa amesema Serikali imetoa kiasi cha shilingi bilioni 13 kwa ajili ya ukamilishaji wa vyumba vya madarasa 1,853 ya Shule za Msingi na kiasi cha shilingi bilioni 23 kwa ajili ya ukamilishaji wa vyumba vya madarasa 1,840 ya Shule za Sekondari.

Ameongeza, Serikali imeendelea kutoa fedha kwa ajili ya ukamilishaji wa vyumba vya maabara 869 vya sayansi shule za sekondari lengo likiwa kuwawezesha wanafunzi kujifunza kwa vitendo na kuacha kusoma kwa nadharia ili kuwaongezea ujuzi na maarifa ya masomo ya sayansi.

Kuhusu changamoto ya upatikanaji wa vitabu mashuleni Waziri Bashungwa amesema kiasi cha shilingi bilioni 50 kimetolewa kwa ajili ya ununuzi wa vitabu vya shule za msingi na sekondari ili kuboresha elimu nchini kwa kuhakikisha kila mwanafunzi anakuwa na kitabu cha kujifunzia.

Kwa upande wa ujenzi wa mabweni ya wanafunzi wenye mahitaji maalum Serikali kupitia fedha za UVIKO-19 imetoa kiasi cha bilioni 4 kwa ajili ya ujenzi wa mabweni ya wanafunzi wenye mahitaji maalum katika shule za Msingi

Waziri Bashungwa amesema kupitia fedha za Tozo ya mawasiliano shilingi bilioni 7 zimetolewa kwa ajili ya ukamilishaji wa maboma ya vyumba vya madarasa 560 ya shule za Sekondari nchini. Aidha, Waziri Bashungwa ameeleza kuwa ndani ya utawala Rais Samia Suluhu Hassan tayari ameshatoa kibali na OR-TAMISEMI wameajiri Walimu 6949 ambapo Walimu 3000 walikuwa Walimu wa sayansi kwa shule za Sekondari. Pamoja na mafanikio hayo, Waziri Bashungwa ameeleza kuwa Wizara imeomba kibali kwa Mhe. Rais aridhie ajira za Walimu 7,000 ili kupunguza upungufu wa walimu kwa shule za msingi na sekondari.

Vile vile, Waziri Bashungwa amebainisha kuwa kupitia bajeti inayoandaliwa kwa mwaka 2022/23 kipaumbele kitawekwa katika kukabiliana na upungufu wa matundu ya vyoo hasa kwa shule za msingi itakayokwenda sambamba na kuanza kujenga nyumba za walimu.

Walimu pia hawakusahaulika na kupitia mradi wa GPE-LANES, Serikali imetoa shilingi milioni 550 kwa ajili ya ujenzi wa nyumba za waalimu, shilingi Bilioni 6.8 kwa ajili ya ujenzi wa madarasa 304, matundu ya vyoo 548 yamejengwa kwa shilingi mili 600 na ujenzi shule mpya za msingi 10 ambazo zimegharimu shilingi bilioni 4.

Aidha, Waziri Bashungwa amesema kuwa kutokana na maboresho makubwa yaliyofanywa kwenye sekta ya elimu ikiwemo ukarabati wa shule kongwe na ujenzi wa miundombinu nchini ufaulu wa wanafunzi wa Darasa la saba, Kidato cha pili na nne umeongezeka Mfano katika matokeo ya kidato cha nne mwaka 2021 matokeo yanaonyesha shule kongwe na shule maalum za Serikali zilifanya vizuri mitihani hiyo

"Katika matokeo ya kidato cha nne mwaka 2021 katika shule bora 10 kitaifa shule ya Sekondari Mzumbe (Morogoro) yenye jumla ya watahiniwa 102 walifanya mtihani huo na kufaulu wanafunzi wote, shule ya illiboru ni ya serikali maalum wanafunzi wote walifaulu, hizi ni baadhi ya shule zilizofanya vizuri kwenye matokeo ya kidato cha nne, hii ni kutokana na juhudi za serikali katika kuhakikisha wanaboresha mazingira ya kujifunza na kujifunzia nchini" , amesisitiza Waziri Bashungwa.

Aidha, Waziri Bashungwa amesema kwa upande wa Kidato cha Kwanza mwaka 2022, jumla ya wanafunzi 907,803 wakiwemo wavulana 439,836 na wasichana 467,967 wamechaguliwa kujiunga na Kidato cha Kwanza ikilinganishwa na wanafunzi 833,872 waliojiunga kidato cha kwanza 2021.

Hakika tunajivunia kuwekeza kwenye Elimu na mfumo wa utoaji na upatikanaji wa Elimu nchini ukizidi kuboreshwa siku hadi siku.




# Changamoto za Muungano 11 zapatiwa ufumbuzi

## Changamoto za Muungano Zapungua

## • Sera ya Taifa ya Mazingira Yazinduliwa

Na **Robert Hokororo**
**Ofisi ya Makamu wa Rais - Muungano na Mazingira**

Serikali ya Awamu ya Sita imeendelea kuhakikisha kwamba, nchi yetu inaendelea kuwa yenye umoja, amani na usalama na Muungano wetu unaendelea kulindwa, kudumishwa, kuendelezwa na kuimarishwa. Pia imeendelea kusimamia Sekta ya Mazingira kwa ustawi wa Taifa letu.

Kimsingi yapo mafanikio makubwa yaliyopatikana katika kipindi cha miezi 11, ya Serikali ya Awamu ya Sita yaliyosaidia kuimarisha na kudumisha amani na utulivu wa Tanzania ambayo ni tunu muhimu na fahari ya Nchi yetu. Baadhi ya mafanikio yaliyopatikana ni kama ifuatavyo: -

**1.VIKAO VYA KUTAFUTA UFUMBUZI WA CHANGAMOTO ZA MUUNGANO.**

Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (JMT) na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ) zimeweka utaratibu wa kutatua changamoto za Muungano kupitia mfumo rasmi wa Vikao vya Kamati ya Pamoja ya JMT na SMZ ya kushughulikia Masuala ya Muungano. Vikao vya Kamati ya Pamoja ya JMT na SMZ hufanyika katika ngazi tatu ambazo ni: Makatibu Wakuu wa JMT na SMZ, Mawaziri wa JMT na SMZ na kikao cha Kamati ya Pamoja ya JMT na SMZ, ambacho Mwenyekiti wake ni Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Lengo la kuweka utaratibu huu ni kuimarisha Muungano wetu kwa kuhakikisha kuwa, changamoto zote zinatafutiwa ufumbuzi wa kudumu na ndio kipaumbele cha Serikali zetu zote mbili.

Tarehe 17 Oktoba, 2020 Ikulu, jijini Dar es Salaam, hoja 5 za Muungano zilizopatiwa ufumbuzi zilisainiwa hati za makubaliano na kuondolewa katika orodha ya Hoja za Muungano. Hoja zilizosainiwa hati za makubaliano ni:- Ushirikishwaji wa SMZ kwenye Masuala ya Kimataifa na Kikanda; Ushiriki wa Zanzibar katika Jumuiya ya Afrika Mashariki; Gharama za Kushusha Mizigo Bandari ya Dar es Salaam kwa Mizigo inayotoka Zanzibar; Utafutaji na Uchimbaji wa Mafuta na Gesi Asilia; na Utaratibu wa Vikao vya Kamati ya Pamoja ya JMT na SMZ ya Kushughulikia Masuala ya Muungano.

Katika kipindi cha mwaka mmoja wa Serikali ya Awamu ya Sita vimefanyika vikao vya kujadili masuala ya Muungano katika ngazi zifuatazo: Kikao cha Kamati ya Pamoja ya JMT na SMZ kilifanyika Zanzibar tarehe 24 Agosti, 2021; Hafla ya kusaini Hati za Makubaliano ya kuondoa hoja zilizopatiwa ufumbuzi tarehe 24 Agosti, 2021; Kikao cha Mawaziri wa JMT na SMZ kilifanyika Zanzibar tarehe 23 Agosti, 2021; Kikao cha Makatibu Wakuu wa JMT na SMZ kilifanyika Dar es Salaam tarehe 10 Agosti, 2021; Kikao cha Kamati ya Fedha, Uchumi na Biashara ngazi ya Makatibu Wakuu kilifanyika Dodoma tarehe 2 Agosti, 2021; Kikao cha Kamati ya Fedha, Uchumi na Biashara kilifanyika Dodoma tarehe 3 Agosti, 2021; Kikao cha Sekretarieti ya Kamati ya Pamoja ya JMT na SMZ kilifanyika Dodoma tarehe 4 Agosti, 2021; na Kikao cha Sekretarieti ya Kamati ya Pamoja ya JMT na SMZ kilifanyika Zanzibar tarehe 16 Agosti, 2021

Vikao hivyo vilijadili kwa kina hoja 18 ambapo hoja 11 zimepatiwa ufumbuzi na kuondolewa kwenye orodha ya hoja za Muungano. Hafla ya kusaini hati za makubaliano ya kuondoa hoja za Muungano zilizopatiwa ufumbuzi ilifanyika tarehe 24 Agosti, 2021 katika Ukumbi wa Chuo cha Utalii, Maruhubi Zanzibar.

Hoja zilizopatiwa ufumbuzi na kuondolewa kwenye orodha ya hoja na Muungano ni:Uingizaji wa maziwa kutoka Zanzibar; Usimamizi wa ukokotoaji na ukusanyaji wa Kodi kwenye Huduma za Simu unaofanywa na Mamlaka ya Mapato Zanzibar (ZRB), Mkataba wa mkopo wa fedha za ujenzi wa Barabara ya Chake chake hadi Wete – Pemba, Mkataba wa mkopo wa fedha za Mradi wa Ukarabati wa Hospitali ya Mnazi

Mmoja;Mkataba wa mkopo wa fedha za ujenzi wa Bandari ya Mpigaduri, Uvuvi kwenye Ukanda wa Uchumi wa Bahari Kuu; Ajira kwa Watumishi wa Zanzibar katika Taasisi za Muungano, Mgawanyo wa mapato yatokanayo na Misaada kutoka Nje ya Nchi, Mapato yanayokusanywa na Uhamiaji kwa upande wa Zanzibar; Uteuzi wa Makamu Mwenyekiti wa Tanzania Revenue Appeal Tribunal (TRAT) kutoka Zanzibar; na Uteuzi wa Mjumbe wa Bodi ya Bima ya Amana (Deposit Insurance Board - DIB) kutoka Zanzibar.

**2. MIRADI YA MAENDELEO INAYOTEKELEZWA PANDE MBILI ZA MUUNGANO**

Serikali ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar zimeendelea kushirikiana katika miradi mbalimbali ya maendeleo. Miradi hii imewawezesha wananchi wa pande zote mbili za Muungano kushiriki katika shughuli za kiuchumi na kuongeza ajira kupitia utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo.

Utekelezaji wa miradi hiyo umefanikiwa kuinua hali ya wananchi, kukuza uchumi na kupunguza umaskini wa kipato na kuinua ubora wa maisha na ustawi wa jamii wa pande zote mbili za Muungano. Miradi hiyo ya maendeleo hufadhiliwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kushirikiana na Washirika wa Maendeleo.

Mafanikio mengine ni usogezaji wa huduma za mawasiliano maeneo ambayo yana mawasiliano hafifu au hayana mawasiliano kabisa ambapo Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (UCSAF) na Kampuni ya Mawasiliano Zanzibar (Zantel) wameingia makubaliano mwezi Januari, 2022 ya kujenga minara ya simu 42 katika shehia 38 kwa lengo la kuboresha huduma ya mawasiliano Zanzibar.

Vile vile, Zanzibar ilipatiwa jumla ya shilingi bilioni 230 zilizotokana na mkopo nafuu kutoka IMF kwa ajili ya kukabiliana na athari za UVIKO 19 ambapo fedha hizo zimeelekezwa kwenye huduma za kijamii zikiwemo afya, elimu, miundombinu na ujenzi wa masoko.

**3. KUIMARISHA USHIRIKIANO**

Vikao vya kuimarisha ushirikiano kwa masuala yasiyo ya Muungano na Ushirikiano baina ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa masuala yasiyo ya Muungano umeimarika. Serikali zote mbili zimeweka utaratibu wa vikao vya kisekta vya ushirikiano kwa Wizara, Idara na Taasisi zisizo za Muungano.

Lengo la kufanya vikao hivyo ni kuimarisha ushirikiano wa pande mbili za Muungano kwa manufaa ya Watanzania. Vikao hivyo vinajadili masuala ya kisekta ikiwemo kubadilishana ujuzi, utaalamu na uzoefu kupitia mafunzo, masuala ya sera na ushiriki katika masuala ya kimataifa ili kuleta ufanisi na uwiano wa maendeleo kwa pande zote mbili za Muungano.

Serikali mbili zimeandaa Mwongozo wa Vikao vya Ushirikiano vya Kuimarisha Ushirikiano kati ya Wizara, Idara na Taasisi zisizo za Muungano za JMT na SMZ.

Kwa mujibu wa mwongozo huo, Wizara, Idara na Taasisi zisizo za Muungano za JMT na SMZ zinazoshabihiana kimajukumu, zinatakiwa kufanya vikao vya ushirikiano visivyopungua viwili kwa mwaka.

Kwa kipindi cha mwako mmoja, Serikali ya Awamu ya Sita (6), vimefanyika vikao 21. Sekta zilizokutana ni Sekta ya Nishati, Sekta ya Maji, Sekta ya Madini, Sekta ya Uchukuzi, Sekta ya Utumishi na Utawala Bora, Uratibu wa shughuli za Serikali, Sekta ya Viwanda na Biashara, Sekta ya Maliasili na Utalii, Sekta ya Afya, Sekta ya Kilimo, Sekta ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Sekta ya Ardhi, Sekta ya Fedha na Mipango na Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa.

Ofisi ya Makamu wa Rais na Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Zanzibar zitaendelea kuzikumbusha Wizara zisizo za Muungano za pande zote mbili umuhimu wa kufanya vikao vya ushirikiano. Ushirikiano huo ni muhimu kwa kuwa unasaidia kuzitafutia ufumbuzi kwa haraka na kwa ufanisi changamoto za Muungano na za kisekta zilizopo na zinazojitokeza. Tathmini inaonesha Wizara za Kisekta zinapokutana changamoto zinapungua na Muungano unazidi kuimarika.

**Mafanikio katika Mazingira**

Kumekuwa na juhudi mbalimbali zilizofanywa na Serikali katika uhifadhi na usimamizi wa mazingira na yote hii ni kutokana na ukweli kuwa suala la hifadhi na usimamizi wa mazingira nchini ni moja ya vipaumbele muhimu vya Serikali.

**UZINDUZI WA SERA YA TAIFA YA MAZINGIRA YA MWAKA 2021**

Februari 12, 2022 Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Philip Isdor Mpango alizindua Sera ya Taifa ya Mazingira ya mwaka 2021.

Sera hiyo imeweka malengo na matamko mahususi ya Kisera yatakayowezesha kukabiliana na changamoto za mazingira nchini kwa ufanisi mkubwa. Aidha, Sera hii imezingatia fursa za kiuchumi katika hifadhi na usimamizi wa mazingira nchini ambazo hazikutambuliwa na Sera ya awali.

Fursa hizo ni kama vile: Urejelezaji wa taka ambao unapunguza gharama za udhibiti wa taka na kuongeza kipato, Utengenezaji wa bidhaa rafiki kwa mazingira kama mifuko mbadala ya plastiki, majiko banifu na Mkaa mbadala na Biashara ya hewa ukaa



katika kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi. Vilevile, Sera hii imezingatia kuwepo kwa mipango mipya ya maendeleo ya kitaifa na kimataifa ikiwemo Mpango Elekezi wa Miaka Kumi na Tano (2011/12 – 2025/26); Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2021/22- 2025/26); Malengo ya Maendeleo Endelevu (2030) na Makubaliano ya Paris kuhusu Mabadiliko ya Tabianchi.

**KAMPENI YA KITAIFA YA UPANDAJI MITI**

Ofisi imeendelea kuratibu utekelezaji wa Kampeni ya Upandaji Miti kwa lengo la kurejesha Uoto wa Asili na kupunguza hali ya kuenea kwa jangwa na ukame ambapo kila Halmashauri ya Wilaya imeelekezwa kupanda miti milioni 1.5 kila mwaka. Hadi kufikia Mei 2020 takriban miti 608,494,464 ilipandwa katika mikoa yote 26 katika Halmashauri zote. Baada ya tathmini asilimia 62.8 ya miti iliyopandwa ndiyo iliyopona. Aidha, kutokana na umuhimu wa kulinda hifadhi ya bahari, wananchi wameshirikishwa kupanda na kuhifadhi mikoko katika maeneo mbalimbali ya Pwani Tanzania Bara na Tanzania Visiwani hatua inayosaidia kupunguza changamoto ya mabadiliko ya tabianchi.

**MATUMIZI YA NISHATI MBADALA**

Ofisi imeendelea kuhamasisha uzalishaji na matumizi ya nishati mbadala wa kuni na mkaa hususai katika Taasisi za Serikali zinazotumia kiwango kikubwa cha nishati ya kuni na mkaa.

Wizara na Taasisi zikiwemo Magereza, Jeshi la Kujenga Taifa, Jeshi la Wananchi, Uhamiaji, Kurugenzi ya Huduma ya Wakimbizi pamoja na Vyuo na Taasisi zilizopo chini ya Wizara ya Maliasili na Utalii zimewasilisha mipango yao ya kupunguza matumizi ya kuni na mkaa. Uchambuzi unaonesha Taasisi nyingi zinatumia gesi ya kwenye mitungi (Liquefied Petroleum Gas - LPG), vitofali vya mkaa (Briquettes) na umeme kwa ajili ya kupikia.

**MIRADI INAYOTEKELEZWA**

Miradi mbalimbali ya mazingira inayotekelezwa ni pamoja na Mradi wa Kurejesha Ardhi Iliyoharibika na Kuongeza Uhakika na Usalama wa Chakula katika Maeneo Kame ya Tanzania, Mradi wa Kuhimili Mabadiliko ya Tabianchi kwa Kutumia Mifumo Ikolojia Vijijini, Mradi wa kujengea uwezo taasisi ili Kupunguza Hewa Ukaa inayosababishwa na ukataji miti na uharibifu wa misitu ifikapo mwaka 2022, Mradi wa kujenga uwezo wa Kitaifa kuwezesha utekelezaji wa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira na Mradi wa Majaribio wa Kikanda wa Kuhimili Mabadiliko ya Tabianchi katika Bonde la Ziwa Victoria.

**ITIFAKI NA MIKATABA YA KIMATAIFA KUHUSU MAZINGIRA**

Pamoja na yote, Tanzania imepiga hatua kubwa katika kuweka mfumo wa Usimamizi wa Mazingira nchini kwa kuungana na Jumuiya za Kimataifa katika kukuza juhudi za kuhifadhi mazingira kupitia Itifaki 8 na Mikataba 10 ya Kimataifa ambayo Tanzania imesaini na kuridhia.

Ni dhahiri kuwa mafanikio makubwa yaliyopatikana ndani ya kipindi cha mwaka mmoja cha Serikali ya Awamu ya Sita yametokana na jamii yenye umoja, mshikamano na isiyo na ubaguzi. Watu wa pande mbili za Muungano wanaishi na wanafanya kazi zao za kujiletea maendeleo katika sehemu yoyote ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania bila ya kubughudhiwa. Aidha, Ofisi itaendelea kushirikiana na wadau wa ndani na nje ya nchi katika kutekeleza mipango, mikakati na programu mbalimbali za kuhifadhi mazingira kwa maendeleo endelevu.










DODOMA SECONDARY
UHAI WETU
Mazingira


Soma na Mti!





# Awamu ya Sita yaendelea kuwatengenezea vijana mfumo maalum wa kupata ujuzi

Na **Adam Haule**
**OWM (KVAU)**

Moja ya mafanikio makubwa ya Serikali ya Awamu ya Sita chini ya Uongozi wa Rais Samia Suluhu Hassan imeendelea kuwatengenezea vijana mfumo maalum wa kupata ujuzi ili kuwaondolea changamoto ya ajira.

Inafahamika kuwa ukuzaji wa fursa za ajira ni miongoni mwa agenda za kipaumbele katika programu za maendeleo za kidunia, kikanda na hata kitaifa. Umuhimu wa ukuzaji wa fursa za ajira umejengwa katika misingi ya kijamii na kiuchumi. Kwa upande wa kijamii inaelezwa kuwa kila mtu ana haki ya kufanya kazi pamoja na kupata ajira za staha.

Kiuchumi, ajira za staha pamoja na tija ya nguvukazi ndiyo kichocheo cha ukuaji wa uchumi jumuishi na endelevu. Kwa ujumla ajira za staha ndiyo njia pekee inayoweza kupunguza kiwango cha umasikini wa kipato.

Serikali kwa kushirikiana na wadau imekuwa ikichukua hatua mbalimbali za kuongeza kasi ya kukuza fursa za ajira nchini. Hatua zilizochukuliwa ni pamoja na za kisera kama vile: kutoa mitaji kupitia mikopo nafuu kwa vijana, wanawake, na wenye ulemavu; na kutoa mafunzo ya ujuzi kulingana na mahitaji.

Baadhi ya hatua za kukuza ajira zilizotekelezwa ni pamoja na: Kutekeleza Sera ya Taifa ya Ajira ya mwaka 2008; Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Vijana ya Mwaka 2007; Sera ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi ya mwaka 2004 pamoja na Sera nyingine za Kisekta. Aidha, Serikali imeanzisha Mifuko ya Uwezeshaji Wananchi kwa lengo la kuwezesha mitaji; Programu ya Taifa ya Kukuza Ujuzi; na Mkakati wa Kuwezesha Vijana Kushiriki katika Kilimo.

Kwa kutambua umuhimu wa kuzalisha fursa mpya za ajira, Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi (CCM) ya mwaka 2020, imeilekeza Serikali kuweka mikakati ya kuzalisha ajira milioni nane (8).

Katika Ilani hiyo Ibara ya 26 (e) imeelekeza kuandaliwa kwa Programu Maalum za kuwezesha vijana waliomaliza taasisi za elimu ya juu na kati kujiajiri au kuajirika.

Programu hizo zilenge kuweka mazingira ya vijana kupata mitaji, elimu ya ujasiriamali, ardhi na mazingira wezeshi kuweza kushiriki kikamilifu katika shughuli wanazokusudia kuzifanya. Vilevile, Mpango wa Tatu wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano (FYDP III: 2021/22 – 2025/26) umeweka mikakati ya kuwezesha nguvukazi ya Taifa kupata ajira za staha. Hivyo, Serikali imeandaa Programu ya Kuzalisha Fursa za Ajira kwa Vijana itakayotekelezwa kwa kipindi cha miaka mitano (2021/2022 - 2025/2026).

Serikali kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu imeendelea kuwajengea uwezo vijana kwa kutekeleza Programu ya Taifa ya Ukuzaji Ujuzi ili vijana hao waweze kujiajiri na hatimaye kuondokana na changamoto ya ajira.

Programu hiyo imekuwa ikitekelezwa kuptia mafunzo ya kukuza ujuzi kwa vijana kwa njia ya Uanagenzi "Apprenticeship training", mafunzo ya urasimishaji ujuzi uliopatikana katika mfumo rasmi "Recognition of Prio Learning" mafunzo kwa Utarajali "Internship training", Mafunzo ya Kilimo cha Kisasa kwa kutumia Teknolojia ya Kitalu Nyumba "Greenhouse Training" na mafunzo ya kukuza ujuzi kwa walio makazini "Skills Updating/Upgrading".

Mapema Agosti mwaka 2021 Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Kassim Majaliwa alizindua mafunzo ya kukuza ujuzi kwa vijana

kwa njia ya Uanagenzi "Apprenticeship training" awamu ya tatu alieleza kuwa Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mhe. Rais Samia Suluhu Hassan imetenga shilingi bilioni tisa kwa ajili ya kugharamia mafunzo ya Uanagenzi kwa vijana ambao hawakubahatika kupata nafasi kwa sasa.

Alieleza kuwa, Serikali imeamua kuimarisha Programu hiyo ya Taifa ya Kukuza Ujuzi kwa kuongeza idadi ya wanufaika ili vijana hao watambue kwamba fursa hiyo waliyopata ni adimu sana na wanapaswa kuithamini na kuitumia kama ilivyokusudiwa.

"Nendeni mkajifunze kwa bidii, muwe na nidhamu kwani bidii yenu kwenye kujifunza ni ufunguo wa kupata maarifa yatakayowawezesha kufanya kazi kwa weledi baada ya kuhitimu." alieleza. Aidha, wito kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa zihakikishe vijana hao wanawaunganisha kwenye vikundi vya ushirika na kuwapatia mikopo ya asilimia 10 inayotolewa kwa vijana, wanawake na wenye ulemavu ili wapate nyenzo za kufanyia kazi.

"Waheshimiwa Wakuu wa Mikoa wote hakikisheni mnasimamia kwa karibu suala hili ili kuwawezesha vijana kushiriki kikamilifu katika kujenga nchi yetu badala ya kuwa watazamaji." alisema.

Januari 15, 2022 akitunuku vyeti kwa Wanagenzi wahitimu wa mafunzo ya kurasimisha ujuzi uliopatikana nje ya mfumo rasmi wa mafunzo katika Chuo cha Ufundi Stadi VETA Njiro, Jijini Arusha, Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu anayeshughulikia Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu Prof. Joyce Ndalichako alieleza kuwa Serikali ya Awamu ya Sita Inayoongozwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Samia Suluhu Hassan imeweka kipaumbele katika programu za kukuza ujuzi kwa lengo la kuwasaidia vijana ili waweze kujiajiri au kuajiriwa sambamba na kuwajengea uwezo wa kukuza na kuboresha uzalishaji katika fani mbalimbali. "Serikali ina dhamira ya dhati ya kuwasaidia vijana nchini na katika kutekeleza hilo Serikali kupitia Mpango wa Tatu wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2021/2022 – 2025/2026), imejipanga kukuza ujuzi kwa watanzania wapatao 681,000," alisema

Pia, Masuala ya Watu wenye Ulemavu ni moja ya kipaumbele muhimu kwa Serikali anayo iongoza Rais Samia Suluhu Hassan katika kuhakikisha kuwa haki za kundi hilo haziachwi nyuma.

Serikali kupitia fedha za UVIKO – 19 imepanga kujenga na kukarabati Vyuo vya Ufundi Stadi kwa Watu wenye Ulemavu ambapo tayari shilingi Billioni Nane zimetolewa kwa ajili ya vyuo hivyo. Kwa sasa Wizara inaratibu kwa kazi ujenzi wa Vyuo vipya katika Mkoa wa Songwe na Kigoma. Pia ukuarabati wa Chuo cha Yombo – Dar es Salaam, Mirongo – Mwanza, Masiwani – Tanga, Luanzari – Tabora, Sabasaba – Singida na Mtapika – Mtwara.









# Ziara za kimataifa zapaisha biashara na uwekezaji nchini

Na **Na Emmanuel Buhohela**
**MAMBO YA NJE**

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Samia Suluhu Hassan anatimiza mwaka mmoja tangu aingie madarakani. Rais Samia aliapishwa Machi 19,2021 kushika wadhifa huo kufuatia kifo cha aliyekuwa Rais wa Jamhuri ya Muuungano wa Tanzania Dkt. John Pombe Magufuli.

Mara baada ya kuapishwa Rais Samia alianza mara moja utekelezaji wa majukumu yake akiwa ni Rais na Amiri Jeshi Mkuu katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambapo jambo alilolipa kipaumbele ni kuhakikisha kuwa Jmahuri ya Muungano wa Tanzania inaendelea kukubalika na kuheshimika Kimataifa ikiwa ni pamoja na kuweka msisitizo katika Diplomasia ya Uchumi.

Katika kipindi cha mwaka mmoja wa uongozi wa Rais wa Awamu ya Sita, Mhe. Samia Suluhu Hassan, Serikali ya Tanzania imeendelea kutekeleza Sera ya Mambo ya Nje ya Tanzania ya mwaka 2001 ambayo imejikita katika diplomasia ya uchumi.

Diplomasia ya uchumi inajumuisha shughuli zote za kiuchumi kama vile kutafuta masoko ya bidhaa na huduma nje ya nchi; uagizaji bidhaa na huduma kutoka nje ya nchi; uwekezaji wa moja kwa moja kutoka nje au kuwekeza nje ya nchi katika sekta mbalimbali za uchumi; kutafuta mikopo yenye masharti nafuu; kukuza sekta ya utalii; kutafuta misaada kutoka washirika wa maendeleo; na kutafuta fursa za ajira na ufadhili wa masomo nje ya nchi.

Mwaka mmoja wa Rais Samia, Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa kushirikiana na wadau wa diplomasia ya uchumi, nchi marafiki, jumuiya za kikanda na kimataifa imeratibu mikakati mbalimbali ambayo imekuwa na manufaa makubwa kwa nchi yetu:

**Kuimarika na kukua kwa biashara**

Takwimu za hivi karibuni zimerekodi ongezeko kubwa la mauzo ya nje kwa bidhaa na huduma za Tanzania katika nchi mbalimbali za Afrika Mashariki. Mathalani takwimu zilizotolewa na Ofisi ya Takwimu ya nchini Kenya (Kenya National Bureau of Statistics) zimeonesha kukua maradufu kwa mauzo ya Tanzania katika nchi ya Kenya kwa takribani shilingi bilioni 20.5 kwa nusu ya kwanza ya mwaka 2021/2022 kutoka bilioni 10.8 kwa mwaka uliopita wa 2020/2021.

Hii imetokana na mahusiano mazuri ya kibiashara yaliyopo baina ya nchi hizi mbili ambayo yamechangiwa kwa kiasi kikubwa na ziara iliyofanywa na Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan nchini Kenya.

Kupitia ziara hiyo tofauti na vikwazo vingi vya kibiashara vya kiforodha na visivyo vya kiforodha ambavyo vilikuwa vikiathiri ushirikiano wa kibiashara baina ya Tanzania na Kenya vulipunguzwa na vingine kuondolewa kabisa baada ya mazungumzo.

Licha ya ziara hiyo kusaidia kupunguza vikwazo na kuondoa tofauti za kibiashara, Tanzania na Kenya pia zilikubaliana kuimarisha sekta ya utalii, kukamilisha utekelezaji wa miradi ya pamoja ya miundombinu inayounganisha nchi hizi

mbili na utekelezaji wa mradi wa bomba la kusafirisha gesi asilia kutoka Dar es Salaam hadi Mombasa. Katika kipindi hiki cha mwaka mmoja Tanzania na Kenya zimefanikiwa kushughulikia vikwazo zaidi ya 30 miongoni mwa jumla ya zikwazo 64 visivyo vya kikodi vilivyokuwepo.

Katika kuendelea kukuza biashara, Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki Desemba 2021, iliratibu na kufanikisha majadiliano baina ya benki ya CRDB na Mamlaka za Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo ili kuwezesha kuanzishwa kwa kampuni tanzu ya benki hiyo itakayotoa huduma za kifedha katika soko la DRC.

Majadiliano hayo yaliwezesha kuanza kwa taratibu za usajili ambapo leseni za biashara zinatarajiwa kukamilika mwezi Machi 2022. Hatua hiyo itachochea ukuaji wa biashara kati ya Tanzania na DRC kwa kurahisisha upatikanaji wa huduma za kifedha kwa wafanyabiashara wanaonunua bidhaa za Tanzania na kuziuza nchini DRC.

Wakati huo huo, Novemba 2021, Wizara iliratibu na kufanikisha ziara ya ujumbe wa Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko Tanzania (CPB) jijini Kigali, Rwanda na katika jimbo la Haut-Katanga nchini DRC ambayo ililenga kutafuta masoko ya nafaka zinazozalishwa nchini.

Kutokana na ziara hiyo, CPB ilifanikiwa kupata soko la tani 100,000 za bidhaa za chakula pamoja na kusaini mkataba wa kufungua ofisi ya kusimamia mauzo na ghala la kuhifadhi na kusambaza bidhaa za chakula lenye ukubwa wa mita za mraba 5,443 jijini Lubumbashi, DRC. Hadi sasa shehena ya kwanza ya tani 450 za unga, mahindi, ngano, mchele na maharage zimewasili jijini Lubumbashi, DRC kwa ajili ya kuuzwa. Hatua hii ya CPB kufanikiwa kupata soko la bidhaa za kilimo itakuza sekta ya kilimo nchini na uchumi kwa ujumla.

Wakati huo huo, Wizara katika kipindi cha mwaka mmoja wa Serikali ya Awamu Sita imeratibu na kufanikisha upatikanaji wa soko la bidhaa za Tanzania hususan dagaa, samaki na mchele nchini Ubelgiji. Hadi sasa, tani 4 za dagaa kutoka Kigoma na tani 25 za mchele kutoka Mbeya zimeuzwa nchini humo.

Aidha, wastani wa tani 40 - 50 za minofu ya samaki zinauzwa kila wiki nchini Ubelgiji. Ubelgiji ni soko muhimu kwa Tanzania kwa kuwa bidhaa za nchi yetu zinazouzwa katika soko hilo hupata fursa ya kuuzwa katika masoko mengine ndani ya nchi za Umoja wa Ulaya.

**Kusainiwa kwa Mikataba ya Maendeleo**

Katika kuendelea kuhakikisha maslahi ya Taifa nje ya nchi yanalindwa, sambamba na kunufaika na fursa zilizopo Kimataifa, Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki imeendelea kuratibu ziara za Viongozi Wakuu wa Serikali, Mashirika na Taasisi za Serikali. Ziara hizo zimepelekea kusainiwa kwa mikataba ya maendeleo inayogusa sekta mbalimbali nchini.

Mathalani kupitia ziara za Rais Samia Suluhu Hassan, katika maeneo mbalimbali Duniani, hati za makubaliano ambazo zinalenga kuboresha sekta mbalimbali nchini zilisainiwa. Miongoni mwa maeneo ambayo hati za makubaliano zimesainiwa kutokana na ziara ni pamoja na: Hati ya Makubaliano ya Ushirikiano kati ya Kituo cha Uwekezaji cha Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mamlaka ya Uwekezaji ya Jamhuri ya Kenya kuhusu Ushirikiano katika Uwekezaji; Hati ya Makubaliano ya Ushirikiano kati ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Jamhuri ya Kiislamu ya Misri katika Sekta ya Elimu, Hati ya Makubaliano ya Ushirikiano kati ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Jamhuri ya Kiislamu ya Misri kuhusu Kuimarisha Uhusiano katika Uwekezaji.

Maeneo mengine ni pamoja na Hati ya Makubaliano ya Ushirikiano kati ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Jamhuri ya Burundi katika Sekta ya Uvuvi; Hati ya Makubaliano ya Ushirikiano kati ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Jamhuri ya Burundi katika Sekta ya Madini; Hati ya Makubaliano ya Ushirikiano kati ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Jamhuri ya Burundi kuhusu Ufundishaji wa Lugha ya Kiswahili nchini Burundi na Lugha ya Kifaransa nchini Tanzania; Hati ya Makubaliano ya Ushirikiano kati ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Jamhuri ya Burundi katika Sekta ya Nishati; Hati ya Makubaliano ya Ushirikiano kati ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Jamhuri ya Burundi katika Sekta ya Kilimo, Kusainiwa kwa makubaliano ya kuanza utekelezaji wa mradi wa kuongeza mnyororo wa thamani mazao ya nyuki hapa nchini kwa ufadhili wa Euro milioni 10 sawa na shilingi bilioni 27 kutoka Umoja wa Ulaya mwezi Septemba 2021.

Makubaliano hayo yanahusisha pia utafutaji wa masoko na mradi utatekelezwa katika mikoa ya Katavi, Rukwa, Kigoma, Tabora na Singida na Pemba, Zanzibar. Vilevile mwezi Novemba 2021 Tanzania na Ubelgiji ziliwekasaini Mkataba kuhusu Ushirikiano katika Huduma za Usafiri wa Anga. Mkataba huu unalenga kuimarisha huduma za kimataifa za usafiri wa anga za kibiashara kati nchi hizi ambapo ndege za Tanzania zitaweza kwenda moja kwa moja Ubelgiji na ndege za Ubelgiji kuja Tanzania. Kuanzshwa kwa safari za ndege baina ya nchi hizi mbili kunalenga pia kuongeza idadi ya watalii kutoka bara la Ulaya.

Katika hatua nyingine, akiwa nchini Senegal Mhe. Balozi Liberata R. Mulamula (Mb), Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki pembezoni mwa Mkutano wa Nane wa Mawaziri wa Jukwaa la Ushirikiano kati ya China na Afrika alipata fursa ya kukutana na kufanya mazungumzo na Mheshimiwa WANG Yi, Kansela Mkuu na Waziri wa Mambo ya Nje wa Jamhuri ya Watu wa China.

Katika mazungumzo yao pamoja na mambo mengine Mhe. Waziri WANG Yi aliahidi kutoa msaada wa fedha kwa Tanzania kiasi cha RMB 100,000,000 sawa na Shilingi za Kitanzania bilioni 35 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo nchini ambayo itakubalika na pande zote mbili.

Aidha, Wizara imeshiriki na kuratibu kusainiwa kwa Mkataba wa Makubaliano ya awali kati ya Shirika la Taifa la Madini (STAMICO) na kampuni ya SUNESS Limited ya Italia kwa ajili ya kuendeleza mradi mkubwa wa shaba katika mkoa wa Kilimanjaro.

Kwa muda mrefu kwenye nyanja ya diplomasia, ziara za kimataifa zimeendelea kuwa miongoni mwa nyenzo muhimu katika kufanikisha upatikanaji wa fursa za kiuchumi na kijamii kutoka wabia wa maendeleo. Hali kadhalika, katika kipindi cha mwaka mmoja wa Serikali ya Awamu ya Sita chini ya uongozi wa Mhe. Samia Suluhu Hassan, ziara za kimaitafa za Viongozi Wakuu, Mawaziri na Watendaji wa Serikali zimeendelea kuwa moja ya nyenzo muhimu katika kufanikisha maslahi ya kiuchumi na kijamii.

Rais Samia pia ameshudia utiaji saini wa zaidi ya mikataba 30 ya biashara na uwekezaji jijini Dubai ambapo alikuwa Mgeni rasmi katika Kongamano la Kimataifa la Biashara na Uwekezaji.

Hakika katika kipindi cha mwaka mmoja wa Serikali ya Awamu ya Sita, Diplomasia ya Uchumi imetekelezwa kwa vitendo na kuinufaisha Tanzania.




United Nations
Climate Change
UN CLIMATE CHANGE CONFERENCE UK 2021


unesco






unesco




CHAMA CHA WATANZANIA




EXPO2020


EMBASSY OF THE UNITED STATES OF AMERICA





# Watanzania Wanufaika Kiteknolojia na Anwani za Makazi na Postikodi

Na **Prisca Ulomi**
**Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari**

Tanzania inapoadhimisha Mwaka mmoja wa Serikali ya Awamu ya Sita madarakani chini ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Samia Suluhu Hassan, Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari imetekeleza miradi mitano ikiwemo Ujenzi wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano, Mradi wa Tanzania ya Kidijitali, Mradi wa Mfumo wa Anwani za Makazi na Postikodi, Upanuzi wa Usikivu wa Shirika la Utangazaji Tanzania (TBC) na Habari kwa Umma.

Kwa mujibu wa taarifa ya Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Kabla ya mwezi Machi, 2021 Kilomita 7,910 za Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano zilikua zimejengwa. Katika kipindi cha mwaka mmoja Machi, 2021 – Machi, 2022 Kilomita 409 zimejengwa na kufikisha Kilomita 8,319; pia kukamilika kwa ukarabati wa kilomita 105 za ujenzi wa mkongo kati ya Jiji la Arusha na Namanga kupitia kwenye miundombinu ya TANESCO.

Aidha, upembuzi yakinifu wa kujenga Mkongo wa Mawasiliano kuunganisha na nchi ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC) kupitia kwenye Ziwa Tanganyika umekamilika.

Wizara imeingia Mkataba wa Mashirikiano na Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) kwa ajili ya kufanya kazi pamoja ya kupitisha miundombinu ya mawasiliano kwenye miundombinu ya umeme kwa lengo la kuongeza mtandao wa mawasiliano na wa umeme.

Hatua hii itapunguza gharama za ujenzi wa Mkongo na kuharakisha mradi huu, ambapo zilikuwa zijengwe Kilomita 1,880 lakini kutokana na Mkataba huu zitajengwa Kilomita 4,442.

Aidha, kwa fedha hizi vitajengwa vituo 111 vya kutolea huduma na kuongeza nguvu (Transmission and Power systems) ambapo upanuzi utafanyika kwenye vituo 74 na vituo vipya 37 vitajengwa ikijumuisha ujenzi wa majengo 68 ya Mitambo (Civil Works).

Hadi kufikia mwezi Februari, 2022 Wizara imesaini mikataba 12 ya ujenzi wa mkongo na mikataba sita (6) ipo katika hatua za mwisho. Mikataba hii 18 itagharimu shilingi bilioni 136

Ndani ya kipindi cha mwaka mmoja wa Rais Samia madarakani, Wizara imetekeleza Mradi wa Mfumo wa Anwani za Makazi kwa kusimika miundombinu kwenye jumla ya Kata 135, kutoka kata 117 zilizokuwa zimesimikwa Machi, 2021. Kusimikwa kwa nguzo 5,300 za majina ya barabara/ mitaa katika Kata 18 za Halmashauri ya Jiji la Mwanza; kubandikwa kwa vibao 78,138 vya namba za nyumba katika kata 18 za Halmashauri ya Jiji la Mwanza; kukusanywa kwa taarifa za nyumba na viwanja 98,801 kwa Makazi na Wakazi kwa kutumia Programu Tumizi; kukamilika kwa uandaaji wa ramani za mipaka ya kiutawala katika Halmashauri 20 za Majiji ya Ilala, Tanga, Mwanza, Mbeya na Dodoma, Manispaa za Tabora, Morogoro, Bukoba, Lindi, Shinyanga, Songea, Moshi, Kigamboni, Kinondoni, Temeke, Ubungo, Singida, Iringa, Kigoma Ujiji, na Sumbawanga ambapo mipaka yake imetasfiriwa kwa mujibu wa Matangazo ya Serikali (GN).

Aidha, Serikali imeunda Programu Tumizi (Mobile App) ya Mfumo kwa ajili ya kuwezesha matumizi na utekelezaji wa Mfumo.

Programu Tumizi inatumika katika kumuongoza mtu kutoka Anwani ya moja Makazi kwenda Anwani ya Makazi nyingine.

Wizara imeandaa rasimu ya Mpango Mkakati utakaowezesha kukamilisha Mfumo wa Anwani za Makazi Ifikapo Mwezi Mei, 2022 ili kurahisisha zoezi la Sensa. Mkakati husika utahitaji jumla Shilingi Bilioni 714, ambapo Shilingi bilioni 107 zitapaswa kutoka Serika-




lini na Shilingi bilioni 607 zitanatarajiwa kutoka kwa wadau mbalimbali wakiwemo wananchi wanaochangia utekelezaji.

Mikataba 12 ya Mradi wa Anwani za Makazi na Postikodi ipo katika hatua ya tathmini ambayo ina thamani ya Shilingi 21,642,259,792.

Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora (OR-MUUUB) imekamilisha maandalizi ya Mradi wa Tanzania ya Kidijitali ambao ni wa mkopo wa Benki ya Dunia na kufanikisha kusainiwa rasmi tarehe 19 Agosti, 2021 kisha kuanza kutekelezwa mwezi Novemba, 2021.

Mradi huu utagharimu jumla ya Dola za Marekani milioni 150 na utatekelezwa kwa miaka mitano. Wizara kwa Kushirikiana na wadau wengine imeanza taratibu za ujenzi wa Kituo cha Wataalam wa TEHAMA ili kuongeza ubunifu na kuwajengea utaalam.

Katika kipindi hicho, Wizara imekamilisha ujenzi wa jengo la kituo cha kurushia matangazo ya masafa ya FM katika kituo cha Kisaki mkoani Morogoro; kukamilika kwa ujenzi na ufungaji wa mitambo ya kituo cha Redio ya Jamii Makao Makuu Jijini Dodoma; kukamilika kwa taratibu za ununuzi wa wazabuni wa kufunga mitambo ya masafa ya FM katika mikoa mipya ya Njombe, Songwe na Simiyu, sambamba na wilaya za Kilwa, Serengeti pamoja na visiwa vya Unguja na Pemba; kuboreshwa na kufungwa kwa mitambo yenye vifaa vya kisasa katika studio za redio zilizoko Barabara ya Nyerere; kuendelea na ufungaji wa mitambo ya masafa ya FM katika Wilaya za Karagwe, Same, Bunda, Kasulu, Kahama, Nkasi na Sikonge ambapo utekelezaji wake umefikia asilimia 80; kuendelea na ujenzi wa mitambo ya masafa ya FM katika Wilaya za Ngara, Kyela, Ruangwa, Kilombero na Ludewa ambapo utekelezaji wake umefikia asilimia 95; kuendelea na ujenzi wa mitambo ya masafa ya FM katika wilaya za Tanganyika/Mlele, Makete, Uvinza, Mbinga na Ngorongoro ambapo utekelezaji wake umefikia asilimia 70.

Taarifa hiyo inaeleza kuwa Wizara imeendelea shughuli za kutangaza na kuhabarisha wananchi kuhusu utekelezaji wa Sera, Mipango, Mikakati, Miradi na program mbalimbali za Serikali ambapo Wizara kupitia Idara ya Habari - MAELEZO imeendelea kuuhabarisha Umma kuhusu utekelezaji wa kazi za Serikali kwa kuandaa vipindi mbalimbali vinavyoangazia utekelezaji wa Miradi mbalimbali unaofanywa na Serikali ya Awamu ya Sita vikiwemo vipindi vya KAZI IENDELEE kinachorushwa na TBC 1, Channel Ten na Televisheni mbalimbali za mtandaoni zimekuwa zikirusha kipindi hicho.

Aidha, Wizara kupitia Idara ya Habari iliandaa Makala Maalum ya Televisheni kuhusu Mafanikio, Mwelekeo na Changamoto za Serikali katika Sekta mbalimbali katika kipindi cha Miaka 60 ya Uhuru wa Tanzania Bara, kuchapisha Jarida maalum la NCHI YETU kuhusu mafanikio ya Miaka 60 ya Uhuru, kutoa Jarida Mtando la NCHI YETU la kila Wiki, Vipindi mbalimbali katika Televisheni Mtandao ya MAELEZI TV, kuratibu Waheshimiwa Mawaziri kuongea na Vyombo vya Habari kuelezea mafanikio ya Miaka 60 ya Uhuru wa Tanzania Bara.

Kazi hii imefanyika kwanza kwa kununua vitendea kazi vikiwemo kamera, kompyuta na visaidizi (accessories) na kuvitumia kuandaa video fupi, vibango na makala maalumu kwa ajili ya matangazo ya televisheni na mitandao ya kijamii pamoja na makala maalumu zilizochapishwa kwenye magazeti mbalimbali na jarida maalumu.

Wizara imeshiriki katika mkutano wa PAPU uliofanyika Zimbabwe tarehe 21-25 Juni, 2021 ambapo Tanzania ilipata nafasi ya kupenyeza nia yake ya kugombea katika nafasi za uongozi katika Umoja wa Posta Duniani (UPU).

Katika mkutano huo uliofanyika tarehe 9 – 27 Agosti, 2021 chaguzi mbalimbali za viongozi na mabaraza zilifanyika na Tanzania kufanikiwa kushinda katika nafasi ya Baraza la Utawala na Baraza la Utendaji wa Umoja wa Posta Duniani (Council of Administration).

Kazi ya Mabaraza haya ni kuendesha shughuli za Umoja wa Posta Duniani ikiwa ni pamoja na kupitisha Bajeti za Umoja na kupitisha miradi ambayo itatekelezwa na Nchi wanachama wa Umoja huo. Faida tutakayopata kwa Nchi kuwepo kwenye Baraza nchi kuwa na fursa ya kunufaika na misaada ya kitaalam, vifaa, kuwakilisha mawazo ya nchi mbalimbali ambazo ni mwanachama wa umoja hususani Kusini mwa Afrika.

Hakika katika kipindi cha mwaka mmoja wa Serikali ya Awamu ya Sita mafanikio maridhawa yamepatikana kupitia Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari hususani Ujenzi wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano, Mradi wa Tanzania ya Kidijitali, Mradi wa Mfumo wa Anwani za Makazi na Postikodi, Upanuzi wa Usikivu wa Shirika la Utangazaji Tanzania (TBC) na Elimu kwa Umma.


MFUMO WA ANWANI ZA
MHESHIMIWA SAMIA SULUHU HASSAN,
OFISI YA RAIS, IKULU,
1 BARABARA YA JULIUS NYERERE,
40400 CHAMWINO - DODOMA.



KAZI
OFISI YA WAZIRI MKUU,
MJI WA SERIKALI-MTUMBA
1 MTAA WA KAZI,
40480 DODOMA.


Posta
Let's Go!








OptiX OSN 9800 M12
SUB RACK 01 - DWDM _MASASI<>MTAMBASWALA
HUAWEI






# Mwaka Mmoja Awamu ya Sita Madarakani Sekta ya Ujenzi Yazidi Kuimarika

Na **Segolena Francis**
**Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi**

Tanzania inapoadhimisha mwaka mmoja wa Rais Samia Suluhu Hassan madarakani, juhudi za Serikali ya Awamu ya Sita za kuboresha miundombinu ya usafiri zinajidhihirisha. Miradi mikubwa ya ujenzi wa barabara, madaraja, vivuko na reli inazidi kutengewa fedha nyingi na kuifanya iendelee kutekelezwa kwa kasi.

Mnamo tarehe 22 Aprili 2021 Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Samia Suluhu Hassan, alihutubia Bunge la 12 ila Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dodoma kwa kuelezea Bunge pamoja na Watanzania kwa ujumla Dira na Mwelekeo wa Serikali ya Awamu ya Sita.

Katika hotuba hiyo Mhe. Rais alieleza dhahiri nia yake ya kudumisha mazuri ya Awamu zilizopita, kuyaendeleza mema yaliyopo na kuleta mengine mapya na kufafanua kuwa, kimsingi ndiyo dhana na maana halisi ya kaulimbiu/salamu ya "Jamhuri ya Muungano wa Tanzania – Kazi Iendelee".

Mhe. Rais alieleza kuwa ili kuchochea shughuli za kiuchumi na uzalishaji katika sekta ya kilimo, viwanda, madini na utalii atahakikisha anaendeleza jitihada za kuimarisha miundombinu ya usafiri ambayo ni moyo wa ukuzaji uchumi.

Alieleza kuwa, kwenye miaka mitano iliyopita, jitihada kubwa zilifanyika za kuimarisha usafiri wa barabara, reli, maji na anga hali iliyowezesha kujengwa kwa jumla ya kilometa 3,537 za barabara za lami pamoja na madaraja makubwa 12 na hivyo aliahidi kukamilisha ujenzi wa madaraja makubwa, likiwemo la JPM, Kigongo – Busisi, Wami na Tanzanite.

Sekta ya Ujenzi inaendelea kutekeleza kwa vitendo juhudi hizo za Mhe. Rais na hivi karibuni tumeshuhudia kukamilika na kuanza kutumika kwa daraja jipya la Tanzanite lililopo mkoani Dar es Salaam lenye urefu wa kilomita 1.30 na barabara unganishi zenye urefu wa kilomita 5.2 lililogharimu kiasi cha shilingi bilioni 243.

Daraja hili ambalo linapita baharini kuunganisha eneo la Agha Khan pamoja na Coco Beach linajumuisha njia 4 za magari pamoja na njia 2 za watembea kwa miguu limepunguza kwa kiasi kikubwa changamoto ya foleni ambayo daraja la zamani la Selander lilizidiwa kutokana na kuongozeka kwa shughuli za kibinadamu katikati ya Jiji la Dar es Salaam.

Aidha, Rais Samia Suluhu Hassan ameendelea kuelekeza fedha kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya kimkakati ikiwemo ujenzi wa daraja la JPM katika eneo la Kigongo-Busisi mkoani Mwanza ambalo limefikia zaidi ya asilimia 33.68 ambapo hadi kukamilika kwake mwaka 2024 litagharimu shilingi bilioni 716.33.

Mradi mwingine uliobainishwa katika hotuba hiyo ni ujenzi wa Daraja jipya la Wami lenye urefu wa mita 510 na upana wa mita 11.85 ambalo limezingatia sehemu ya barabara za magari, watembea kwa miguu na vizuizi kwa ajili ya usalama linalotarajiwa kupunguza ajali katika eneo la Mto Wami na kuhuisha huduma za usafiri na uchukuzi katika Barabara Kuu ya Chalinze - Segera.

Ujenzi wa daraja jipya la Wami unajumuisha ujenzi wa barabara za maingilio ya daraja kwa pande zote mbili zenye jumla ya urefu wa kilomita 3.8 ambapo kilomita 2.1 zimegawanywa upande wa Kusini wa daraja na upande wa Kaskazini kilomita 1.7 ambapo gharama ya mradi wa ujenzi huo ni Sh. bilioni 72 ikiwa ni fedha za malipo ya mkandarasi na mhandisi – mshauri. Ujenzi kwa sasa umefikia asilimia 75.57.

Serikali iliamua kuanza ujenzi wa daraja hili kutokana na daraja lililopo lenye urefu wa mita 88.75 lililopo sehemu ya Barabara Kuu ya Chalinze – Segera (Km 47.80 kutoka Chalinze) lililojengwa mnamo mwaka 1959 ambalo kiungo muhimu kati ya jiji la Dar es Salaam na Mikoa ya Kusini kuelekea/kutoka Mikoa ya Kaskazini na Nchi za Jirani kutokidhi mahitaji ya magari yanayopita kwa kuwa lilijengwa miaka mingi iliyopita na ni jembamba lenye njia moja.

Aidha, barabara zinazounganisha daraja hili ziko kwenye miinuko mikali na kona mbaya hivyo ajali mbaya na vifo vimekuwa vikitokea mara kwa mara katika eneo la daraja.

Wizara (Ujenzi) imeendelea kutekeleza



miradi mbalimbali ya ujenzi na ukarabati wa barabara nchini ambapo hivi karibuni Rais Samia Suluhu Hassan amezindua mradi wa ujenzi wa barabara ya mzunguko wa nje (Outer Ring Road) yenye urefu wa Kilomita 112.3 katika Jiji la Dodoma itakayogharimu shilingi bilioni 249 ambazo ni gharama za ujenzi na ulipaji fidia kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huo.

Barabara hii ambayo ni kichocheo cha ukuzaji wa uchumi imesanifiwa kuwa na umbali wa km 20 kutoka katika ya jiji la Dodoma imegawanywa katika sehemu mbili sehemu ya kwanza inayopita eneo la Veyula – Mtumba hadi Bandari kavu ya Ihumwa yenye urefu wa km 52.3 na sehemu ya pili inayoanzia Bandari kavu ya Ihumwa kupitia Matumbulu hadi Nala yenye urefu wa km 60.

Mradi huo unatarajia kupunguza msongamano wa magari katikati ya jiji la Dodoma na hivyo kuwezesha magari yanayosafiri katika barabara ya Ushoroba wa kati (Central Corridor) na Ushoroba wa barabara Kuu ya Kaskazini Great North Corridor (Trans – Africa 4) unaoanzia Cape Town Afrika Kusini hadi jiji la Cairo nchini Misri kupita kwa urahisi katikati ya jiji la Dodoma.

Vilevile, miradi ya barabara ya Malagarasi – Uvinza (km 51.1), Maswa – Bariadi (km 49.7), Bagamoyo – Horohoro – Lungalunga-Malindi; sehemu ya Pangani – Tungamaa inaendelea kujengwa kwa kiwango cha lami na ipo katika hatua mbalimbali za kukamilika kwake.


Aidha, miradi mingine ya barabara ipatayo 25 imepata kibali cha kuanza ujenzi wake kwa kiwango cha lami ambayo ni barabara ya Ntendo – Muze – Kilyamaundu (km 200); sehemu ya Ntendo – Muze (km 37), Isyonje – Kikondo – Makete (km 96.2); sehemu ya Ipelele – Iheme (km 36.3), Karatu – Mbulu – Hydom – Sibiti River – Lalago – Maswa (km 389); sehemu ya Mbulu – Hydom (km 50), Kibaoni – Sitalike (km 71), Bigwa – Matombo – Mvuha (km 78), Matai – Kasesya (km 50),Tarime – Mugumu (km 86), Mpanda, Mishamo – Uvinza (km 159); sehemu ya Vikonge – Mishamo Jct (km 62.35), Kibondo – Mabamba (km 48), Noranga – Itigi – Mkiwa (km 56.9), Handeni – Kibereshi – Kijingu – Kibaya – Njoro – Olboti –Mrijo Chini – Dalai – Bicha – Chambalo – Chemba – Kwa Mtoro – Singida (km 460); sehemu ya Handeni – Kiberashi (km 50), Kitai – Lituhi (km 85) na Daraja la Mnywamaji.

Barabara nyingine ni Itoni – Ludewa – Manda (km 211.4); sehemu ya Itoni – Lusitu (km 50), Mianzini – Ngaramtoni (km 18), TAMCO – Vikawe – Mapinga (km 24), Ibanda – Itungi (km 26), Omugakorongo – Kigarama – Murongo (km 50), Sengerema – Nyehunge – Kahunda; sehemu ya Sengerema – Nyehunge (km 54). Nzera – Nkome (km 20), Same – Kisiwani – Mkomazi (km 97), Ubena Zomozi – Ngerengere (km 11.6) fakara – Kihansi (km 50) na Kibada – Mwasongwa – Tundwisongani – Kimbiji (km 41).

Sambamba na miradi hiyo, Serikali inaendelea na ujenzi pamoja na uboreshaji wa viwanja vya ndege katika mikoa mbalimbali nchini. Hatua za utekelezaji wa miradi hiyo ni kama ifuatavyo:- Kiwanja cha Ndege cha Songea (asilimia 95), Mtwara (asilimia 85), Iringa (asilimia 33.42), Musoma (asilimia 04), pamoja na ujenzi wa jengo la abiria katika kiwanja cha ndege cha Songwe (asilimia 81), ufungaji wa taa za kuongozea ndege (asilimia 49) na ujenzi wa tabaka la juu la barabara ya kuruka na kutua ndege (asilimia 94.44).

Aidha, kuhusu Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Msalato Mkoani Dodoma ulipaji fidia umekamilika kwa asilimia 98, mkataba wa awamu ya kwanza unaohusisha ujenzi wa barabara ya kuruka na kutua ndege, maegesho ya ndege umesainiwa mwezi Septemba, 2021 na mkandarasi tayari amekabidhiwa eneo la mradi mwezi Januari, 2022.

Ni matumaini ya Serikali kwamba miradi hii inayotekelezwa kwa kutumia fedha nyingi za kodi za Watanzania itatunzwa vyema kwa ajili ya kizazi cha sasa na vizazi vijavyo ili kuboresha hali ya sasa ya maisha ya Watanzania na kukuza uchumi wa Taifa kwa Ujumla.




MV. MBEYA II
MV MBEYA II









# Mwaka Mmoja Awamu ya Sita Utekelezaji Miradi ya Nishati Washika Kasi

## Uzalishaji wa umeme wafikia Megawati 1,721.55 kutoka Megawati 1609.55 za awali

## • Ifikapo Desemba, 2022, vijiji vyote 12,345 vya Tanzania Bara kufikiwa na huduma za umeme

Na **Mwandishi wetu**
**WIZARA YA NISHATI,**

Sekta ya Nishati imekuwa na mchango mkubwa katika kukuza maendeleo ya uchumi wa Taifa. Katika kipindi cha mwaka mmoja cha Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mhe. Rais Samia Suluhu Hassan, Sekta ya Nishati imepiga hatua kubwa katika nyanja ya umeme, gesi asilia na mafuta, nishati jadidifu, miradi mkubwa kama wa Julius Nyerere, Bomba la Mafuta la Afrika Mashariki na Majadiliano ya Mradi wa LNG.

Kwa mujibu wa taarifa ya Wizara ya Nishati, katika kipindi cha mwaka mmoja wa Uongozi wa Serikali ya Awamu ya Sita chini ya Mhe. Rais Samia Suluhu Hassan, Tanzania imefanikiwa kupiga hatua katika masuala ya mafuta na gesi kwa kutekeleza miradi mbalimbali ya utafutaji, usafishaji, uagizaji na usambazaji.

Aidha, Wizara imetekeleza miradi ya kimkakati ikiwemo, Mradi wa Utafutaji wa Mafuta katika Vitalu Eyasi Wembere & Mnazi Bay Kaskazini, Mradi wa Kuchakata na Kusindika Gesi Asilia (Liquefied Natural Gas - LNG), Mradi wa Bomba la Kusafirisha Mafuta Ghafi Kutoka Uganda hadi Tanzania (East African Crude Oil Pipeline - EACOP), Mradi wa Kusafirisha Gesi Asilia kutoka Tanzania kwenda nchini Kenya na Mradi wa Kusafirisha Gesi Asilia kutoka Tanzania kwenda Nchini Uganda.

Mradi mwingine unaotekelezwa kwa Awamu ya Sita ni wa Bomba la Kusafirisha Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP) kutoka Hoima - Uganda hadi Chongoleani mkoani Tanga – Tanzania, unatekelezwa na wawekezaji binafsi (TOTAL-Ufaransa na CNOOC-China) kwa kushirikiana na Serikali ya Tanzania na Uganda kupitia Kampuni za Taifa za masuala ya mafuta na gesi.

Mradi huo unajumuisha ujenzi wa bomba lenye kipenyo cha inchi 24 na urefu wa kilomita 1445, vituo sita (6) vya kusukuma mafuta na viwili (2) vya kupunguza kasi ya msukumo wa mafuta, maghala matano yenye ujazo wa mapipa 500,000 kila moja na ghati la kupakia mafuta ghafi na litakuwa na uwezo wa kusafirisha mapipa 216,000 kwa siku.

Ujenzi utakapokamilika, bomba hilo litakuwa na mfumo wa kupasha joto mafuta ghafi ili kuwezesha mafuta kusafirishwa kwa urahisi zaidi. Bomba hilo linatarajiwa kuwa ndilo lenye urefu zaidi duniani lenye mfumo wa namna hiyo. Gharama za awali za Mradi zinakadiriwa kuwa Dola za Kimarekani bilioni 3.5.

Katika kipindi cha uongozi wa Rais Samia Suluhu Hassan mafanikio makubwa yamepatikana katika utekelezaji wa mradi huo ikiwa ni pamoja na kusainiwa kwa mikataba miwili ya mradi baina ya Serikali na Kampuni ya wabia. Mikataba hiyo ni Mkataba wa Wabia wa Mradi (Shareholders Agreement) uliosainiwa tarehe 11 Aprili, 2021 na Mkataba Hodhi (Host Government Agreement) uliosainiwa tarehe 20 Mei, 2021.

Mengine ni kuridhiwa kwa ushiriki wa 15% wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika mradi. Hadi sasa Serikali imetoa jumla ya Shilingi bilioni 259.96 kama



sehemu ya ushiriki wake katika mradi.

Serikali imekamilisha malipo ya fidia kwa wananchi watakaopisha ujenzi wa mradi katika maeneo 14 ya kipaumbele ambapo jumla ya Shilingi bilioni 2.286 zimelipwa kwa wananchi 351 katika maeneo yote ya kipaumbele.

Aidha, Serikali inaendelea kutoa elimu kwa wananchi kuhusu fursa mbalimbali zitakazotokana na ujenzi wa mradi. Jumla ya semina 6 zimefanyika katika maeneo ya Tanga, Misenyi, Chato na Nzega. Pia semina ya Wakuu wa Mikoa nane (8) inayopitiwa na mradi ilifanyika tarehe 27-29 Septemba, 2021 jijini Tanga. Katika kuendelea na utekelezaji wa mradi ujenzi wa coating yard umeanza katika kijiji cha Sojo Wilayani Nzega.

Mafanikio mengine yaliyopatikana katika kipindi cha mwaka mmoja wa uongozi wa Rais Samia Suluhu Hassan ni maandalizi ya utekelezaji wa Mradi wa Kuchakata na Kusindika Gesi Asilia (Liquefied Natural Gas – LNG mkoani Lindi katika eneo la Likong'o.

Mradi huu unalenga kuvuna, kuchakata na kusindika gesi asilia iliyogunduliwa kwenye kina kirefu cha Bahari ya Hindi katika Vitalu namba 1, 2 na 4 kuwa kimiminika ili iweze kuuzwa nje ya nchi na kutenga kiasi kingine kwa matumizi ya soko la ndani.

Mradi huo unatekelezwa kwa ushirikiano kati ya Serikali na Kampuni za Kimataifa zilizogundua gesi asilia katika vitalu husika.

Kampuni hizo ni Shell (60%), Pavillion (20%) na Ophir Energy (20%) kwa upande wa vitalu namba 1 na 4; na Kampuni ya Equinor (65%) na ExxonMobil (35%) kwa upande wa kitalu namba 2. Serikali imetenga eneo katika kijiji cha Likong'o mkoani Lindi lenye ukubwa wa Hekta, 2071 kwa ajili ya ujenzi wa mradi wa LNG. Mradi huo utajengwa katika eneo la Likong'o Mkoani Lindi na unatarajiwa kugharimu takriban Shilingi Trilioni 70.

Mafanikio yaliyopatikana katika Utekelezaji wa Mradi huo kwa kipindi cha Mwaka Mmoja wa Uongozi wa Mhe. Samia Suluhu Hassan ni pamoja na Serikali kukamilisha malipo ya Shilingi bilioni 5.71 kwa ajili ya fidia na riba kwa mujibu wa Sheria kwa Wananchi 642 waliopisha Mradi.

Aidha, wananchi 32 wataendelea kulipwa fidia baada ya kukamilisha taratibu za malipo na utambuzi. Serikali imemuajiri







Mshauri Mwelekezi, Kampuni ya Baker Botts ya Uingereza kwa ajili ya kuishauri Serikali katika majadiliano ambapo tarehe 25 Januari, 2022 mkataba ulisainiwa.

Maandalizi ya Majadiliano ya Host Government Agreement (HGA) yanaendelea ambapo Timu ya Majadiliano ya Serikali GNT imekamilisha Rasimu za Muundo na Muongozo wa Majadiliano (Negotiations Framework) pamoja na Nyenzo ya Majadiliano (Negotiation Brief) zinazotarajiwa kuongoza majadiliano ya HGA.

Mwaka mmoja wa Serikali ya Awamu ya Sita Serikali kupitia TPDC imeendelea kutekeleza miradi ya utafutaji wa mafuta na gesi asilia katika Vitalu vya Eyasi – Wembere kilichopo katika Bonde la Ufa la Afrika Mashariki na Mnazi Bay Kaskazini.

Mafanikio yaliyopatikana ndani ya mwaka mmoja wa Rais ni pamoja na jumla ya visima vifupi vitatu (3) vya utafiti (Stratigraphic Boreholes) vimechimbwa katika maeneo ya Kining'inila –Igunga, Tabora; Nyalanja-Meatu, Simiyu na Luono –Iramba, Singida.

Mafanikio mengine ni katika eneo la kutafuta soko la Gesi kwa nchi jirani, Serikali imeingia makubaliano ya awali (MoU) kwa ajili ya kujenga mabomba ya kusafirisha gesi asilia kwenda Kenya na Uganda. Kwa sasa majadiliano kwa ajili maandalizi ya miradi hii yanaendelea.

Suala jingine la kujivunia ni hali ya upatikanaji umeme nchini kwa ujumla inaendelea kuboreshwa. Hali hiyo imetokana na hatua zinazoendelea kuchukuliwa na Serikali za kukarabati miundombinu ya kuzalisha umeme, kusafirisha na kusambaza umeme.

Mafanikio yaliyopatikana ndani ya kipindi cha mwaka mmoja wa Mhe. Samia Suluhu Hassan ni pamoja uwezo wa mitambo ya kufua umeme iliyoungwa katika mfumo wa Gridi ya Taifa ulifikia Megawati 1,721.55 kutoka Megawati 1609.55 zilizokuwepo awali.

Mradi wa Rusumo MW 80 ambao umefikia asilimia 86 kutoka asilimia 80 za awali,Ujenzi wa Mradi wa kimkakati na kielelezo wa Julius Nyerere Hydro Power Project (JNHPP) Megawati 2,115 hadi mwezi Januari, 2022 utekelezaji wa mradi kwa ujumla ulikuwa umefikia asilimia 55.27, utekelezaji wa Mradi wa Kinyerezi I Extension 185MW – Mradi huu uliokuwa umesimama kwa muda mrefu uko katika hatua nzuri za utekelezaji na unatarajiwa kukamilika mwezi Agosti 2022, na utaongeza Megawati 185 katika Gridi ya Taifa na kukamilishwa kwa taratibu za miradi ya Upepo na Solar nchini.

Jumla ya miradi yenye Megawati 350 ya upepo na Solar ipo katika hatua za mwisho kabla mikataba haijasainiwa.

Mafanikio mengine katika eneo la usafirishaji umeme ni pamoja na kuendelea kutekelezwa kwa miradi ya Julius Nyerere - Chalinze 170km (400kV), Singida – Arusha – Namanga 414km (400kV), Geita – Nyakanazi 133km (220kV), Rusumo - Nyakanazi 95km (220kV), Dar es Salaam – Morogoro 160km (220kV) kwa ajili ya SGR, Morogoro – Dodoma – Singida, 400 kV, Iringa - Mbeya - Tunduma - Sumbawanga kilomita 624, Nyakanazi - Kigoma kilomita 280, Bulyanhulu - Geita kV 220 wenye urefu wa km 55, Mradi wa kuunga Tanzania na Zambia kwa msongo wa kV 400.

Usambazaji Umeme kupitia REA ni jambo jingine la kujivunia katika kipindi cha mwaka mmoja wa Uongozi wa Rais Samia. Katika eneo la umeme vijijini, kazi kubwa imeendelea kutekelezwa. Mradi wa kusambaza Umeme Vijijini wa Awamu ya Tatu, mzunguko wa kwanza, unaendelea na utapeleka umeme katika vijiji 3,559.

Hadi kufikia tarehe 30 Desemba 2021 jumla ya vijiji 3,340 na vitongoji 419 vimepatiwa umeme hivyo kufanya jumla ya vijiji na vitongoji 3,767 kati ya 3,978 sawa na asilimia 95. Aidha, jumla ya wateja wa awali 160,954 kati ya 227,561 sawa na asilimia 70.7 waliunganishiwa umeme.

Mradi wa Kusambaza Umeme Vijijini Awamu ya III Mzunguko wa II, unalenga kufikisha miundombinu ya msingi ya umeme katika vijiji 3,448 ambavyo havijafikiwa kabisa na miundombinu hiyo.

Aidha, vijiji 310 vilivyokuwa vimesahaulika vitapatiwa umeme kupitia mradi huu hivyo, mradi utakapokamilika mwezi Desemba, 2022, vijiji vyote 12,345 vya Tanzania Bara vitakua vimefikiwa na huduma za umeme.

Kuendelea kutekelezwa mradi wa kuongeza wigo wa usambazaji umeme wa ujazilizi fungu la pili, Mradi huu unalenga kusambaza umeme katika vitongoji ambavyo havijafikiwa na miundombinu ya umeme katika mikoa tisa (9) ya Dodoma, Singida, Shinyanga, Mwanza, Tabora, Kilimanjaro, Mbeya, Pwani na Tanga.

Hadi kufikia tarehe 30 Desemba 2021, vitongoji 323 kati ya 1,103 vilikuwa vimewashiwa umeme na wateja wa awali 3,200 wameunganishwa. Pia mradi huu utasambaza umeme katika vitongoji ambavyo havijafikiwa na miundombinu ya umeme katika mikoa kumi (10) ya Arusha, Geita, Kagera, Katavi, Kigoma, Lindi, Morogoro, Njombe, Simiyu na Songwe.

Aidha, ili kuendeleza juhudi za upatikanaji wa umeme nchini, Serikali imeendelea kuweka nguvu katika uzalishaji wa nishati jadidifu, umeme jua, joto ardhi, upepo na Tungamotaka kwa kuzingatia kwamba nishati ya gesi asilia na makaa ya mawe ni rasilimali zinazoisha, katika jitihada za kukabiliana na athari za mabadiliko ya Tabia nchi yanayoathiri vyanzo vya asili vya nishati, nishati jadidifu inatekelezwa kwa ajili ya kuhimili na kupunguza madhara yanayoweza kuathiri upatikanaji endelevu wa nishati.

Sekta za Nishati ni miongoni mwa sekta muhimu katika kuhakikisha kuwa Tanzania inafikia azma yake ya kuwa nchi ya viwanda. Serikali imepata mafanikio makubwa katika Sekta ya Nishati. Pamoja na mafanikio hayo, jitihada zinaendelea katika kuhakikisha Sekta za Nishati inachangia zaidi katika mapato ya Serikali, kipato cha mtu mmoja mmoja na wananchi kwa ujumla.













# Mwaka wa matokeo Sekta ya Madini

Na **Asteria Muhozya**
**Wizara ya Madini**

Mwaka mmoja wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Samia Suluhu Hassan madarakani umekuwa mwaka wa kazi na matokeo makubwa kwa Sekta ya Madini, ambapo Mhe. Rais ameendelea kuisimamia ipasavyo dhamira yake ya kuona Sekta ya Madini ikiakisi na kuendeleza thamani halisi ya rasilimali ambayo nchi imebarikiwa kuwa nayo. Yapo mengi ambayo yametekelezwa katika sekta ya madini lakini Makala hii inaangazia kwa uchache kile kilichofanyika kwa kipindi husika.

**UKUAJI WA SEKTA**

Chini ya uongozi wa Awamu ya Sita, mchango wa sekta ya madini katika Pato la Taifa umekuwa ukiongezeka mwaka hadi mwaka. Mwaka 2017 mchango wa sekta ulikuwa asilimia 4.4, mwaka 2018 asilimia 5.1, mwaka 2019 asilimia 5.2 na mwaka 2020 asilimia 6.5. Aidha, katika kipindi cha Juni hadi Septemba 2021 mchango wa sekta hii umefikia asilimia 7.3.

**MAFANIKIO**

Uongozi wa Mhe. Rais Samia ndani ya kipindi cha mwaka mmoja umeacha alama nyingi katika Sekta ya Madini miongoni mwake ni kuanzishwa kwa kiwanda cha kwanza nchini cha kusafisha madini ya dhahabu cha Mwanza Precious Metals Refinery chenye uwezo wa kusafisha kilo 480 za dhahabu kwa siku kwa kiwango cha kimataifa cha asilimia 999.9. Kiwanda hiki kilifunguliwa tarehe 13 Juni, 2022, na kinatajwa kuwa cha kwanza kwa ukubwa katika ukanda wa Afrika Mashariki na Kati. Dhahabu inayosafishwa kiwandani hapo, inaweza kununuliwa na benki yoyote duniani na kuwekwa kama amana ya Serikali.

Aidha, ndani ya kipindi cha mwaka mmoja wa Mhe. Rais Samia Madarakani, idadi ya masoko ya madini yaliyoanzishwa katika mikoa mbalimbali imefikia masoko 44 ya madini na vituo vya ununuzi wa madini vipatavyo 70. Pia, Serikali imeanzisha viwanda vingine vya kusafisha dhahabu katika mikoa ya Geita na Dodoma.

**UWEKEZAJI**

Mhe. Rais Samia anatamani kuiona Tanzania na wananchi kwa ujumla wanashiriki moja kwa moja katika uwekezaji kwenye sekta ya madini ili kuongeza tija na manufaa kwa Taifa. Ndani ya kipindi cha mwaka mmoja wa uongozi wake, tarehe 13 Desemba, 2021, dunia inashuhudia Serikali ya Awamu ya Sita chini ya Uongozi wa Mhe. Rais ikisaini mikataba minne (4) kwa wakati mmoja na kampuni za uwekezaji katika shughuli za uchimbaji mkubwa na wa kati wa madini yenye thamani ya uwekezaji wa dola za Marekani milioni 735.79. Kwa historia ya sekta ya madini, tukio kama hilo ni la kwanza kutokea na la aina yake kutokana na uwekezaji mkubwa ambao unakwenda kufanyika katika sekta ya madini. Uwekezaji huu unahusisha uchimbaji mkubwa na wa kati ambapo Serikali imeingia kwenye Mikataba hiyo ya uchimbaji madini Tanzania. Madini hayo ni kama vile madini mazito ya Viwandani (heavy mineral sands) yatokanayona mchanga wa Bahari, na madini ya teknolojia ya Rare Earth Elements (REE).

Kampuni zilizosaini Mikataba na Serikali ni pamoja na Kampuni ya Nyanzaga Mining Company Limited (NMCL), ambapo Mkataba husika umelenga kuanzishwa kwa mgodi wa uchimbaji mkubwa wa madini ya dhahabu na madini ambata kama vile shaba, chuma, nikeli, zinki na risasi kwenye eneo lenye ukubwa wa kilomita za mraba 23.36 katika Kijiji cha Sotta, Wilaya ya Sengerema, Mkoa wa Mwanza. Mkataba huu wa uchimbaji mkubwa unafungua ukurasa mwingine wa uwekezaji mkubwa baada ya kupita kipindi cha takribani miaka 15 tangu kuanzishwa kwa migodi mikubwa ya uchimbaji madini hapa nchini. Kupitia

Wilaya ya Sengerema, Mkoa wa Mwanza. Mkataba huu wa uchimbaji mkubwa unafungua ukurasa mwingine wa uwekezaji mkubwa baada ya kupita kipindi cha takribani miaka 15 tangu kuanzishwa kwa migodi mikubwa ya uchimbaji madini hapa nchini. Kupitia mkataba huo, imeundwa kampuni ya ubia ya Sotta Mining Corporation Limited kati yake na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambapo Serikali ina hisa asilimia 16 (non dilutable free carried interest) na kampuni ya Nyanzaga ina hisa asilimia 84. Aidha, uundwaji wa Bodi ya kampuni ya ubia ya Sotta umezingatia uwepo wa wajumbe wa Bodi kutoka Serikalini. Wajumbe hawa ni wawakilishi wa Serikalini katika maamuzi na usimamizi wa mradi huu wa uchimbaji dhahabu.

Mkataba mwingine uliosainiwa kati ya Serikali na wabia ni wa kampuni ya Jacana Resources Limited (Strandline Resources Limited) itakayochimba madini ya mchanga wa baharini (heavy mineral sand) kutoka kwenye Beach Sand katika eneo la Fungoni, Wilaya ya Kigamboni, Mkoa wa Dar es Salaam kwenye eneo lenye ukubwa wa kilomita za mraba 4.45.

Kwa kifupi, uchimbaji wa madini haya ya baharini ni wa kwanza kufanyika katika historia ya uchimbaji madini nchini. Kwa Afrika, nchi nyingine ambazo tayari zimeanza kuchimba madini haya ni Kenya na Msumbiji. Kupitia uwekezaji huu, mkataba wa kuundwa kwa Kampuni ya Ubia ya Nyati Mineral Sands Limited kati ya Serikali ya Tanzania yenye umiliki wa hisa asilimia 16 na Kampuni ya Jacana Resources Limited (Strandline Resources Limited) yenye hisa asilimia 84 ulisainiwa. Aidha, kama ambavyo aliahidi katika hotuba yake wakati alipolihutubia Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuhusu kuondoa vikwazo vya uwekezaji, Mheshimiwa Rais alishuhudia makubaliano mapya kati ya Kampuni ya Petra Diamond Ltd inayoendelea na uchimbaji wa madini ya Almasi katika mgodi wa Williamson Diamonds Limited eneo la Mwadui, Wilaya ya Kishapu, Mkoa wa Shinyanga.

Makubaliano hayo yaliendeleza kampuni ya ubia ya Williamson Diamond Limited ambapo Serikali ya Tanzania imeongeza umiliki kutoka asilimia 25 hadi kufikia hisa za asilimia 37 (non-dilutable shares) na kampuni ya Petra Diamond Limited hisa za asilimia 63. Mkataba huu unalenga kuboresha utendaji kazi katika kampuni hii na kutoa manufaa ya kutosha ya uchimbaji madini ya Almasi kwa nchi ya Tanzania. Kwa hakika Mhe. Rais ametimiza azima yake ili kuvutia na kurahisisha majadiliano kati ya Serikali na wawekezaji katika Sekta ya Madini. Kampuni nyingine iliyoingia mkataba na Serikali ni kampuni ya Black Rock Resources (Mahenge Resources) ambapo mkataba uliosainiwa unahusu uchimbaji mkubwa wa madini ya Kinywe (Graphite) katika eneo la Mahenge, Wilaya ya Ulanga, Mkoa wa Morogoro kwenye eneo lenye ukubwa wa kilomita za mraba 19.73. Kutokana na mkataba huu, imeundwa kampuni ya ubia ya Faru Graphite Corporation Limited kati ya Serikali ya Tanzania ambayo itakuwa na hisa zipatazo asilimia 16 na Mahenge Resources Limited (Black Rock Mining Limited) hisa asilimia 84.

Vilevile, mbali na kampuni hizo kusaini Mikataba hiyo na Serikali, Oktoba 27, 2021 Serikali ya Mhe. Rais Samia ilitoa Leseni ya uchimbaji mkubwa wa Madini ya nikeli kwa kampuni ya ubia ya Tembo Nickel Corporation na kuifanya Tanzania kwa mara ya kwanza kuanza kuchimba madini hayo baada ya shughuli za utafiti wa madini hayo kuchukua takribani miaka 33. Uchimbaji wa madini ya nikeli utafanywa katika wilaya ya Ngara mkoa wa Kagera.

Mbali na manufaa ya kodi na maduhuli ya Serikali katika uwekezaji huo, manufaa mengine ni pamoja na ajira, kuifungamanisha sekta ya madini na nyingine kiuchumi, kurithisha teknolojia za kisasa na utalaamu, kuvutia mitaji na hatimaye kuongeza mchango wa sekta ya madini kwenye Pato la Taifa. Ni dhahiri kwamba, kwa uwekezaji huu, lile lengo la mchango wa Sekta ya madini kwenye Pato la Taifa kufikia asilimia 10 ifikapo mwaka 2025 litafikiwa.

Mbali ya mikataba hiyo, ipo pia Kampuni ya PRNG Minerals Limited ya Australia inayokusudia kufanya uchimbaji mkubwa wa madini ya Rare Earth Element mkoani Songwe. Wakati wa kusaini mikataba hiyo, Mhe. Rais alitoa nafasi ya kukamilishwa kwa majadiliano baina ya Serikali na Kampuni hiyo kuelekea katika hatua ya kutolewa kwa leseni ya uchimbaji mkubwa wa madini ya REE. Ikumbukwe kuwa, Tanzania ni moja ya nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki ambayo ina rasilimali madini nyingi yakiwemo madini haya ya REE ambayo yameifanya kuwa miongoni mwa nchi tano zenye akiba kubwa zaidi za aina hiyo ya madini duniani.

Madini ya REE Tanzania kupitia mradi wa Ngualla chini ya kampuni hiyo yanatajwa kuwa ni yenye ubora wa kiwango cha juu ikilinganishwa na mengineyo duniani. Madini ya REE yanatumika katika matumizi mengi ya teknolojia ikiwemo kutengeneza simu za mkononi, kompyuta na kuendesha magari yanayotumia umeme.

## MAZINGIRA YA UWEZESHAJI

Awamu ya Sita inaendelea kuchukua hatua za kuhakikisha Tanzania inakuwa kitovu cha biashara ya madini barani Afrika kwa kuweka mazingira wezeshi ya biashara ya madini. Moja ya hatua hizo ni marekebisho ya Sheria ya Fedha ya Mwaka 2021 inayogusa madini na hivyo kufanikisha kuondolewa kwa Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) na ushuru wa Forodha kwa madini yanayoingizwa nchini kwa ajili ya kuuzwa kwenye masoko ya madini na katika viwanda vya kusafisha dhahabu.

Hadi sasa kuna jumla yamasoko 44 na vituo vya ununuzi wa madini vipatavyo 70 vilivyoanzishwa katika mikoa mbalimbali nchini vikiwemo viwanda vitatu vya kusafisha dhahabu katika mikoa ya Mwanza, Geita, na Dodoma. Hii ni fursa ya kuruhusu biashara ya madini na nchi nyingine duniani.

## UTENDAJI WA WIZARA NA TAASISI

Serikali ya Awamu ya Sita imeendelea kuliimarisha Shirika la Madini la Taifa (STAMICO) ili liweze kushiriki kikamilifu kwenye shughuli za madini ndani na nje ya nchi. Shirika hilo linaiwakilisha Serikali katika miradi mbalimbali ikiwemo mradi wa kiwanda cha kusafisha dhahabu mwanza. Aidha, ikilinganishwa na hapo awali, Shirika hilo sasa lina uwezo wa ushindani na kampuni za kigeni kiasi cha kufanikiwa kupata kandarasi kubwa za uchorongajii kwenye sekta ya madini kwa taasisi za umma na binafsi ambapo shirika limefanya uchorongaji katika mgodi wa dhahabu wa Geita (GGML) na Kampuni ya Uendelezaji Jotoardhi (TGDC).

Vilevile, shirika hilo limesaini mikataba na benki mbalimbali nchini kwa ajiliya kuwasaidia wachimbaji wadogo kupatiwa mikopo na kuwaunganisha na benki hizo. Benki ambazo zimeingia makubaliano hayo ni Benki ya NMB, KCB na CRDB. STAMICO imeweza kununua mtambo maalum wa kutengeneza makaa ya mawe kwa matumizi ya nyumbani na kuwarahisishia watanzania kupata nishati mbadala yenye ufanisi na bei nafuu. Mtambo huu unaitwa Rafiki Coal Briquette Plant. Aidha, baada ya Serikali ya awamu ya Tano kufanikiwa kuhamishia Makao Makuu kutoka Dar es salaam kuja Dodoma, Serikali ya awamu ya Sita chini ya uongozi shupavu wa Rais Samia umeziwezesha wizara na taasisi mbalimbali ikiwemo wizara ya madini kuanza ujenzi wa jengo jipya la wizara eneo la Mtumba katika mji wa Serikali utakaogharimu kiasi cha shilingi bilioni 22. Hadi sasa ujenzi upo katika hatua


Kwa mafanikio hayo hakuna shaka kuwa, katika kipindi cha mwaka mmoja wa Mhe. Rais Samia madarakani umekuwa mwaka wa matokeo makubwa yanayoonekana katika Sekta ya Madini.























# Upekee wa Tanzania mapambano dhidi ya Uviko-19

Na **Catherine Sungura**
**Wizara ya Afya**

Tanzania imewekeza jitihada madhubuti za kupambana na ugonjwa wa UVIKO-19, kwani nayo ni miongoni mwa nchi zilizoathiriwa na ugonjwa huo, janga ambalo bado lipo ulimwenguni.

Mwaka jana akizungumza na Watanzania, Rais Samia Suluhu Hassan alisema Serikali ya Jamhuri wa Muungano wa Tanzania ilipatiwa mkopo wenye masharti nafuu wenye thamani ya shilingi trilioni 1.3 kutoka Shirika la fedha Duniani (IFM).

Fedha hizo ni kwa ajili ya Kampeni Maendeleo ya Ustawi wa Taifa na Mapambano dhidi ya UVIKO-19. Wizara ya Afya iliidhinishiwa kupokea jumla ya shilingi bilioni 493 ikiwa sawa na asilimia 38 ya fedha zote.

"Fedha hizi zimetengwa kwa ajili ya kutekeleza afua mbalimbali za kukabiliana na athari za UVIKO-19, ikiwemo kuboresha miundombinu ya hospitali za Taifa, Rufaa za Mikoa, Kanda, Maalum, Taifa pamoja na vifaa," anabainisha.

## HUDUMA ZA DHARURA & ICU

Wizara imepanga kuendelea kuimarisha huduma za dharura na wagonjwa mahututi (Critical Care) ndani na nje ya Vituo vya Kutolea Huduma ambapo kiasi cha shilingi bilioni 279.6 sawa na asilimia 57 ya fedha hizo.

Maeneo yafuatayo yanahusika ili kupunguza vifo na kuboresha huduma kwa wagonjwa wenye matatizo ya UVIKO-19, wajawazito, watoto na waliopata ajali, kuimarisha Miundombinu ya kutolea Huduma za Dharura (EMD) katika hospitali Maalum, Kanda, Rufaa za Mikoa na Wilaya.

Serikali inaenda kuimarisha huduma za dharura ambapo kiasi cha shilingi bilioni 116.1 kimetengwa na kati ya fedha hizi, shilingi bilioni 26.8 zitagharimu ukarabati wa vitengo vya huduma za dharura katika hospitali maalum nne.

Hospitali hizo ni hospitali nne za kanda na hospitali 22 za rufaa za mikoa, hospitali za wilaya 83 na shilingi bilioni 89.4 zitanunua vifaa katika vyumba hivyo.

## MAGARI YA WAGONJWA MAHUTUTI

Serikali inalenga kununua magari 243 ya kubebea wagonjwa mahututi (ambulances) kwa shilingi bilioni 47. 1 ambapo magari 195 yatakuwa yenye kiwango cha huduma ya msingi (basic life support) na 48 yenye huduma ya juu (advanced life support).

Magari haya yatasaidia kuokoa maisha ya wagonjwa wa UVIKO-19, wajawazito na waliopata ajali. Hii itaongeza idadi ya magari ya kubebea wagonjwa kutoka 479 yaliyopo sasa mpaka 722. Aidha, magari 195 ya kubebea wagonjwa ni kwa ajili ya hospitali za wilaya.

## VYUMBA VYA ICU

Serikali imepanga kufanya ujenzi na ukarabati wa vyumba vya wagonjwa mahututi na ununuzi wa vifaa katika Hospitali ya Taifa ya Muhimbili, Hospitali Maalumu tatu, Hospitali za kanda tano, Hospitali za Mikoa 28 na Hospitali za Wilaya 29.

Shilingi bilioni 69.6 zimetengwa ambapo shilingi bilioni 10.9 zitatumika kwa ajili ya ujenzi na ukarabati huku shilingi bilioni 58.6 zikinunua vifaa.

## HEWA TIBA YA OKSIJENI

Kupitia mkopo huu, Serikali imetenga shilingi bilioni 27.6 ili kuimarisha upatikanaji wa hewa tiba ya oksijeni kwa kusimika mitambo ya kuzalisha hewa tiba, manunuzi ya mitungi, vifaa wezeshi na mfumo utakaowezesha usambazaji wa hewa tiba kwa wagonjwa katika hospitali husika.

Shilingi bilioni 4.2 zitasimika mitambo saba ya kuzalisha hewa tiba katika Hospitali moja ya Kanda, Hospitali Maalum moja na Hospitali za Wilaya tano, hivyo itaongeza idadi ya mitambo ya kuzalisha hewa tiba ya Oksijeni kutoka 44 hadi 51.

Aidha, katika kuimarisha upatikanaji wa hewa tiba ya Oksijeni kwenye vituo vya kutolea huduma visivyokuwa na mitambo ya kuzalisha hewa tiba ya Oksijeni, shilingi bilioni 3.9 zitanunua mitungi 5,782 na shilingi bilioni 4.6 zitanunua vifaa wezeshi vya utoaji (flowmeters) hewa tiba katika Hospitali 116. Vilevile, shilingi bilioni 14.8 zitawezesha usambazaji wa hewa tiba ya Oksijeni katika Hospitali 76.

**DAMU SALAMA**

Wizara ya Afya imekua ikikusanya damu salama kutoka maeneo tofauti kwenye jamii kwa ajili ya kuokoa maisha hususani ya wajawazito na watoto. Katika kuimarisha upatikanaji wa damu salama, jumla ya shilingi bilioni 3.6 zimetengwa kuimarisha huduma za damu salama ambapo shilingi bilioni 2.1 zitanunua magari sita maalum kwa ajili ya huduma tembezi za ukusanyaji wa damu salama ambayo yatagawanywa kwa kila kanda.

Vile vile, Serikali inapanga kununua mashine za uchambuaji wa mazao ya damu salama (Apheresis machine with starter pack and Plasma Apheresis) zitazogharimu kiasi cha shilingi bilioni 1.5 kwa ajili ya Hospitali za Kanda. Hii itasaidia katika kuboresha matibabu kwa wagonjwa wa UVIKO-19 na wagonjwa wanaohitaji mazao maalum ya damu, pia itapunguza matumizi ya damu katika matibabu ya wagonjwa wa UVIKO-19 na wajawazito. Hii itaongeza mashine hizi kutoka moja mpaka kufikia 11.

**HUDUMA ZA UCHUNGUZI**

Kwa upande wa uimarishaji wa Huduma za Uchunguzi, Serikali inapanga kuboresha huduma za uchunguzi kwa kuimarisha huduma za uchunguzi wa mionzi, maabara na tiba mtandao (Telemedicine), shilingi bilioni 128.6 zinagharamia huduma hizi.

Hii itasaidia wataalamu wachache waliopo katika Hospitali za Kanda na Taifa kusoma majibu ya wagonjwa waliofanyiwa vipimo katika hospitali za Rufaa za Mikoa, Hospitali za Wilaya na vituo vya huduma za Msingi.

Vituo vikubwa vinne vyenye wataalamu bobezi na vituo 27 vya mawasiliano vitaanzishwa katika vituo vya kutolea huduma. Hii itaongeza vituo vikubwa kutoka vituo viwili hadi sita.

**X-RAY ZA KIDIGITAL**

Katika kuboresha huduma za vipimo vya radiolojia vinapatikana katika Hospitali zetu na kuepusha usumbufu kwa wananchi kulazimika kusafiri umbali mrefu kufuata huduma hiyo.

Serikali kupitia Wizara ya Afya inaenda kununua mashine za X-ray, CT-Scan, na MRI na zitafungwa kwenye hospitali zote kuanzia ngazi ya taifa, kanda na mikoa yote huku zikiwa zinafanyiwa marekebisho endapo zitaharibika katika kipindi cha miaka mitano kama ifuatavyo: Shilingi bilioni 35.7 zitatumika kununua na kusimika mashine 85 za X-Ray za kidigitali ambazo zitasimikwa katika Hospitali ya Taifa ya Muhimbili, Hospitali za Kanda mbili, Hospitali za Rufaa za Mikoa 20 na Hospitali za Wilaya 60. Hii itaongeza idadi ya X-Ray hizi kutoka 111 hadi 196.

Serikali itanunua na kusimika mashine 30 CT-Scan kwa jumla ya shilingi bilioni 69 kwa ajili ya Hospitali ya Taifa Muhimbili, Hospitali za Kanda (2), Hospitali maalum (2) na Hospitali 25 za Rufaa za Mikoa. Hii itaongeza idadi ya CT-scan kutoka saba mpaka kufikia 37.

Mashine nne za MRI zitanunuliwa na kusimikwa katika Hospitali za Kanda mbili, Hospitali ya Rufaa ya Mkoa mmoja na Hospitali Maalum moja zitakazogharimu shilingi bilioni 13.2. Hii itafanya idadi ya Hospitali zenye MRI kuongezeka kutoka tano mpaka tisa.

Fedha hizi zitawezesha Serikali kununua mashine saba za huduma za uchunguzi wa moyo (Detailed Echo Cardiography) zitaka-



zogharimu shilingi milioni 840. Hii itaongeza mashine za uchunguzi wa moyo (Detailed Echo Cardiography) kutoka moja hadi nane Serikali itatumia shilingi bilioni 4.3 kwa ajili ya kuimarisha Huduma za Tiba Mtandao (Telemedicine) ya huduma za uchunguzi kwa kujenga vituo vinne vya huduma za tiba mtandao (Telemedicine Hub) pamoja na gharama za usimamizi zinazogharimu shilingi bilioni 1.6.

**HUDUMA ZA MAABARA**

Katika kukabiliana na UVIKO-19 Serikali kupitia Wizara ya Afya itaendelea kuimarisha huduma za maabara kwenye vituo vya kutolea huduma za afya nchini ikiwemo maabara ya Taifa.

Kiasi cha shilingi bilioni 5.6 kinapangwa kuimarisha huduma za maabara ikiwa ni pamoja na ununuzi wa vitendanishi vya upimaji wa virusi vya UVIKO-19 katika maabara ya Taifa na maabara za Hospitali za Rufaa za Mikoa sita.

Aidha, kiasi cha shilingi milioni 300 kinapangwa kugharamia ununuzi wa mashine 10 za upimaji wa anuai za virusi vya UVIKO-19 na Saratani. Hii itawezesha ongezeko la vituo vinavyopima anuai za virusi vya UVIKO-19 kutoka vituo vinne hadi 14.

Pia fedha hizo zitaenda kununua machine za kusaidia kupumua (Ventilators) zipatazo 60, mashine za gesi ya damu, mashine za ultrasounds na nyinginezo ambazo zitasambazwa katika mikoa yote kuanzia ngazi ya taifa mpaka Halmashauri.

**UPATIKANAJI WA CHANJO**

Upatikanaji wa Chanjo ni kipaumbele kingine ambapo Serikali imelenga kuimarisha upatikanaji wa huduma ya chanjo ya UVIKO-19, kiasi cha shilingi bilioni 43.5 kimetengwa.

Kati ya hizo shilingi bilioni 5.3 zitagharamia ununuzi wa dozi 311,765 za chanjo ikiwa mahitaji yataongezeka na shilingi bilioni mbili kwa ajili ya gharama za uingizaji, utunzaji na usambazaji wa chanjo nchini.

Katika kuhamasisha na kuelimisha wananchi kuhusu umuhimu wa chanjo ya UVIKO-19, kiasi cha shilingi bilioni 36.2 kitagharamia uelimishaji na uhamasishaji wa chanjo ikiwemo manunuzi ya magari 214 ya huduma za chanjo kwa ajili Mikoa na Halmashauri, kampeni za kuhamasisha chanjo na mafunzo kwa watumishi ngazi ya jamii juu ya njia za kujikinga na UVIKO-19 ikiwemo kuhamasisha chanjo ya UVIKO-19.

Wizara ya afya kwa kushirkiana na OR-TAMISEMI imetekeleza hili la kuhamaisha wananchi kupata chanjo dhidi ya UVIKO-19 ambapo hadi sasa imezizndua kampeni mbili ambazo zimesaidia kuhamasisha wananchi nyumba kwa nyumba, mtaa kwa mtaa na kuwajengea uwezo wato huduma ngazi ya jmii nchini na hivyo kusaidia kuongeza asilimia za wananchi kupata chanjo hiyo.

**MABORESHO MIUNDOMBINU / NYUMBA ZA WATUMISHI**

Shilingi bilioni 28.5 zimetengwa kwa ajili ya kuboresha miundombinu katika vituo vya kutolea huduma, kati yake shilingi bilioni tano zitagharamia ukarabati wa Hospitali maalum moja na Hospitali za Rufaa za Mikoa tatu.

Shilingi bilioni 13.5 zimetengwa kwa ajili ya kugharamia ukarabati wa jumla ya nyumba 150 za watumishi katika hospitali za Rufaa za Mikoa 26 na Hospitali za Wilaya 124.

Vilevile, katika kuboresha huduma za magonjwa ya kuambukiza, Serikali inapanga kujenga vituo vya kutibu wagonjwa wa magonjwa ya mlipuko ya kuambukiza pamoja na ununuzi wa vifaa katika Mkoa wa Dar es Salaam na Kigoma vitakavyogharimu shilingi bilioni mbili.

**TAFITI**

Serikali imejipanga katika kufanya tafiti na operesheni mbalimbali, shilingi bilioni 2.5 zinapangwa kugharamia tafiti mbalimbali za UVIKO-19 na shilingi bilioni 9.2 zimetengwa kuwajengea uwezo watumishi, ufuatiliaji na usimamizi.












ZINGATIA
HUKU MAISHA YANAENDELEA




# Mwaka mmoja wa mageuzi Sekta ya Elimu

Na **Mwandishi Wetu**
**Wizara ya Elimu**

Wote tunajua Elimu ni ufunguo wa maisha na kwamba kuwekeza katika elimu inasaidia kizazi kilichopo na vizazi vingi vinavyokuja na ndio maana tangu tupate uhuru Mwaka 1961 Serikali za awamu zote zimekuwa zikiwekeza na kutoa kipaumbele katika Sekta ya Elimu.

Vivyo hivyo, Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Samia Suluhu Hassan imejipambanua kwa kuimarisha Sekta hii kwa kuongezea rasilimali ili kuimarisha ujifunzaji na ufundishaji na kuongeza fursa za upatikanaji wa elimu na mafunzo.

Katika Mwaka mmoja wa Mhe. Samia tumeshuhudia pia kupitia fedha za Mpango wa Maendeleo kwa Ustawi wa Taifa na Mapambano dhidi ya Uviko-19 ambapo Sekta ya Elimu ilitengewa Shilingi bilioni 368.9 ambapo Shilingi bilioni 64.9 zilielekezwa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa ajili ya kuimarisha ujifunzaji na ufundishaji kwa wanafunzi wenye mahitaji maalum, Elimu ya Ufundi, Mafunzo ya Ufundi Stadi na Elimu ya Ualimu.

**ELIMU JUMUISHI**

Serikali ya Awamu ya Sita toka iingie madarakani moja ya eneo iliyotoa kipaumbele katika sekta ni uhuishaji wa Mkakati wa Kitaifa wa Elimu Jumuishi wa Miaka Mitano, ambao umezingatia utoaji wa Elimu Jumuishi katika ngazi zote za elimu nchini.

Katika kutekeleza hili kwa mara ya kwanza imewekeza rasilimali nyingi katika kuhakikisha watoto wenye changamoto mbalimbali wanapata elimu kwa mfano fedha za UVIKO 19 kiasi cha Shilingi bilioni 1.4 zilitengwa kwa ajili ya watoto wenye mahitaji maalum katika Shule, Vyuo vya Ufundi na Vyuo Vikuu wa ajili ya ununuzi wa vifaa saidizi na vifaa vya kujifunzia ikiwemo vitabu vya nukta Nundu zaidi ya nakala elfu 21,000,000.

Wizara imekamilisha ujenzi wa Shule ya Sekondari Maalum iliyoko Patandi mkoani Arusha na inakamilisha na ujenzi wa Shule ya Msingi ya watoto wenye mahitaji maalum iliyopo Lukulezi mkoani Mtwara wilayani Masasi. Ndani ya mwaka huu mmoja walimu na wathibiti ubora zaidi ya 1,329 wamepatiwa mafunzo kwa ajili ya kubaini na kufundisha wanafunzi wenye mahitaji maalum.

**ELIMU YA UFUNDI**

Elimu ya Ufundi ni chachu ya kufikia uchumi wa juu wa kati kupitia viwanda. Sekta hii ndogo inachangia kuzalisha nguvukazi yenye ujuzi bila kusahau masuala ya teknolojia. Ili kufikia azma hii kwa kutoa fursa za elimu ya ufundi kwa usawa nchi nzima Serikali inajenga Vyuo vya VETA takribani 25 katika Wilaya. Serikali ya Awamu ya Sita imetoa Shilingi bilioni 28.7 kukamilisha ujenzi wa vyuo hivyo na kuviwekea samani na vifaa Kupitia fedha za mapambano dhidi ya fedha za UVIKO-19. Zaidi ya vyuo 25 vya wilaya, kuna vyuo vingine vinne vikubwa vya Mikoa ikiwemo, Simiyu, Geita, Njombe na Rukwa vinakamiliswa katika Mwaka huu mmoja wa Mhe. Rais Samia Suluhu Hassan.

Serikali pia imeona umuhimu wa kuongeza fursa hizi za Elimu ya Ufundi kwa kutoa zaidi ya Shilingi bilioni 19 kwa ajili ya ujenzi wa Chuo kikubwa cha aina yake cha Ufundi kinachojengwa Jijini Dodoma na kitachukua wanafunzi 3,000 ikikamilika Awamu ya kwanza ya ujenzi mwaka huu 2022.


**VYUO VYA MAENDELEO YA WANANCHI**

Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi (FDC) navyo havikuachwa nyuma katika Awamu ya Sita kwani navyo vimepatiwa kiasi cha Shilingi bilioni 3.6 kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa











miundombinu pamoja na ununuzi wa samani katika vyuo 12.

Vyuo hivi pamoja na kutoa ujuzi kulingana na mahitaji ya eneo husika pia ni sehemu muhimu sana kwa wanafunzi wanaomaliza darasa la saba na ambao hawakuweza kuendelea na mfumo rasmi wa elimu.

Katika vyuo hivi wanafunzi wanapata ujuzi na fursa ya masomo ya Sekondari. Kupitia uboreshaji unaoendelea kufanyika udahili na wahitimu wanaendelea kuongeza, mfano wanafunzi wanaohitimu kutoka 8,568 mwaka 2020 hadi 11,198 mwaka 2021.

**ELIMU YA JUU**

Katika kuendelea kuboresha Elimu ya Juu na kuongeza nafasi, Serikali ya Awamu Sita chini ya Mhe. Samia Suluhu Hassan kusaini Mradi mkubwa wa kimageuzi katika elimu ya juu, mradi wa "HEET" (Higher Education for Economic Transformation).

Mradi huu utatekelezwa kupitia mkopo nafuu wa takriban Shilingi bilioni 972 kutoka Benki ya Dunia na kwa ajili ya kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia kwa kujenga miundombinu katika Vyuo vya Elimu ya Juu, ikiwemo ujenzi wa Chuo Kikuu kipya cha Mwalimu Nyerere cha Kilimo na Teknolojia Butiama, Mradi huu utaongeza idadi ya wanafunzi wa elimu ya juu wanaosoma programmu za sayansi, Teknolojia na , Uhandisi na Hisabati (STEM) kutoka wanafunzi 40,000 , 2020 hadi kufikia wanafunzi 106,000 Mwaka 2026 na pia kutoa ufadhili wa masomo kwa Wahadhiri zaidi ya 623 katika ngazi ya Shahda za uzamivu (PHD) na Umahiri (MSc)

Katika kuondoa vikwazo vya kukosa elimu ya Juu kwa kukosa mkopo, Serikali ya Awamu ya Sita imeongeza bajeti ya fedha za mkopo wa Elimu ya Juu kutoka Shilingi bilioni 464 hadi kufikia bilioni 570 na hivyo kuwezesha kuongeza wanafunzi wanaopata mikopo kutoka 149,398 2020/21 hadi 177,343 2021/22.

**UBORESHAJI MITAALA**

Mhe. Rais Samia Suluhu Hassan alipohutubia Bunge la Jamhuri ya Muungano tarehe 22/4/2021 alielekeza Wizara kupitia mitaala ya elimu katika ngazi zote ili kuhakikisha inaendana na wakati na inayomwezesha mwanafunzi anapohitimu kukabiliana na mazingira ya sasa.

Wizara kupitia Taasisi ya Elimu Tanzania (TET) inaendelea na mapitio ambapo kwa sasa inakamilisha upokeaji wa maoni ya wadau kupitia mikutano, makongamano, mitandao maalum ya kupokea maoni ikiwemo maoniyawadau@tie.go.tz na kuhusisha wadau katika ngazi zote, bila kusahau waajiri na hata wanafunzi.

Uwekezaji umefanyika katika kipindi cha Uongozi wa Awamu ya Sita pia upande wa Uthibiti wa Ubora wa ajili ya Idara ya Uthibiti Ubora wa Shule ili kuiwezesha kuzifikia shule nyingi zaidi kwa muda mfupi na kuhakikish ufundishaji na ujifunzaji unatekelezwa kwa ufasaha.

**FURSA YA KUREJEA SHULE WANAFUNZI WALIOKATISHA MASOMO**

Rais wa Awamu ya Sita, Mhe. Samia Suluhu Hassan amewezesha kuondoa vikwazo katika upatikanaji wa fursa za elimu kwa wanafunzi waliokatisha masomo kutokana na sababu mbalimbali. Serikali kupita Waraka wa Elimu Na 2 wa Elimu wa mwaka 2022 imetoa fursa ya kurejea shule wanafunzi hao ambao ni pamoja na wasichana waliopata ujauzito wakiwa katika shule za msingi au sekondari.

**KUONGEZA MIUNDOMBINU YA ELIMUMSINGI**

Serikali kupitia mradi (SEQUIP) unaolenga kuongeza ubora wa elimu ya sekondari imeanza kujenga shule 1,000 za sekondari za kutwa na shule za sekondari 26 za wasichana. Utekelezaji huu umeanza katika kipindi cha Awamu ya Sita, kwa kujenga shule 274 za kutwa na shule 10 za Wasichana ambapo Serikali imetoa jumla ya Shilingi bilioni 1.4.



# Utalii waing'arisha Tanzania kimataifa mwaka mmoja Awamu ya Sita

Na **Aron Msigwa**
**Wizara ya Maliasili na Utalii**

Tanzania ni miongoni mwa nchi chache duniani zilizotenga maeneo makubwa kwa ajili ya shughuli za Uhifadhi wa wanyamapori, misitu na Malikale. Takribani asilimia 32.5 ya ardhi yote ya Tanzania sawa na Kilometa za mraba 307,873 imehifadhiwa chini ya usimamizi wa Wizara ya Maliasili na Utalii.

Maeneo haya yanahusisha Hifadhi za Taifa 22, Mapori ya Akiba ya Wanyamapori 22, Mapori Tengefu 29, Misitu ya Hifadhi za Mazingira Asilia 20, Hifadhi iliyohifadhiwa kisheria misitu 363, mashamba ya miti ya Serikali 23, maeneo Matatu (3) ya Ardhioevu chini ya Mkataba wa Ramsar, Jumuiya za Uhifadhi wa Wanyamapori 38 na Vituo vya Mambo ya Kale 133.

Maeneo haya yamekua na mchango mkubwa katika uchumi wa nchi kupitia shughuli za Utalii. Aidha, shughuli za kuhamasisha na kutangaza utalii ndani ya nchi na kwenye masoko mbalimbali ya Kimataifa zinazofanywa na Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Samia Suluhu Hassan zimekuwa na matokeo chanya na neema kubwa kwa nchi yetu ambapo vivutio vya utalii vya Tanzania vimepata umaarufu mkubwa na tuzo za Kimataifa.

Aidha, jitihada mahsusi za Rais Samia Suluhu Hassan katika kuitangaza Tanzania kimataifa kupitia programu maalum ya Royal Tour zimeifungua Tanzania na kuipa umaarufu zaidi Kimataifa. Mtandao maarufu wa habari nchini Marekani wa theGrio umetambua juhudi za Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Samia Suluhu Hassan katika kuiongoza vyema sekta ya utalii nchini na kuifanya Tanzania iwe kivutio cha kwanza cha utalii Barani Afrika kwa mwaka 2022.

Programu ya Royal Tour kwa ujumla imeanza kuleta matunda kwa kuvutia watalii na wawekezaji mbalimbali waje nchini. Mathalan, wakala wa utalii zaidi ya 30 kutoka katika nchi masoko ya utalii yakiwemo Marekani, Ufaransa na Lithuania wamehamasika kuitembelea Tanzania ili kujifunza na kujionea vivutio mbalimbali vya utalii kwa lengo la kuvitangaza katika nchi zao.

Vilevile, wawekezaji kutoka Taifa la Bulgaria wanakusudia kuwekeza katika huduma za malazi za hadhi ya kimataifa kwa kujenga loji nne (4) zenye hadhi ya nyota tano (5) ambazo zitaendeshwa na Kampuni ya Kempiski katika Hifadhi za Taifa za Serengeti, Manyara, Tarangire na Eneo la Hifadhi ya Ngorongoro hatua ambayo italeta matokeo chanya katika kuongeza idadi ya vyumba na wigo wa mnyororo wa huduma katika sekta ya utalii.

Katika hatua nyingine Wizara ya Maliasili na Utalii imeendelea kuimarisha utangazaji utalii kupitia njia mbalimbali ndani na nje ya nchi ambazo zimehusisha ushiriki wa Tanzania katika mikutano na makongamano makubwa ya kutangaza utalii duniani kutumia TEHAMA, Balozi zetu nje ya nchi, na Mabalozi wa Hiari wa Utalii yaani Tourism Goodwill Ambassadors kutangaza vivutio vya utalii vilivyopo nchini.

Aidha, juhudi za kutangaza utalii zimeendelea kuiletea neema Tanzania kwa Hifadhi ya Taifa ya Serengeti kuwa hifadhi Bora zaidi barani Afrika katika kwa miaka 3 mfululizo kuanzia 2019, 2020 na 2021 pia hifadhi za Taifa Kilimanjaro, Serengeti na Tarangire zimeshinda tuzo ya ubora ya mwaka 2021. Ushindi huu umekua chachu kwa nchi yetu kuendelea kufahamika duniani na kuongeza idadi ya watalii wanaoitembelea Tanzania.

Kwa upande mwingine Tanzania imeendelea kupata mafanikio makubwa katika utoaji wa huduma za utalii



kufuatia Shirika la Hifadhi za Taifa Tanzania (TANAPA) kutangazwa kuwa mshindi wa kundi la dhahabu miongoni mwa washindi 51 kutoka nchi 39 duniani wa tuzo ya Ubora wa huduma za viwango vya Kimataifa kwa mwaka 2020 iliyotolewa na European Society for Quality Research (ESQR).

Aidha, hifadhi 5 za Taifa ambazo ni Kilimanjaro, Serengeti, Mkomazi, Manyara na Arusha zimepata tuzo za huduma za viwango vya Kimataifa kwa mwaka 2020.

Mbali na mafanikio hayo Tanzania imeendelea kuwa mfano wa kuigwa na nchi nyingine katika shughuli za uhifadhi hatua iliyoiwezesha kupata Tuzo ya Ufanisi katika Uhifadhi na Utalii iliyotolewa na Serikali ya Jamhuri ya Sudan Kusini pamoja na Tuzo ya Utalii ya Bara la Afrika (Continental Tourism Award 2021) iliyotolewa na Bodi ya Utalii ya Afrika (African Tourism Board) wakati wa onesho la kwanza la Utalii la Jumuiya ya Afrika Mashariki (EARTE) lililofanyika Jijini Arusha Oktoba, 2021.

Aidha, mwaka 2021 Tanzania ilichaguliwa na taasisi inayoandaa tuzo za utalii duniani (World Travel Awards - WTA) kuwa nchi inayoongoza kwa shughuli za utalii Barani Afrika (Africa's leading destination for the year 2021) pamoja na Thanda Island, katika Kisiwa cha Shungi Mbili, Mafia kuchaguliwa na taasisi ya World Travel Awards kuwa Kisiwa Bora chenye Mandhari ya kuvutia zaidi Barani Afrika (Africa's Leading Luxury Island 2020 and The World's Leading Exclusive Private Island 2020).

Mbali na umaarufu huo Tanzania imeendelea kung'ara katika anga za kimataifa kufuatia Tripadvisor Travelers' Choice Destination – Africa kuziorodhesha Zanzibar na Jiji la Arusha kuwa miongoni mwa maeneo kumi bora ya shughuli za utalii Barani Afrika pia mtandao wa Safaribook-



ings.com mmumetoa orodha ya vivutio kumi (10) bora vya utalii vinavyofaa kutembelea katika Bara la Afrika kwa mwaka 2021/2022 na kuitaja Hifadhi ya Taifa ya Serengeti kuwa kinara kwa kuibuka kivutio namba moja. Aidha, katika orodha hiyo imo pia Hifadhi ya Taifa Mahale ambayo inasifika kwa utalii wa sokwe na ikolojia.

Kwa upande wa mikutano ya Kimataifa, mkutano wa Shirika la Utalii Duniani - Kamisheni ya Afrika (64th UNWTO-CAF) uliofanyika mwezi Septemba mwaka 2021 katika Kisiwa cha Sal, Cabo Verde, Tanzania ilichaguliwa kuwa Mwenyeji wa Mkutano ujao wa 65 wa UNWTO-CAF utakaofanyika kwa mara ya kwanza nchini mwezi Oktoba, 2022.

Pia katika Mkutano wa UNWTO uliofanyika Jijini Windhoek, Namibia tarehe 14 hadi 16 Juni, 2021 Tanzania ilichaguliwa kuwa mojawapo ya nchi tatu za Bara la Afrika ambazo zitahusika katika programu maalum ya uwekezaji na utangazaji utalii. Mbali na mafanikio hayo Baraza la Utalii Afrika (Africa Tourism Council-ATC) limeichagua Tanzania kuwa mwenyeji wa mkutano wake mkuu utakaofanyika Zanzibar mwezi Septemba mwaka 2022.

Aidha, Jumuiya ya Afrika Mashariki iliipa Tanzania heshima ya kuwa nchi mwenyeji wa Onesho la Kwanza la Kimataifa la Utalii la Jumuiya ya Afrika Mashariki (East African Regional Tourism Expo - EARTE 2021) lilofanyika kwa mafanikio Jijini Arusha kuanzia tarehe 9 hadi 16 Oktoba, 2021.

Pia Tanzania ilipewa heshima ya kuwa nchi pekee ya Kanda ya Afrika kushiriki mdahalo maalum wa mawaziri kuhusu masuala ya kisera ya uendelezaji utalii katika maeneo ya vijijini yaani Ministerial Debate on Policies to Foster Tourism for Rural Development. Mdahalo huo ulifanyika wakati wa Mkutano Mkuu wa 24 wa Shirika la Utalii Duniani (24th UNWTO General Assembly) Jijini Madrid, Uhispania ambapo Tanzania ilisisitiza uimarishaji wa uhifadhi na utalii endelevu.

Aidha, Tanzania ilipongezwa kwa mkakati wake wa kuendeleza utalii wa utamaduni na vyakula (cultural and gastronomy tourism) kupitia zao jipya la Swahili Tourism.

Katika hatua nyingine Tanzania imepewa heshima ya kuwa mwenyeji wa Shindano la Kimataifa la Mchezo wa Gofu la International Golf Tournament Challenge Tour kwa washiriki kutoka Bara la Ulaya (European Tour) linalotarajiwa kufanyika Jijini Arusha Tanzania tarehe 7 hadi 10 Aprili, 2022. Tukio hili ni fursa mojawapo ya kuendeleza zao la utalii wa michezo na kutangaza vivutio vingine.

















# Mwaka Mmoja Awamu ya Sita Tanzania Yaendelea Kuimarisha Amani na Utulivu

Na **Christina Mwangosi**
**Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi**

Katika kipindi cha mwaka mmoja wa Serikali ya Awamu ya Sita, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi ambayo katika jukumu lake la Usimamizi wa Usalama wa Raia na Mali zao limefanikiwa kuongeza ajira kwa askari ili kuboresha utendaji kazi, upandishwaji Vyeo kwa maafisa, askari na raia, mafunzo, ujenzi wa Ofisi, Vituo vya Polisi na Nyumba za Makazi kwa maafisa na askari wa Vyombo vya Ulinzi na Usalama vilivyoko chini ya Wizara hii ni miongoni mwa mafanikio hayo.

Yote haya yamesaidia kuimarisha Usalama wa Raia na Mali zao katika kipindi hiki hivyo kuifanya jamii ya watanzania na wageni kuendelea kushiriki shughuli za Maendeleo ya Kiuchumi, Kijamii wakiwa katika hali ya amani, usalama na utulivu. Katika Makala hii utafahamu mengi kutoka Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi.

## UIMARISHWAJI WA HALI YA ULINZI NA USALAMA

Katika kipindi cha mwaka mmoja Serikali ya Awamu ya Sita Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kupitia Vyombo vya Ulinzi vilivyo chini yake, imefanikiwa kuimarisha hali ya Ulinzi na Usalama, ambapo jumla ya askari 4,224 wa Cheo cha Mkaguzi Msaidizi wa Polisi wamepelekwa katika Kata zote Tanzania kwa ajili ya kusimamia suala zima la Ulinzi na Usalama wa raia na mali zao.

## AJIRA KWA ASKARI

Serikali ya Awamu ya Sita imeajiri askari 6,023 kwa ajili ya Vyombo vya Ulinzi na Usalama vilivyoko chini ya Wizara hii, ambapo Jeshi la Polisi limeajiri askari wapya 4,103, Jeshi la Magereza 700, Idara ya Uhamiaji 820 na Jeshi la Zimamoto na Uokoaji askari 400. Ajira hizi zilizotolewa katika Kipindi cha mwaka mmoja wa Serikali ya Awamu ya Sita zimesaidia kuboresha utendaji kazi kwa vyombo hivi, na hivyo kuimarisha na kurahisisha utekelezaji wa jukumu la Usimamizi wa Usalama wa raia na mali zao na kuifanya Nchi yetu kuendelea kuwa na usalama, amani na utulivu.

## UPANDISHWAJI VYEO

Upandishwaji Vyeo ni eneo mojawapo la mafanikio ambapo jumla ya Maafisa, Wakaguzi, askari na watumishi raia 34,698 walioko kwenye Vyombo vya Ulinzi na Usalama vilivyoko chini ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi walipandishwa vyeo mbalimbali katika kipindi cha mwaka mmoja Serikali ya Awamu ya Sita. Hatua hii, imeongeza morali ya utendaji kazi kwa wote waliopandishwa Vyeo hivyo kuleta tija katika utendaji kazi kwa Wizara hii.

## MAFUNZO

Mafanikio mengine ni mafunzo yaliyotolewa kwa maafisa na askari 34,000 wa vyeo mbalimbali kutoka kwenye Vyombo vya Ulinzi na Usalama vilivyoko chini ya Wizara hii, ambao wamehudhuria mafunzo mbalimbali kwa ajili ya kupanda vyeo katika Vyuo vya Vyombo hivyo hapa Nchini, jambo ambalo limeongeza uwezo wa kiutendaji na kuleta ufanisi katika utekelezaji wa majukumu ya maafisa na askari wa vyombo hivyo.

## UJENZI NA UBORESHAJI WA OFISI ZA MAKAO MAKUU NA MAKAZI YA MAAFISA NA ASKARI

Kukamilika kwa Ujenzi wa Ofisi za Makao Makuu ya Jeshi la Magereza na ujenzi wa Ofisi za Makao Makuu ya Idara ya Uhamiaji unaogharimu shilingi 20,283,091,685 unaoendelea jijini Dodoma ni miongoni mwa mafanikio yaliyopatikana katika kipindi hiki, Aidha, umefanyika ujenzi wa Ofisi za Makamanda wa Polisi katika Mikoa ya Mara, Njombe, Katavi, na Tarime ujenzi uliogharimu shilingi 5,919,288,400/= nyumba zaidi ya 15 za Makazi ya askari na Maafisa wa jeshi la Polisi na Vituo zaidi ya 13 vya Polisi zimejengwa katika Mikoa mbalimbali nchini ikiwemo ya

Mikoa ya Kusini Unguja, Kaskazini Unguja, Mkoa wa Kusini na Kaskazini Pemba.

Jeshi la Magereza limeendelea kukamilisha ujenzi wa nyumba za kisasa 119 zenye uwezo wa kuchukua familia 210 za Maafisa na askari wa jeshi hilo katika Mikoa mbalimbali nchini, sambamba na ujenzi wa Gereza jipya la Karatu, Kilosa Mkoani Morogoro. Serikali ya awamu ya Sita, imelipatia kiasi cha shilingi 4,352,434,000 kwa ajili ya ukamilishaji wa nyumba za Makazi ya askari wa jeshi hilo katika eneo la Kikombo ambao ukikamilika utachukua familia 80 ujenzi umefikia asilimia 65.

Aidha, Serikali ya Awamu ya Sita imewezesha ujenzi wa Kituo cha Zimamoto na Uokoaji Nzughuni Dodoma ujenzi wake umefikia asilimia 75. Aidha, Serikali imelipatia Jeshi la Zimamoto na Uokoaji shilingi bilioni 2,397,178,675 kwa ajili ya kukamilisha Ujenzi wa Kituo cha Zimamoto na Uokoaji TAZARA Mchicha Dar es Salaam.

Serikali ya awamu ya Sita imeiwezesha Idara ya Uhamiaji kuendelea kutekeleza ujenzi wa Ofisi za Uhamiaji katika Mikoa ya Geita, Mtwara, Lindi pamoja na ujenzi wa Kambi ya Mafunzo ya Uhamiaji ya Boma Kichakamiba mkoani Mtwara.

**MFUMO WA KIELEKTRONIKI WA KUSAJILI KAMPUNI ZA ULINZI NA WALINZI**

Katika kipindi hiki cha mwaka mmoja, Serikali imeiwezesha Wizara ya Mambo ya Ndani kupitia Jeshi la Polisi kuanzisha mradi wa kanzi data ambao hadi sasa umesajili kampuni za ulinzi 340 pamoja na walinzi 23,077, Mfumo huu utasaidia Serikali kufuatilia utendaji kazi wa walinzi wote kwa kuwa tayari wamechukuliwa alama za vidole zikiwemo taarifa za kina za mhusika.

**UHAMIAJI MTANDAO**

Katika kipindi cha mwaka mmoja wa Serikali ya Awamu ya Sita Idara ya Uhamaiaji kupitia Mfumo wa Uhamiaji Mtandao imefanikiwa kutoa hati za kusafiria za kielektroniki 60,726 kwa raia wa Tanzania waliohitaji kusafiri nje ya Nchi kwa madhumuni mbalimbali, Visa 317,653 zimetolewa kwa njia ya mtandao "e-Visa kwa wageni walioingia nchini, ambapo pia Vibali vya Ukaazi 16,533 vimetolewa kwa wageni walioingia nchini.

**USAJILI NA UTAMBUZI WA WANANCHI**

Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA) imefanikiwa kusajili wananchi 1,061,998 katika kipindi cha Serikali ya Awamu ya Sita hivyo kufanya jumla ya Wananchi 22,802,296 tangu kuanzishwa kwa Mamlaka hiyo. Katika kipindi hicho zimetolewa Namba za Utambulisho 1,335,298 hivyo kufanya Mamlaka kuwa imetoa jumla ya Namba za Utambulisho wa Taifa (NIN) 19,223,516 tangu kuanza kwa zoezi hilo.

**MAKUSANYO YA MADUHULI**

Katika Kipindi hicho Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, kupitia Jeshi la polisi limekusanya shilingi 61,519,176,593.87, Idara ya Uhamiaji kupitia huduma za utoaji wa pasipoti, Visa, Vibali vya Ukaazi na faini zinazotokana na operesheni mbalimbali imekusanya shilingi bilioni 147,257,712,898.69 ambapo NIDA imekusanya shilingi bilioni 20.5.

**NISHANI**

Katika kipindi cha mwaka mmoja wa Serikali ya Awamu ya Sita, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Samia Suluhu Hassan alitoa Nishani 268 zikiwemo za miaka 60 ya Uhuru, Utumishi wa Muda mrefu na tabia njema na Utumishi uliotukukavkwa Vyombo vya Ulinzi na Usalama vilivyoko chini ya Wizara hii, yaani Jeshi la Polisi, Magereza, Zimamoto na Uokoaji na Idara ya Uhamiaji na Jeshi.











# Siku 365 za kishindo cha Rais Samia Sekta ya Uchumi

Na **Benny Mwaipaja**
**Wizara ya Fedha na Mipango**

Ni siku 365 za kishindo cha Mhe. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Sita wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika Nyanja ya uchumi na maendeleo ya nchi kwa ujumla tangu ashike hatamu ya kuongoza nchi kwa mujibu wa Katiba, baada ya kifo cha aliyekuwa Rais wa Awamu ya Tano Hayati Dkt. John Pombe Magufuli.

Makala haya yanaangazia mafanikio ya kiuchumi yaliyopatikana katika kipindi cha mwaka mmoja wa Rais Samia kuwa madarakani kama mwananchi namba moja wa Taifa la Tanzania. Tunampongeza sana kwa uongozi wake mahili.

Kwa mujibu wa taarifa ya Wizara ya Fedha na Mipango, katika kipindi chake cha mwaka mmoja uchumi wa nchi umekua kwa wastani wa asilimia 4.9 kutoka 4.8 ambapo shughuli za madini ziliongoza kwa kuwa na ukuaji mkubwa wa asilimia 10.9, ikifuatiwa na shughuli za habari na mawasiliano asilimia 10.2, huduma nyingine za kijamii asilimia 9.8, umeme asilimia 9.7 na maji asilimia 7.0. Kuongezeka kwa kasi ya ukuaji huo kumetokana na jitihada mbalimbali zinazoendelea kuchukuliwa na Serikali yake ikiwemo utekelezaji wa mpango wa kukabiliana na athari hasi za UVIKO-19 pamoja na usimamizi madhubuti wa miradi mbalimbali ya maendeleo.

Taarifa hiyo inasema kuwa mafanikio hayo yanatokana na usimamizi wake pamoja na utekelezaji mzuri wa Bajeti ya Serikali ambapo katika kipindi cha nusu ya kwanza ya mwaka wa fedha 2021/22, Serikali ilitarajia kukusanya na kutumia jumla ya shilingi trilioni 18.24 na kufanikiwa kukusanya jumla ya shilingi trilioni 16.95 kutoka vyanzo vyote, sawa na asilimia 92.9 ya lengo.

Kwa upande ukusanyaji wa mapato, kuanzia Julai 2021 hadi Januari 2022, mapato ya ndani yakijumuisha mapato ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa yalifikia takribani shilingi trilioni 14.1 sawa na asilimia 92.5 ya lengo la kukusanya shilingi trilioni 15.2. Kati ya hayo, mapato yaliyokusanywa na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) yalikuwa shilingi trilioni 12.04 sawa na asilimia 92.8 ya lengo la kukusanya shilingi trilioni 12.99.

Katika kipindi hicho, Mhe. Rais Samia Suluhu Hassan aliiagiza Wizara ya Fedha na Mipango kuisimamia vizuri Mamlaka ya Mapato Tanzania kusimamia ukusanyaji wa mapato ya Serikali kwa weledi kwa kutowabughudhi wafanyabiashara ama walipa kaodi.

Baada ya maelekezo yake hayo, makusanyo halisi ya TRA yaliyokusanywa mwezi Desemba 2021 yalifikia shilingi trilioni 2.3 sawa na asilimia 103.1 ya lengo, ikiwa ni kiwango cha juu zaidi kuwahi kukusanywa na Mamlaka hiyo.

Mhe. Rais ameimarisha mahusiano ya kiuchumi na kidiplomasia na washirika wetu wa maendeleo zikiwemo taasisi kubwa za fedha duniani. Tangu ashike usukani wa kuiongoza nchi, Serikali imefanikiwa kupokea kiasi cha shilingi trilioni 1.9 kutoka kwa Washirika wa Maendeleo sawa na asilimia 135.2 ya lengo la shilingi trilioni 1.4 ambapo kati ya kiasi hicho, misaada na mikopo nafuu ya miradi ya maendeleo ni shilingi trilioni 1.7 sawa na asilimia 141.0 ya lengo.

Kiasi hicho kilichopokelewa ni kutokana na ahadi ya Washirika wa Maendeleo kuchangia katika bajeti ya Serikali ya mwaka 2021/22 shilingi trilioni 2.95 ikijumuisha misaada shilingi trilioni 1.14, na mikopo nafuu shilingi trilioni 1.82.

Aidha, kati ya fedha zilizoahidiwa, mifuko ya pamoja ya kisekta ni shilingi bilioni 282.3 na miradi ya maendeleo ni shilingi trilioni 2.7 ambazo zilipokelewa hadi Januari 2022.

Serikali yake ya Awamu ya Sita inaende-



lea kuimarisha na kuratibu juhudi za pamoja na Washirika wa Maendeleo za upatikanaji wa rasilimali fedha na uwekezaji kwa ajili ya kuwezesha utekelezaji wa Bajeti ya Serikali kwa kutekeleza Mwongozo wa Ushirikiano wa Maendeleo (DCF) pamoja na kusimamia misingi na sera mbalimbali za ushirikiano ikiwemo Kuratibu na kusimamia ratiba za majadiliano kati ya Serikali na Washirika wa Maendeleo, Kuhamasisha Washirika wa Maendeleo kuzingatia mifumo na vipaumbele vya Serikali katika utekelezaji wa Mpango na Bajeti pamoja na Kuzingatia misingi ya utawala bora na utawala wa sheria.

Serikali ya Awamu ya Sita imeendelea kusimamia vilivyo deni la Serikali ambalo hadi Desemba 2021, deni la Serikali lilikuwa shilingi trilioni 68.5 ikilinganishwa na shilingi trilioni 59 katika kipindi kama hicho mwaka 2020 ambapo katika kiasi hicho, deni la nje ni shilingi trilioni 47,399.5 na deni la ndani ni shilingi trilioni 21.1.

Ongezeko hilo limetokana na kupokelewa kwa fedha za mikopo kwa ajili ya kugharamia miradi mbalimbali ya maendeleo ikiwemo ujenzi wa miundombinu ya barabara, reli, viwanja vya ndege, umeme na maji pamoja na malimbikizo ya riba ya deni la nje, hususan nchi zisizo wanachama wa kundi la Paris Club ambazo Serikali inaendelea kujadiliana nazo. Pamoja na hayo tathmini iliyofanyika Novemba, 2021 imeonesha kuwa deni ni himilivu katika kipindi cha muda mfupi, wa kati na mrefu. Katika tathmini hiyo, viashiria vinaonesha kuwa thamani ya sasa ya deni la Serikali kwa Pato la Taifa ni asilimia 31.0 ikilinganishwa na ukomo wa asilimia 55 na thamani ya sasa ya deni la nje kwa Pato la Taifa ni asilimia 18.8 ikilinganishwa na ukomo wa asilimia 40.

Lakini Serikali ya Mhe. Rais Samia imeendelea kutekeleza mikakati mbalimbali ya kuhakikisha deni hilo linaendelea kuwa himilivu ikiwemo kuhakikisha mikopo inayopewa kipaumbele ni ile yenye masharti nafuu, mikopo yenye masharti ya kibiashara itaelekezwa katika miradi inayochochea kasi ya ukuaji wa uchumi na mauzo nje ya nchi pamoja na kuimarisha mikakati ya kukusanya kodi ili kuhakikisha sehemu kubwa ya bajeti inagharamiwa na mapato ya ndani pamoja na kupunguza matumizi yanayoweza kuepukika.

Mhe. Rais Samia Suluhu Hassan ameendelea kusimamia ipasavyo Mfumuko wa Bei ambapo katika kipindi cha Machi 2021 hadi Januari 2022, ulikuwa wa wastani wa asilimia 3.8 na kiwango hiki bado kipo ndani ya wigo wa kati wa asilimia 3.0 – 5.0 na lengo la nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki la asilimia 8.0. Serikali ya Awamu ya Sita imeweka mikakati mbalimbali ili kuhakikisha mfumuko wa bei hauendelei kuongezeka ikiwemo matumizi thabiti ya sera za bajeti na za fedha ili kuwa na kiasi cha fedha katika uchumi kinachotosheleza mahitaji ya soko bila kuathiri utulivu wa bei na kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji kwa kuhakikisha upatikanaji wa umeme wa uhakika ili kuhamasisha uzalishaji.

Katika kipindi chake cha mwaka mmoja, Thamani ya mauzo ya bidhaa na huduma katika kipindi cha Machi hadi Desemba 2021 iliongezeka na kufikia dola za Marekani milioni 8,696.8 kutoka dola za Marekani milioni 7,007.7 katika kipindi kama hicho mwaka 2020, sawa na ongezeko la asilimia 24.1.

Hii ilitokana na kuongezeka kwa mauzo ya bidhaa zisizo asilia pamoja na mapato ya

huduma hususan usafiri (travel) ikiashiria kuimarika kwa shughuli za utalii. Vile vile, thamani ya bidhaa na huduma zilizoagizwa kutoka nje zilifika dola za Marekani milioni 10,229.2 ikilinganishwa na kiasi cha dola za Marekani milioni 7,373.1 katika kipindi kama hicho mwaka 2020.

Mhe. Rais Samia Suluhu Hassan amesimamia ipasavyo Akiba ya Fedha za Kigeni, ambayo imeendelea kuwa ya kuridhisha na yenye kukidhi mahitaji ya fedha za kigeni kwa ajili ya uagizaji bidhaa na huduma nje ya nchi. Hadi Desemba 2021, akiba ya fedha za kigeni ilikuwa dola za Marekani milioni 6,386.0.

Kiasi hicho kinatosheleza uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje ya nchi kwa kipindi kisichopungua miezi 6.6, ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 4,767.7 katika kipindi kama hicho mwaka 2020, kiasi kilichotosheleza uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje ya nchi kwa kipindi cha miezi 5.6. Kiwango hiki ni zaidi ya lengo la miezi 4.0 la nchi, miezi 4.5 kwa nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki na miezi 6 kwa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika.

Serikali ya Awamu ya Sita pia imeendeleza usimamizi na utekelezaji mzuri wa sera za fedha na kibajeti, usimamizi kwenye kuhakikisha uwazi na utaratibu mzuri katika soko la kubadilisha fedha za kigeni, kuimarika kwa shughuli za utalii pamoja na uwepo wa akiba ya kutosha ya fedha za kigeni hali inaifanya Thamani ya Shilingi kuwa tulivu na thabiti.

Katika kipindi cha Machi hadi Desemba mwaka 2021, dola moja ya Marekani ilibadilishwa kwa wastani wa shilingi 2,297.6 ikilinganishwa na shilingi 2,295.2 kipindi kama hicho mwaka 2020. Hii inamaanisha kuwa, shilingi ya Tanzania dhidi ya dola ya Marekani ilipungua thamani kwa kiwango kidogo sana cha asilimia 0.1.

Katika Mikopo kwa Sekta Binafsi, usimamizi mzuri wa Serikali ya Rais Samia imeiwezesha mikopo hiyo kukua kwa kasi ambapo Hadi Desemba 2021, mikopo hiyo ilikua na kufikia shilingi trilioni 22.3 ikilinganishwa na shilingi trilioni 20.3 katika kipindi kama hicho mwaka 2020, sawa na ongezeko la asilimia 10.0 ikilinganishwa na ongezeko la asilimia 3.1 katika kipindi kama hicho 2020.

Aidha, sehemu kubwa ya mikopo kwa sekta binafsi imeendelea kuelekezwa kwenye shughuli binafsi, biashara, uzalishaji viwandani, pamoja na kilimo. Kuongezeka kwa







kasi ya ukuaji wa mikopo kwa sekta binafsi kunatokana na utekelezaji madhubuti wa sera ya fedha yenye kuongeza ukwasi katika uchumi sambamba na kupungua kwa mikopo chechefu. Katika kipindi kilichoishia Desemba 2021, mikopo chechefu ilipungua kufikia wastani wa asilimia 8.2 kutoka asilimia 9.8 Desemba 2020.

Vilevile Serikali ya Awamu ya Sita, chini ya uongozi thabiti wa Mama Samia Suluhu Hassan, iliandaa Mpango Mahususi wa Kukabiliana na Athari za Kijamii na Kiuchumi za UVIKO-19 (TCRP) katika sekta za kiuchumi na kijamii ambao uliwezesha Serikali kupata mkopo usio na riba kutoka Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF) wenye thamani ya shilingi trilioni 1.3 (dola za Marekani milioni 567.3).

Hadi Januari 2022, jumla ya shilingi bilioni 689.98 zilitolewa kwa ajili ya kugharamia ujenzi wa shule, vituo vya afya, miundo mbinu na ununuzi wa vifaa tiba, ukarabati, upanuzi na uongezaji wa miundombinu ya usambazaji wa maji pamoja na kuwezesha kaya masikini kupitia mfuko wa TASAF.

Waswahili wana msemo usemao nyota njema huonekana asubuhi. Umahili wa uongozi wa Serikali ya Awamu ya Sita umeonesha nuru ya kuendelea kuenzi jitihada za watangulizi wake wa kuhakikisha kuwa masuala ya uchumi yanasimamia vyema kwa ajili ya kuwaletea wananchi maendeleo ya haraka na kwa kasi ya ajabu. Pamoja na mafanikio hayo makubwa, moyo wake wa kujitoa kwa ajili ya maendeleo ya wananchi wake, pongezi nyingi zimwendee pamoja na wasaidizi wake wote.

Kazi inaendelea.









# Mwaka mmoja wa Rais Samia, Upatikanaji wa Maji waongezeka

## Shilingi bilioni 207 zaongezwa kwenye bajeti ya Maji

Na **Mwandishi Wetu**
**Wizara ya Maji**

Serikali ya Awamu ya Sita imeonyesha kazi kwa vitendo kwa kutekeleza miradi ya maji inayohudumia wananchi wote, mijini na vijijini. Serikali hii imeona maji ni hitaji na kimbilio la msingi la kila mtu hapa nchini, hivyo ni huduma ya kipaumbele. Serikali inaendelea kuwathamini Watanzania bila kujali itikikadi au eneo, na kutambua kuwa huduma ya maji ni moja ya sadaka kubwa hapa Duniani.

Tarehe 19 Machi 2021 Serikali hii ilianza kazi, kwa kuapishwa kwa Rais Samia Suluhu Hassan. Hivyo, Machi 19, mwaka huu Rais Samia anatimiza mwaka mmoja akiwa kiongozi wa nchi yetu.

Yapo mengi ya kujivunia ya uongozi shupavu wa kujituma wa Rais Samia katika kipindi cha mwaka mmoja tangu aingie madarakani. Haya yanaonekana katika sekta mbalimbali, ikiwamo maji.

Rais Samia amenukuliwa mara kadhaa akisema anatambua changamoto mbalimbali katika jamii, kwa mfano akina mama wa Tanzania katika baadhi ya maeneo wanavyotumia muda mrefu katika kuhakikisha uwepo wa maji kwa matumizi ya familia kwa muda wote. Katika kuthibitisha hilo, Waziri wa Maji Mhe. Jumaa Aweso mara kadhaa amesikika akisema kuwa Rais Samia humuita na kumuelekeza kuhakikisha changamoto ya huduma ya maji inapatiwa majibu kwa wananchi katika maeneo mbalimbali hapa nchini.

Serikali inayoongozwa na Rais Samia katika hili la kuwapatia wananchi huduma ya maji imedhamiria kwa vitendo. Rais Samia kwa uthubutu mkubwa na kuthamini Watanzania hasa akina mama ambao ndio waathirika wakubwa inapotokea upungufu wa huduma ya maji aliongeza fedha kiasi cha shilingi bilioni 207 katika bajeti ya shilingi bilioni 680 iliyoidhinishwa na Bunge la Bajeti kwa mwaka wa fedha 2021/2022. Ongezeko hili limesaidia kwa kiasi kikubwa miradi ya maji kutekelezwa kwa kasi na haraka.

Pamoja na hilo, jingine ni ununuzi wa mitambo ya kisasa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maji. Mitambo hii inanunuliwa kupitia Mpango wa fedha za Maendeleo kwa Ustawi wa Taifa na Mapambano dhidi ya UVIKO-19. Serikali katika utekelezaji huo iliamua kuelekeza kiasi cha shilingi Bilioni 139.4 ili kuhakikisha changamoto za huduma ya maji kwa wananchi zinapata majibu.

Waziri wa Maji Mhe. Aweso ananyambulisha matumizi ya fedha hizo kuwa ni; shilingi Bilioni 104.2 zimepangwa kutekeleza miradi ya majisafi 218, shilingi Bilioni 17.5 kununua seti 25 za mitambo ya kuchimba visima ambapo mitambo hii itasambazwa kwa kila mkoa hapa nchini. Bilioni 17.6 kununua seti tano za mitambo ya ujenzi wa mabwawa pamoja na seti nne za vifaa vya utafiti wa maji.

Matumizi ya vifaa hivi ni hatua kubwa ya utekelezaji wa miradi ya maji hapa nchini. Aidha, teknolojia ya matumizi ya vifaa hivi itapunguza gharama za utekelezaji wa miradi ikiwamo gharama ya kukodi mashine katika kutekeleza miradi.

Ndani ya mwaka huu mmoja Sekta ya Maji imezidi kung'aa kupitia Rais Samia. Nguvu na kasi ya utekelezaji wa miradi ya maji imeendelea kuwa kubwa. Tarehe 17 Oktoba, 2021 Rais Samia alipotembelea mradi mkubwa wa maji wa Jiji la Arusha unaogharimu kiasi cha shilingi Bilioni 520, akiwa katika kituo cha







kusukuma maji kilichopo eneo la Chekereni aliagiza Wizara ya Maji kuhakikisha kituo hicho kinapokea na kusambaza maji kwa wananchi kabla ya sikukuu ya Noeli ya mwaka 2021.

Kufuatia agizo hilo, Wataalamu wa Sekta ya Maji, pamoja na viongozi wake walipambana usiku na mchana kuhakikisha agizo linatekelezwa. Tarehe 23 Desemba, 2021 Katibu Mkuu wa Wizara ya Maji Mhandisi Anthony Sanga alishuhudia maji yakiingia katika kituo hicho, na kuwasha pampu tayari kwa kuanza kupata huduma ya majisafi na salama. Mradi huu unatarajia kukamilika itakapofika Juni 2022.

Mapema mwaka 2022, Rais Samia amekoleza moto zaidi katika Sekta ya Maji kwa kuweka jiwe la msingi la ujenzi wa miradi ya maji mkoani Mara, ukiwemo mradi wa maji unaoanzia mji mdogo wa Mugango, Halmashauri ya Wilaya ya Musoma kupitia Kiabakari hadi Butiama.

Mradi huu unagharimu shilingi bilioni 75. Mradi mwingine ukiwa ni mradi wa ujenzi wa chujio la maji la mji wa Bunda gharama yake ikiwa shilingi bilioni 10.

Yapo mengi, kwa mwaka mmoja wa Rais Samia madarakani. Sekta ya Maji imepiga hatua kubwa kwa kutekeleza miradi ya maji katika kuhakikisha wananchi kila kona ya nchi wanapata huduma ya majisafi.

Hatua imepigwa na kazi inaendelea katika kuhakikisha hakuna mwananchi anayeachwa katika kupata huduma ya majisafi, salama na yenye kutosheleza. Mambo mazuri yanazidi kuletwa na Serikali.



# Rais Samia aimarisha usawa wa kijinsia, ustawi na maendeleo ya jamii

Na **Mwandishi Wetu**
**Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum**

Katika mwaka mmoja wa uongozi wa Mhe. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Awamu ya Sita wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum imetekeleza masuala makubwa sita katika kuimarisha ustawi na maendeleo ya jamii nchini.

Moja ya masuala hayo ni katika kutekeleza ajenda ya usawa wa kijinsia, Wizara imefanikisha uzinduzi wa Kamati ya Ushauri ya Kitaifa ya Utekelezaji wa Ahadi za Nchi kuhusu Kizazi chenye Usawa (Generation Equality Forum - GEF) yenye lengo la kusaidia nchi katika malengo ya Jukwaa la Kizazi chenye Usawa, Tanzania imechagua kuwa kinara wa utekelezaji wa Eneo la Haki na Usawa wa Kiuchumi.

Katika kuimarisha usawa wa kijinsia kwenye uongozi, Serikali imeendelea kuhamasisha na kutoa elimu kuhusu fursa za kushirikisha wanawake katika nafasi na ngazi mbalimbali za uongozi. Jitihada hizi zimewezesha ongezeko la wanawake katika nafasi za uongozi na maamuzi. Kuanzia Machi 2021 hadi Februari 2022 idadi ya Mawaziri wanawake imeongezeka kutoka Mawaziri watano hadi kufikia Mawaziri tisa na Majaji kutoka 33 hadi Majaji 40. Jambo la pili Wizara katika mwaka mmoja wa Rais Samia, Wizara imeendelea kutekeleza Mpango Kazi wa Taifa wa Kutokomeza Ukatili dhidi ya Wanawake na Watoto (MTAKUWWA) wa mwaka 2017/18 mpaka 2021/2022.

Mambo muhimu yaliyotekelezwa chini ya Mpango huo ni pamoja na kuzinduliwa kwa Mwongozo wa Uanzishaji, Uendeshaji na Ufuatiliaji wa Madawati ya Jinsia katika Vyuo vya Elimu ya Juu na Kati umesaidia kuanzishwa kwa jumla ya Madawati sita katika Vyuo Vikuu sita kati ya Vyuo 50 vilivyokusudiwa katika kipindi cha Julai hadi Februari, 2022.

Katika kupambana na vitendo vya ukatili dhidi ya Wanawake na Watoto, Wizara ilizindua Mpango kazi wa "Kampeni ya Twende Pamoja, Ukatili Tanzania Sasa Basi" ngazi ya mkoa wenye lengo la kuimarisha utekelezaji wa MTAKUWWA ambapo hadi kufikia Februari 2021, jumla ya mikoa sita ya Dar es Salaam, Mara, Mwanza, Katavi, Kigoma na Dodoma imefanikiwa kuzindua mpango wa Kampeni hii.

Katika kuimarisha ulinzi wa wanawake na watoto dhidi ya vitendo vya ukatili, Serikali imeendelea kuratibu jitihada za kuimarisha ulinzi wa wanawake na watoto kupitia utekelezaji wa Mpango Kazi wa Taifa wa Kutokomeza Ukatili Dhidi ya Wanawake na Watoto (NPA VAWC 2017/18 2021/22). Jitihada hizi zimewezesha kuanzishwa kwa Kamati 1,843 na kufanya idadi ya kamati za Ulinzi wa Wanawake na Watoto kufikia 18,186 kuanzia ngazi ya Kijiji/Mtaa hadi Taifa.

Katika kuhakikisha Kada ya Maendeleo ya Jamii inatumika katika kusaidia kutatua changamoto katika jamii, Serikali imeendelea kuzalisha wataalam wa maendeleo ya jamii ambao ni muhimu katika kuchochea mabadiliko na kufanya mageuzi ya kifikra miongoni mwa jamii ili kuwawezesha wananchi kushika hatamu ya maendeleo yao. Mafunzo yanatolewa kuanzia ngazi ya astashahada hadi shahada ya uzamili.

Mwaka 2021/22, jumla ya wanafunzi 5,014 walidahiliwa kwa kufuata vigezo vilivyowekwa na Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi (NACTE) pamoja na Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania (TCU).

Aidha, jumla ya wanafunzi 4,500 walihitimu katika mwaka 2020/21 katika Taasisi ya Maendeleo ya Jamii Tengeru, Vyuo sita vya Maendeleo ya Jamii vya Buhare, Rungemba, Ruaha, Uyole, Mlale na Monduli pamoja na vyuo viwili vya Maendeleo ya Jamii Ufundi vya Misungwi na Mabughai.

Ili kuongeza thamani ya mafunzo yanayotolewa na vyuo vilivyo chini ya Wizara, programu za ujuzi (uanagenzi) zinazomuandaa mhitimu kujiajiri na kuajiriwa zimetekelezwa ambapo jumla ya vijana 721 kati ya 850 waliotarajiwa wamehudhuria mafunzo katika Taasisi mbalimbali, kati ya hao 114 wamehitimu ambapo 29 wamejiajiri na 13 wameajiriwa na makampuni mbalimbali kwa mwaka 2021/22.

Moja ya mahitaji muhimu kwa maisha ya binadamu ni malazi ambayo utokana na uwepo wa makazi bora, katika kuhakikisha hili linatokea Wizara imeanza kutekeleza Kampeni ya Ujenzi wa Nyumba Bora katika maeneo yenye makazi duni. Ujenzi wa nyumba hizo unatumia gharama nafuu kupitia mifumo ya asili ya kusaidiana miongoni mwa jamii. Mwongozo wa Uhamasishaji Ujenzi wa Nyumba Bora Ngazi ya Jamii wa Mwaka 2019 unalenga kufikia mikoa 26 ifikapo mwaka 2025.

Katika kipindi cha Machi 2021 hadi Februari 2022, kampeni hii imetekelezwa katika Mikoa tisa na hivyo kuvuka lengo la Mikoa mitano iliyopangwa. Aidha, nyumba zilizojengwa zimeongezeka kutoka nyumba 751 mwaka 2020 hadi kufikia nyumba 3,257 Februari 2022. Mikoa ambapo nyumba hizo zimejengwa ni Arusha, Morogoro, Songwe, Shinyanga, Pwani, Katavi, Singida na Mwanza.

Pia Vyuo vya Maendeleo ya Jamii vilivyo chini ya Wizara vimeanzisha Programu za ubunifu zinazotoa fursa kwa wanafunzi na jamii inayozunguka vyuo kufanya kazi za ubunifu unaosaidia kutatua changamoto mbalimbali, ikiwemo ajira zinaendelea kutekelezwa katika vituo tisa vya ubunifu wa kidigitali zimetekelezwa, ambapo jumla ya mawazo 52 yameibuliwa na yapo katika hatua mbalimbali.

Yapo mawazo ambayo yamefika mwisho, ikiwepo App ya kurekodi mauzo iliyobuniwa katika Taasisi ya Maendeleo ya Jamii Tengeru ambayo inatumika na wafanya biashara wa kati; App ya kupakua rejea ya vitabu kutoka kwenye kanzidata ya maktaba ya chuo bila kutumia internet katika Chuo cha Maendeleo ya Jamii Ufundi Mabughai; na pampu ya maji inayosukuma maji kwa kutumia maji yenyewe katika Chuo cha Maendeleo ya Jamii Mlale ipo katika majaribio.

Katika kukuza ustawi wa watoto nchini Serikali iliandaa na inatekeleza Ajenda ya Kitaifa ya Kuwekeza katika Afya na Maendeleo kwa Vijana Balehe nchini (2021/22 - 2024/25. Ajenda hii imejikita katika nguzo sita ambazo ni: - Kuzuia maambukizi ya Virusi Vya UKIMWI, Kutokomeza Mimba za Utotoni, Kuzuia ukatili wa Kimwili, Kisaikolojia na Kingono; Kuboresha lishe, Kuhakikisha Watoto wa Kike na Kiume wanabaki shule na Kuwajengea Vijana Balehe ujuzi na Uwezo wa Kufikia fursa za kiuchumi.

Katika kuimarisha makuzi jumuishi ya watoto ikiwa ni pamoja na ujifunzaji wa Awali, ulinzi wa mtoto, lishe bora, Elimu ya Afya Msingi na mawasiliano, Serikali imeandaa programu ya Malezi na Makuzi ya Watoto yenye lengo la kujenga vituo vya kijamii vya kulea Watoto wadogo mchana (Community Based ECD Centers).

Vituo hivi vinatarajiwa kujengwa katika Vijiji/Mitaa yote nchi nzima ambapo hadi kufikia Septamba 2021, jumla ya vituo 30 vimejengwa katika Halmashauri ya Temeke (5) na Kigamboni (5) katika Mkoa wa Dar es Salaam na Bahi (5), Kongwa (5), Chamwino (5) na Kondoa (5) katika Mkoa wa Dodoma.

Vituo hivyo vina lengo la kutoa huduma jumuishi za Malezi na Makuzi kwa watoto walio na umri kuanzia miaka 2 hadi chini ya miaka 5, ili kuwakuza watoto katika utimilifu wao kwa kuwapatia huduma jumuishi za afya, lishe, ulinzi, ujifunzaji na uchangamshi wa awali kabla ya kujiunga na darasa la awali anapofikia umri wa Miaka mitano.

Katika kuimarisha huduma kwa watoto walio katika Mazingira Hatarishi, Serikali kwa kushirikiana na wadau imekamilisha ujenzi wa Makao ya Watoto katika Eneo la Kikombo Mkoani Dodoma.

Makao haya yameanza kuchukua Watoto walio katika mazingira hatarishi ikiwemo wanaoishi na kufanya kazi mtaani ambapo hadi kufikia Februari 2022, kuna jumla ya Watoto 55 (Ke 21 na Me 34). Lengo ni kuwapatia huduma za msingi, kurekebisha tabia zao kwa lengo la kuwatengamanisha na kuwaunganisha na Familia zao.

Wizara katika kuhakikisha wazee wanakuwa na ustawi bora imeendelea kutekeleza Mkakati wa Kutokomeza Mauaji ya Wazee Nchini (2018/19-2022/23) ikiwa ni pamoja na kufuatilia afua zinazotekelezwa katika kuimarisha ulinzi na usalama kwa wazee. Lengo ni kutokomeza mauaji ya wazee nchini ifikapo mwaka 2023. Jitihada hizi zimesaidia kupunguza mauaji ya wazee kutoka 190 mwaka 2015 hadi kufikia 54 mwezi Februari, 2022.

Katika kuyatambua na kuyawezesha makundi Maalum Serikali anayoiongoza na Mhe. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alipofanya mazungumzo na viongozi wa Machinga Dar es Salaam na kutamka kuwa inawatambua Machinga kama Kundi Maalum na kwamba Shughuli zao zitaratibiwa chini ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum.

Aidha, Wizara imefanikiwa kuwakutanisha viongozi 10 wa Shirikisho la Umoja wa Machinga (SHIUMA) ngazi ya Taifa na viongozi 78 ngazi ya mikoa tarehe 22-23 Februari, 2022 jijini Dodoma. Katika kikao hicho, viongozi hao walipata mafunzo kuhusu utunzaji wa fedha, ujasiriamali, uongozi, fursa za mikopo na utii wa sheria bila shuruti. Vilevile Wizara ilifanikiwa kuwapatanisha viongozi wa SHIUMA Taifa na viongozi wa machinga mkoani Dar es Salaam ambao walikuwa na mgogoro wa muda mrefu.

Mashirika Yasiyo ya Kiserikali ni wadau muhimu wnaoshirikiana na Serikali katika kutatau changamoto za jamii katika maeneo tofauti nchini kwa kuzingatia hilo Wizara kwa kushirikiana na Baraza la Taifa la Mashirika Yasiyo ya Kiserikali (NaCoNGO) na wadau wengine imefanya mkutano wa mwaka wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali mnamo tarehe 30 Septemba, 2021 ambapo Mhe. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alikuwa mgeni rasmi na kuhudhuriwa na Mashirika na wadau 3,000.

Mkutano huo, ulitanguliwa na mafunzo kwa wadau wa Mashirika yaliyofanyika tarehe 29 Septemba, 2021 ambapo walijengewa uwezo juu ya Sheria, Kanuni na Miongozo inayosimamia Mashirika Yasiyo ya Kiserikali Tanzania Bara

Aidha, katika kusajili na kuuratibu Mashirika Yasiyo ya Kiserikali Wizara imetengeneza Mfumo wa Kielektroniki wa usajili wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali umekamilika kwa asilimia 100 ambapo umeshaanza kutumika. Mfumo huu umesaidia kuleta ufanisi katika usajili na uratibu wa Mashirika hayo.



# Serikali ya Awamu ya Sita yaipaisha Sekta ya Uvuvi

Na **Mwandishi Wetu**
**Mifugo na Uvuvi**

Sekta ya Uvuvi ni miongoni mwa sekta muhimu ambazo zimekuwa ni muhimili katika kutoa ajira na lishe bora kwa jamii hapa nchini. Mpaka sasa sekta hii inachangia uhakika wa upatikanaji wa chakula na lishe kwa asilimia 30, na ajira za moja kwa moja za wavuvi 195,435.

Kufuatia umuhimu huo, Serikali inayoongozwa na Mhe. Rais, Samia Suluhu Hassan tangu iingie madarakani imeendelea kuipa nguvu sekta hiyo kwa kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo ili sekta hiyo iendelee kutoa mchango mkubwa kwa Taifa.

Miradi hiyo imejikita kulinda rasilimali za uvuvi, kukuza sekta binafsi kupitia uwekezaji, kuwajengea uwezo wavuvi, kuboresha mazao ya uvuvi na miundombinu ya uvuvi, kufanya utafiti na kuboresha mfumo wa taarifa za uvuvi.

Mradi mmojawapo unaotekelezwa ni wa Usimamizi Shirikishi wa Rasilimali za Uvuvi Kusini Magharibi mwa Bahari ya Hindi– (Southwest Indian Ocean Fisheries Governance and Shared Growth - SWIOFish) ambao unalenga kuongeza faida za kiuchumi, kijamii na kimazingira ili kuwezesha uvuvi endelevu. Mradi huu umetekelezwa katika pande zote mbili za Muungano wa Tanzania kwa thamani ya Dola za Marekani milioni 36 ambapo Tanzania Bara ilipata Dola milioni 17.28, Serikali ya Mapinduzi Dola 11.52 na Mamlaka ya Kusimamia Uvuvi wa Bahari Kuu (DSFA) Dola milioni 7.2.

Mafanikio yaliyopatikana ni pamoja na Ujenzi wa miundombinu ya uvuvi ikiwemo Maabara ya Utafiti wa Uvuvi Dar es Salaam na Nyumba tatu za watumishi katika Hifadhi ya Bahari ya Silikanti Tanga (TACMP) na ofisi tano, pamoja na kuanzishwa kwa Vikundi vya Ulinzi Shirikishi wa Rasilimali za Uvuvi katika Halmashauri za Bagamoyo, Tanga Jiji, Mkinga, Pangani na Lindi Vijijini.

Aidha, pamoja na mafanikio mengine, kupitia mradi huo, mapambano dhidi ya uvuvi haramu yameimarika hususan uvuvi wa milipuko katika Ukanda wa Bahari ya Hindi ambao umepungua kwa kiasi kikubwa.

Mradi mwingine ni wa Kuwezesha Utekelezaji wa Programu ya Kilimo na Uvuvi (Agriculture and Fisheries Development Program-AFDP) unaogharamiwa na Mfuko wa Kimataifa wa Maendeleo ya Kilimo (IFAD). Dola za Marekani milioni 58.85 zinatekeleza mradi huo ambapo Sekta ya uvuvi imepangiwa jumla ya Dola za Marekani Milioni 34 kuanzia Julai 2021.

Kupitia mradi huo, sekta ya uvuvi itatumia shilingi bilioni 20 kununua meli nne za uvuvi kwa upande wa Tanzania Bara.

Kwa upande wa tasnia ya ukuzaji viumbe maji, Serikali inatekeleza miradi sita ya ujenzi wa vituo vya kuendeleza ukuzaji viumbe maji ikiwemo ujenzi wa Kituo cha Kuendeleza Ukuzaji Viumbe Maji Rubambagwe kilichopo Mkoa wa Geita unaogharimu shilingi bilioni tatu.

Miradi mingine ni ukarabati na utanuzi wa kituo cha Ukuzaji Viumbe Maji Ruhila kilichopo mkoani Ruvuma unaogharimu shilingi milioni 204 pamoja na ukarabati na utanuzi wa Kituo cha Ukuzaji Viumbe Maji Nyengedi kitakachogharimu kiasi cha Shilingi milioni 556.

Aidha, Serikali inaendelea na ujenzi wa Kituo cha Ukuzaji Viumbe Maji Bahari cha Ruvula kilichopo katika Mkoa wa Mtwara wenye thamani ya shilingi milioni 983 na Ujenzi wa

Kituo cha Ukuzaji Viumbe Maji Bahari Kunduchi kilichopo Dar es Salaam kwa thamani ya shilingi bilioni 1.645. Sambamba na hayo, Serikali inaendelea na ujenzi wa mashamba darasa ya ufugaji samaki katika Halmashauri 14 utakaogharimu shilingi milioni 715.

Kupitia Mamlaka ya Kusimamia Uvuvi wa Bahari Kuu (DSFA) kwa kushirikiana na Wizara zinazosimamia uvuvi (Bara na Zanzibar) imetekeleza mradi wa Usimamizi wa Uvuvi katika Ukanda wa Kusini Magharibi mwa Bahari ya Hindi (SWIOFish) na baadhi ya mafanikio yaliyofikiwa ni pamoja na kuandaa na kupitishwa kwa Sheria ya Kusimamia na Kuendeleza Uvuvi wa Bahari Kuu, Sura ya 388 ya mwaka 2020 iliyoridhiwa na Baraza la Wawakilishi. Sheria na Kanuni hizo zimechochea uwekezaji katika uvuvi wa bahari ambapo DSFA kuanzia mwezi wa Juni 2021 hadi sasa imekusanya Shilingi bilioni 2.4 na kutoa gawio kwa serikali (SMT na SMZ) ya asilimia 50 ya mapato hayo.

Pia, mradi wa Kutambua Maeneo yenye Samaki wengi Baharini (Potential Fishing Zone - PFZ) umewafaidisha wavuvi wadogo 3,360 katika maeneo ya mwambao wa Tanzania ikiwemo Mafia, Nungwi, Wete, Bagamoyo na Kilwa. Teknolojia hii imewasaidia wavuvi kupunguza kwa asilimia 50 gharama na muda wa kutafuta samaki.

Vilevile, Serikali imeratibu tafiti za uvuvi kwenye Bahari Kuu na Maji ya Kitaifa kuhusu mnyororo wa thamani, wingi wa samaki, maeneo ya mazalia ya samaki na hali za kimazingira ya bahari zinazochangia katika upatikanaji wa samaki. Tafiti hizo zimegharimu shilingi bilioni 1.7. Pia, Kuzijengea uwezo taasisi za utafiti na vyuo vikuu nchini kwa kutoa vifaa vya utafiti vyenye thamani ya shilingi milioni 360.

Serikali imewajengea uwezo wavuvi wadogo kwa kuwapatia vifaa vyenye thamani ya shilingi milioni 204 vya kuwawezesha kukusanya takwimu na kudhibiti uvuvi haramu kwa kusimamia sheria na kanuni na kuboresha mifumo ya kufuatilia mienendo ya meli na kufanya doria za anga kwa kushirikisha taasisi za Serikali ya Muungano na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.











# Mwaka Mmoja wa Serikali ya Awamu ya Sita, Amani, Usalama Vyatawala

## Vijana zaidi ya 9,341 Waajiriwa

Na **Lt. Col. Josephat Musira**
**Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa**

Kujenga Taifa ni jukumu la kuendelea kulinda Jamhuri ya Muungano wa Tanzania dhidi ya adui wa aina yoyote kutoka ndani na nje ya nchi kwa kuhakikisha kuwa mamlaka na maslahi mapana ya nchi yetu yanakuwa salama. Hivyo, Ulinzi na usalama ni tunu muhimu kwa maendeleo ya taifa lolote duniani ambayo inahitaji kulindwa kwa gharama yoyote.

Serikali ya Awamu ya Sita ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inayoongozwa na Mhe. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu imeendelea kuhakikisha tunu hiyo inalindwa kwa kuimarisha umoja, mshikamano na utulivu nchini.

Katika kipindi cha mwaka mmoja, Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa imefanikiwa kutekeleza majukumu yake ya msingi kwa weledi na mafanikio, hatimaye kuiwezesha nchi kuendelea kuwa na amani na utulivu.

Wizara kupitia Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ), imeimarisha ulinzi wa mipaka ya nchi yetu na imeendelea kuwa shwari. Hata hivyo, changamoto chache zimejitokeza katika baadhi ya mipaka ya nchi hususan katika mpaka wa Kusini na changamoto hizo zimeshughulikiwa ipasavyo na hali ya amani na utulivu imeendelea kuwepo.

Kwa upande wa mafunzo, JWTZ limeendelea kutoa mafunzo mbalimbali ya kijeshi katika Shule na Vyuo vya kijeshi ndani na nje ya nchi. Tarehe 17 Aprili, 2021 na 22 Novemba, 2021 Rais na Amiri Jeshi Mkuu alitunuku Kamisheni ya Kwanza na ya Pili ya Shahada ya Kwanza ya Sayansi ya Kijeshi (Bachelor of Military Science) mtawalia.

Shahada hii inatolewa na Chuo cha Mafunzo ya Kijeshi (TMA) kwa kushirikiana na Chuo cha Uhasibu Arusha (IAA) kwa ajili ya kuongeza weledi katika utendaji kwa Maafisa. Aidha, Wizara kupitia Chuo cha Ulinzi cha Taifa (NDC) inaendesha mafunzo ya Ulinzi na Stratejia ya muda mrefu na mfupi kwa Maafisa wa Vyombo vya Ulinzi na Usalama pamoja na Watumishi wa Umma.

Wizara inaendelea na Ujenzi wa miundombinu ya Makao Makuu ya Ulinzi wa Taifa (Kikombo - Dodoma) unaotekelezwa na wataalamu wa ndani kwa kugharamiwa na Serikali ambapo ujenzi huo umefikia asilimia 60. Vile vile, JWTZ imeendelea na ujenzi wa hospitali yake yenye hadhi ya Daraja la Nne kwa msaada wa Serikali ya Ujerumani ambayo inaendelea kujengwa eneo la Msalato Jijini Dodoma.

Wizara kupitia JWTZ, imeendelea kushirikiana na Umoja wa Mataifa (UN), Umoja wa Afrika (AU) na Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) katika Operesheni mbalimbali za Ulinzi wa Amani katika nchi zenye migogoro kwa kupeleka vikosi, waangalizi wa kijeshi, wanadhimu na makamanda. Mpaka sasa JWTZ ina vikosi vya ulinzi wa amani katika nchi za Lebanon, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo na Jamhuri ya Afrika ya Kati. Vile vile, nchini Msumbiji JWTZ inashiriki katika misheni ya SADC (SAMIM) ambapo inaisaidia kupambana na ugaidi.

Aidha, Jeshi lina Maafisa Wanadhimu, Waangalizi wa Kijeshi na Makamanda kwenye Operesheni za Amani nchini Lebanon, Sudan Kusini na Jamhuri ya Afrika ya Kati.

Vile vile, Wizara kupitia JWTZ imeendelea




kushiriki kikamilifu katika ulinzi wa baadhi ya miradi ya kielelezo nchini ikiwemo miradi ya Reli ya Kisasa (SGR) na Mradi wa Kufua Umeme wa Maji wa Julius Nyerere (JNHPP).

Aidha, JWTZ imeendelea kushiriki katika ulinzi wa maeneo ya kimkakati kwa nchi ikiwemo; Mgodi wa Tanzanite uliopo Mirerani, mkoani Manyara, Mamlaka ya Bandari Tanzania (TPA), Kampuni ya Simu Tanzania (TTCL) na maeneo ya viwanja vya Ndege ambapo Maafisa na Askari wa JWTZ wanashiriki kikamilifu.

Wizara kupitia Jeshi la Kujenga Taifa (JKT), imeendelea kutoa mafunzo ya awali ya kijeshi kwa vijana wa Mujibu wa Sheria na Kujitolea kwa lengo la kujenga uzalendo, ukakamavu na kutoa elimu ya stadi za kazi.

Vile vile, JKT imeendelea kutekeleza Mkakati wa Kilimo unaolenga kuongeza uzalishaji wa mazao na kujitosheleza kwa chakula ili kuipunguzia Serikali gharama.

Wizara kupitia JWTZ na JKT imeendelea kutoa huduma za matibabu kwa Maafisa, Askari, Vijana wa JKT, Watumishi wa Umma na Familia zao na Wananchi wanaoishi karibu na vituo vya tiba vya Jeshi hapa nchini. Wanufaika wakubwa wa huduma hizi ni wananchi kwa zaidi ya asilimia 80.

Aidha, Wizara imeendelea na maboresho ya Bima ya Afya Jeshini.

Wizara kupitia mashirika yake ya Tanzania Automotive Technology Centre (TATC) na MZINGA, imeendelea kufanya tafiti na uhawilishaji wa teknolojia kwa ajili ya kuzalisha bidhaa na huduma mbalimbali kwa matumizi ya kijeshi na kiraia.

Aidha, Serikali imepitisha Mpango wa Miaka Kumi (10) wa kuliimarisha Shirika la TATC ili liweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi. Pia, Wizara kupitia Shirika la Uzalishaji Mali la JKT (SUMAJKT), imeendelea kuipunguzia Serikali gharama za uendeshaji wa mafunzo ya Vijana wa JKT kupitia shughuli za ujenzi, viwanda, kilimo na mifugo, ulinzi na mradi wa matrekta na zana za kilimo.

Wizara imefanikiwa kutekeleza na kusimamia mikakati ya kupambana na maambukizi ya Virusi vya UKIMWI, kwa kutoa elimu ya jinsi ya kujikinga ili kuzuia maambukizi mapya na kupunguza vifo vitokanavyo na UKIMWI na Ugonjwa wa Virusi vya Korona (UVIKO -19).

Vile vile, Wizara inashiriki kutoa mafunzo kwa wataalamu mbalimbali wa tiba na kutoa ushauri nasaha kwa walioambukizwa na kuhimiza upimaji wa hiari kwa Maafisa, Askari, Vijana wa JKT na Watumishi wa Umma. Aidha, Kwa wale ambao wamethibitika kuwa na maambukizi ya Virusi vya UKIMWI wanaendelea kupatiwa dawa za kufubaza virusi katika Vituo vya Huduma na Matibabu na posho kwa ajili ya lishe.

Sambamba na hilo, kwa upande wa magonjwa yasiyoambukizwa jitihada mbalimbali zimekuwa zikifanyika ikiwemo kutoa elimu ya afya ili kupunguza magonjwa hayo na kupima afya mara kwa mara na kuwahimiza watumishi kufanya mazoezi.

Wizara kupitia Taasisi zake imefanikiwa kutunza fukwe katika mikoa ya Dar es Salaam, Tanga na Mtwara ili kuzuia mmomonyoko wa udongo. Mashirika yaliyo chini ya Wizara yameendelea na uzalishaji kwa kuzingatia sheria, kanuni na taratibu za uhifadhi wa mazingira. Uzalishaji huo hutumia njia za kisasa za kutibu maji yenye kemikali (water treatment) yanayotoka viwandani.

Sambamba na hilo, Wizara kupitia Shirika la TATC imefanikiwa kukamilisha utafiti wa mashine kwa ajili ya uzalishaji wa nishati mbadala. Mashine hizo ni za Agrowaste briquette na Coal briquette ambazo zinatumia mabaki ya mashambani, vyakula, vumbi la makaa ya mawe na udongo mfinyanzi kutengeneza mkaa.

Aidha, Shirika la MZINGA limefanikiwa kuzalisha zao la msingi kwa ajili matumizi vyombo vya Ulinzi na Usalama. Vile vile, Shirika kupitia kampuni tanzu ya Mzinga Holding Company Ltd limefanikiwa kujenga majengo ya Serikali ifuatavyo; Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Ikungi, Mbulu, Ushetu na Nzega; na Shule ya Sekondari Kahororo na Bukoba katika Manispaa mkoani Kagera. Aidha, kwa upande wa madeni kwa kipindi hiki cha mwaka mmoja wa Mhe. Rais, Wizara imefanikiwa kulipa madeni yenye thamani ya zaidi Shilingi billioni 175 kwa wazabuni waliotoa huduma mbalimbali kwa JWTZ.

Vile vile, Wizara pamoja na taasisi zilizo chini yake katika miradi mbalimbali inazotekeleza zimefanikiwa kutoa ajira zaidi ya 9,341 kwa vijana ambapo kati ya ajira hizo za kudumu ni 145 na 9,196 ni za muda.

Mafanikio ambayo Wizara imeyapata katika kutekeleza majukumu yake, yametokana na uwezeshaji unaofanywa na Serikali ya Awamu ya Sita ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Aidha, mafanikio hayo yamewezesha kuwepo kwa zana, vifaa na vitendea kazi.












# Serikali ya Awamu ya Sita yaupiga mwingi Sekta ya Uchukuzi

Na **Mwandishi Wetu**
**Uchukuzi**

Ni mwaka mmoja umepita toka Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mama Samia Suluhu Hassan iingie madarakani na kuendeleza gurudumu la maendeleo kwa kukendelea kutenga fedha kwa ajili ya kuimarisha sekta mbalimbali nchini.

Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi Sekta ya Uchukuzi ni miogoni sekta ambazo zimepewa fedha za kutekeleza miradi ya kimkakati amabyo ambayo kukamilika kwake kutaongeza tija na kukuza uchumi katika Taifa la Tanzania.

Miongoni mwa miradi mikubwa ambayo imeshuhudiwa kupigiwa chapuo kwa awamu ya sita ni pamoja na mradi wa ununuzi wa ndege tano kwa ajili ya kuendelea kutoa huduma ndani na nje ya nchi, Kusainiwa kwa mkataba wa Ujenzi wa Reli Sehemu ya Makutupora hadi Tabora kilomita 368, Mwanza hadi Isaka Kilomita 341, mkataba wa ununuzi wa vichwa vya treni ya Reli ya Kisasa ya SGR, Ukarabati wa Meli katika maziwa na miradi ya bandari.

Katika sekta ya usafiri nchi kavu hususani usafiri wa Reli Serikali ya awamua ya sita ilisaini mkataba wa Ujenzi wa Mwanza hadi Isaka kilomita 314 mkataba wake ulisainiwa 14 Juni 2021 kwa fedha takribani trilioni tatu na mradi huo unatarajiwa kukamilika mapema mei 2024.



Ni mwaka mmoja umepita toka Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mama Samia Suluhu Hassan iingie madarakani na kuendeleza gurudumu la maendeleo kwa kukendelea kutenga fedha kwa ajili ya kuimarisha sekta mbalimbali nchini.

Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi Sekta ya Uchukuzi ni miogoni sekta ambazo zimepewa fedha za kutekeleza miradi ya kimkakati amabyo ambayo kukamilika kwake kutaongeza tija na kukuza uchumi katika Taifa la Tanzania.

Miongoni mwa miradi mikubwa ambayo imeshuhudiwa kupigiwa chapuo kwa awamu ya sita ni pamoja na mradi wa ununuzi wa ndege tano kwa ajili ya kuendelea kutoa huduma ndani na nje ya nchi, Kusainiwa kwa mkataba wa Ujenzi wa Reli Sehemu ya Makutupora hadi Tabora kilomita 368, Mwanza hadi Isaka Kilomita 341, mkataba wa ununuzi wa vichwa vya treni ya Reli ya Kisasa ya SGR, Ukarabati wa Meli katika maziwa na miradi ya bandari.

Katika sekta ya usafiri nchi kavu hususani usafiri wa Reli Serikali ya awamua ya sita ilisaini mkataba wa Ujenzi wa Mwanza hadi Isaka kilomita 314 mkataba wake ulisainiwa 14 Juni 2021 kwa fedha takribani trilioni tatu na mradi huo unatarajiwa kukamilika mapema mei 2024.

Katika Mradi wa kipande cha Mwanza hadi Isaka mpaka sasa mradi umefikia zaidi ya asilimia 15 ambapo mkandarasi kampuni ya China Civil Engineeing Construction Corporations (CCECC) na Kampuni ya China Railway Construction Corporation Limited (CRCC) ambapo mpaka mwezi septemba 2021 Serikali yaw amu ya sita ilikuwa imeshamlipa mkandarasi zaidi ya shilingi bilioni 380.

Serikali ya awamu ya sita ya chini ya Uongozi wa Rais Samia Disemba 21 kupitia Shirika la Reli ya Tanzania (TRC) ilishuhudia utiaji saini wa mradi wa Reli ya SGR sehemu ya Makutupora hadi Tabora KM 368 ambao unakamlisha utekelezaji mradi mzima wa SGR kufikia sehemu nne kati ya tano ambazo zinatakiwa kutekelezwa.

Juhudi zote hizi ni katika kuhakikisha ahadi ya Rais Samia kuwa inatekelezwa kuwa miradi yote ya kimkakati itaendelezwa kwa kutengewa fedha ili kukamilika kwa wakati na hatimaye kuchochea uchumi wa Taifa.

Kwenye sekta ya Anga Rais Samia kwa mwaka wa fedha 21/22 ameendelea kuwekeza kwenye sekta hiyo kwa kuanza manunuzi ya 5 ikiwemo Boeing 767-300 F ndege moja kwa ajili ya mizigo, Boeing B737-9 Max ndege mbili na dash 8Q400 moja ambapo idadi hiyo itafikisha idadi ya ndege kumi na sita.

Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Ndege Tanzania Ladislaus Matindi anasema manufaa ya uwepo wa ndege hizo ni pamoja na kukidhi soko la ndani ya nchi kwa kutumia dash 8 Q400 na ndege kubwa kuhudumia abiria wa masafa marefu hususani kwa nchi ambazo ATCL inatoa huduma kama Goungzhou, India na badaae London.,

Kwa sasa tayari Serikali imeshanunua ndege 11 ambazo ni Boeing 787-8 Dreamliner mbili, Airbus A220-300 ndege nne, na Dash Q400 ndege nne na ndege hizo zinatoa huduma ndani ya nchi kwa vituo 15 na safari za kikanda vito zaidi ya 4 na nje ya nchini kwa vituo takribani mbili.


Serikali kwa upande wa usafirishaji kwenye Maziwa nchini kwa Ziwa Viktoria pamoja na ujenzi wa meli ya MV Mwanza unaoendelea ambapo kwa sasa umefikia zaidi ya asilimia 70 Serikali imetoa fedha kwa ajili ya ukarabati mkubwa wa meli ya MV Umoja amabpo mradi huo utagharimu zaidi ya shilingi bilioni 19.

Kwa upande wa Ziwa Tanganyika Serikali imewekeza fedha zadi ya shilingi bilioni nane kwa ajili ya ukarabati wa meli ya MT Sangara ambapo ukarabati huo umeshaanza na umefikia zaidi ya asilmia 20 na unatekelezwa chini ya Mkandarasi KTMI Co. Limited.

Serikali ya awamu ya sita imeendeleza kuwekeza fedha katika miradi ambapo ndani ya mwaka mmoja tumeshuhudia Serikali ikitekeleza Mradi Mkubwa wa Uboreshaji Bandari ya Dar es Salaam (Dar es Salaam Maritime Gateway Project- DMGP) unaohusisha kuongeza kina na kuimarisha Gati Na. 1 – 7 hadi kufikia kina cha mita 14.5 na kujenga Gati maalumu (RoRo berth) ya kuhudumia meli za magari.








Aidha, mradi huu utaongeza kina na upana wa Lango la kuingilia meli na eneo la kugeuzia meli (deepening and widening of entrance channel and turning basin) hadi kufikia kina cha mita 15.5, Kuboresha mtandao wa Reli (improvement of rail layout) ndani ya Bandari ya Dar es Salaam; na Kuongeza kina na kuimarisha Gati Na. 8 – 11 hadi kufikia kina cha mita 14.5. Mradi mzima unatekeleza kwa gharama ya Dola za kimarekani milioni 421 ambazo ni fedha za Mkopo milioni 345 kutoka benki ya dunia, milioni 12 fedha kutoka benki ya maendeleo ya Uingereza (DFID) na milioni 64 fedha kutoka Serikali ya Awamu ya Sita.

Uwekezaji wa zaidi ya trilioni 10 kwa maeneo matatu ya Sekta ya Uchukuzi yanaonesha dhamira ya Serikali katika kukuza uchumi wa nchini na kuwapatia wananchi fursa za kuchagua usafiri wanaooutaka kutoka sehemu moja kwenda sehemu nyingine.















# Mwaka mmoja wa Rais Samia Mapinduzi ya Utamaduni, Sanaa na Michezo Yadhihirika

Na **Shamimu Nyaki**
**Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo**

Mnano Machi 2022 Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Samia Suluhu Hassan inatimiza mwaka mmoja Madarakani ambapo mafanikio kadhaa yamepatikana.

Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo yenye dhamana ya kuwaburudisha na kuwapa furaha watanzania, kuwawezesha kuwa na ukunjufu wa moyo, uchangamfu na bashasha wakati wote imeona mafanikio katika sekta hii ndani ya mwaka huu mmoja. Moja ya mafanikio yaliyoonekana katika sekta hii ni hadhi iliyopewa lugha adhimu na aushi ya Kiswahili ambayo pia ni lugha ya Taifa.

Lugha hii imepiga hatua kubwa ndani na nje ya nchi ambapo katika Mkutano Mkuu wa 41 wa Shirika la Umoja wa Mataifa la Elimu, Sayansi na Utamaduni (UNESCO) uliofanyika mwezi Novemba 2021, Paris nchini Ufaransa ilipelekea kuitangaza rasmi tarehe 7 Julai ya kila mwaka kuwa siku ya Kiswahili duniani.

Azimio hilo limepitishwa na nchi zote Wanachama wa UNESCO bila kupingwa, kwa hakika mwaka mmoja huu wa Rais Samia tuna haja ya kutembea kifua mbele na kusema "Kazi Iendelee".

Aidha, Mkutano wa 35 wa Wakuu wa Nchi na Serikali umeridhia na kupitisha ombi la Tanzania la kutaka Kiswahili kuwa lugha ya kazi katika Umoja wa Afrika ambapo ombi hilo liliwasilisha na Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Philip Mpango.

Katika kushadadia mafaniko haya Serikali ya Awamu ya Sita imeliwezesha Baraza la Kiswahili la Taifa (BAKITA) kupata vifaa vya kisasa vya ukalimani ambavyo vitasaidia kuendesha mafunzo ya msasa kwa Wakalimani na Wamilisi wenye uwezo katika fani ya ukalimani. Tangu kuwasili vifaa hivyo tayari Baraza limetoa mafunzo ya msasa kwa Wakalimani 18 katika awamu mbili.

Naibu Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, Mhe. Pauline Gekul amesema Baraza hilo limeandaa Mkakati wa Taifa wa miaka 10 wa Kubidhaisha Kiswahili, (2021-2031) kama zana kukuza na kubidhaisha lugha hiyo. "Lengo la mkakati huo ni kukuza Kiswahili ili kitumike kama chachu na bidhaa katika kuleta maendeleo ya kiuchumi, kisiasa na kijamii ndani na nje ya nchi".

"Baraza linaendela kuhakikisha kuwa fursa zote zinazopatikana duniani kuhusuLugha ya Kiswahili zinaendela kunufaisha nchi ikiwemo huduma za Kiswahili kupitia kwa tafsiri na ithibati ambapo kwa mwaka 2021 lilitoa ithibati kwa miswada 142 iliyoandaliwa na Taasisi ya Elimu na watu binafsi, huduma ya ukalimani pamoja na kuendesha darasa la stadi za kufundisha Kiswahili kwa wageni", anaongeza Mhe. Gekul.

Kwa upande wa Sekta ya Sanaa, Serikali ya Awamu ya Sita pamoja na mambo mengine imesaidia kuanzishwa kwa Mfuko wa Utamaduni na Sanaa ambao umehuishwa ili pamoja na mambo mengine uweze kugharamia mafunzo kwa sekta za Sanaa na Utamaduni na kutoa mikopo ya masharti nafuu kwenye miradi bora ya sanaa na utamaduni. Mfuko huo umezinduliwa mwezi Novemba 2021 umetengewa kiasi cha shilingi bilioni 1.5 katika mwaka wa fedha 2021/2022 ili kusaidia wasanii.



Serikali ya Awamu ya Sita imeonesha nia ya dhati katika kusimamia Sekta ya Sanaa ambayo imeendela kuwaajiri vijana wengi nchini katika kazi mbalimbali za Sanaa ikiwemo Tamsha la Muziki la Serengeti na Tamasha la Sanaa na Utamaduni Bagamoyo ambayo yameendelea kuwaleta pamoja wasanii wakongwe na chipukizi nchini.

Mhe. Mchengerwa anasema sekta ya Sanaa inaajiri vijana wengi imepitia mabadiliko ambayo hatimaye wasanii wameanza kunufaika na kazi zao. Ili msanii anufaike na kazi zake ni lazima kwanza asajiliwe na kusajili kazi zao katika Taasisi ya Hakimiliki Tanzania (COSOTA).

Hatua hiyo imepelekea Serikali Awamu ya Sita kusimamia kidete haki za wasanii na sasa wameanza kupokea mirabaha kulingana na matumizi ya kazi zao kwenye vyombo vya habari na maeneo mengine yanayotumia kazi hizo.

"Ilikuwa ni kiu kubwa ya wasanii kuona wananufaika na kazi zao, kupitia COSOTA chini ya Serikali ya Awamu ya Sita kiasi cha shilingi milioni 312 zimetumika kulipa Mirabaha ya wasanii 1,123", anabainisha Mhe. Mchengerwa. Katika Sekta ya Michezo mafanikio mbalimbali yamepatikana ikiwemo ujenzi wa miundombinu ambao tayari Serikali ya Awamu ya Sita chini ya Mhe. Rais Samia Suluhu Hassan imetoa kiasi cha shilingi bilioni 9.5 kwa ajili ya kujenga viwanja vya wazi vya michezo na kiasi cha shilingi bilioni 1.3 kwa ajili ya kuzisaidia timu zote za taifa.

"Katika kuboresha miundombinu ya michezo sote tumemsikia Mhe. Rais na azma ya Serikali yake kuhakikisaha viwanja vya michezo nchini vinawekewa nyasi za bandia, ndiyo maana hatua ya kwanza Serikali imeanza na msamaha wa kodi kwenye nyasi bandia za viwanja vya michezo na kutaka asilimia tano ya mapato ya kwenye michezo ya kubahatisha kwenda katika mfuko wa kuendeleza michezo nchini" anasema Katibu Mkuu wa Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo, Dkt. Hassan Abbasi.

Aidha, michezo ya UMITASHUMTA na UMISETA, Wizara imeendelea kushirikiana na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia pamoja na Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) kuhakikisha mashindano hayo yanakuwa kitalu cha kuibua vipaji vya michezo na Sanaa mbalilmbali kwa wanafunzi nchini. Kwa kuanzia wanafunzi ambao wamefanya vizuri katika mchezo wa soka Serikali imechukua jukumu la kuendeleza vipaji vya wanafunzi hao kwa kuwapeleka katika Chuo cha Mandeleo ya Michezo Malya pamoja na vituo mbalimbali vya michezo nchini.

Fauka ya hayo, Chini ya Uongozi wa Serikali ya Awamu ya Sita limefanyika Tamasha la Michezo kwa Wanawake la Tanzanite kwa lengo la kuhamasisha wanawake kupenda michezo. Pia yamefanyika mashindano ya michezo ya walemavu pamoja na Taifa Cup imefanyika kwa mafanikio makubwa ambapo nchi imechangamka na inaendelea kuchangamka.

Mafanikio haya na ubunifu ndani ya Wizara ya Utamaduni Sanaa na Michezo ni mwanzo na ni kipenga ndiyo kimelia kuhakikisha Utamaduni wa Mtanzania kupitia kazi za Sanaa na michezo zinaendelea kulindwa, kuenziwa, kuhifadhiwa na kutunzwa kwa manufaa ya kizazi cha sasa na vizazi vijavyo.







# Mwaka Mmoja wa Rais Samia Waongeza Kasi ya Upangaji, Upimaji Ardhi Nchini

Na **Munir Shemweta**
**WIZARA YA ARDHI**

Serikali ya Awamu ya Sita chini ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Samia Suluhu Hassan inatimiza mwaka mmoja huku ikiwa imeelekeza nguvu kubwa katika kuinua uchumi wa Tanzania na maendeleo ya wananchi kwa ujumla.

Juhudi hizo zinazolenga kuleta ustawi kwa watanzania na nchi kwa ujumla zinagusa maeneo mbalimbali kama vile mawasiliano, miundombinu, uwekezaji na huduma za jamii. Sekta ya ardhi ni moja ya eneo muhimu katika maisha ya binadamu na halikuachwa katika mipango ya serikali ya awamu ya sita.

Katika kipindi cha mwaka mmoja wa Serikali ya Mhe. Samia juhudi kubwa zimefanyika na zinaendelea kufanyika kuhakikisha mifumo ya utunzaji kumbumbu za ardhi inaimarishwa huku ardhi ya Tanzania ikipangwa, kupimwa na kumilikishwa ili kuinua uchumi wa nchi na maendeleo ya mtu mmoja mmoja.

Katika kipindi cha mwaka mmoja tu tumeshuhudia Wizara ya Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi ikisimika na kujenga mfumo wa utunzaji kumbukumbu za ardhi katika jiji la Dodoma. Hivi sasa wamiliki wa ardhi kwenye mkoa huo wanapata hati za kielektroniki za kurasa moja ndani ya muda mfupi na tayari jumla ya hati 4,429 zimetolewa kufikia Februari 2022. Usimikaji mfumo huo unaifanya Wizara ya Ardhi kuwa na maeneo mawili yanayotoa hati za kielektroniki ambayo ni Mkoa wa Dar es Salaam na Dodoma.

Aidha, Wizara ya Ardhi imeanzisha Kituo cha Mawasiliano kwa wateja makao makuu ya Wizara eneo la Mji wa Serikali Mtumba, Dodoma ambapo kituo hicho kinapokea na kuzitafutia ufumbuzi wa haraka changamoto za sekta ya ardhi zilizoshindwa kutatuliwa kwenye ofisi zake za ardhi za mikoa na halmashauri nchini.

Katika juhudi za kuhakikisha ardhi inapangwa na kupimwa, Serikali ya Awamu ya sita kupitia Wizara ya Fedha na Mipango imeipatia Wizara ya Ardhi kiasi cha shilingi bilioni 50 kwa ajili ya kuzikopesha Halmashauri 55 kutekeleza Programu maalum ya Kupanga, Kupima na Kumilikisha Ardhi nchini. Utekelezaji programu hiyo pamoja na kusaidia kuondoa migogoro ya ardhi lakini itatengeneza chanzo kipya cha kodi kwa miaka inayokuja.

Aidha, Serikali ya Awamu ya Sita ya Mhe. Samia Suluhu Hassan kupitia Wizara ya Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi inazo programu mbalimbali zenye lengo la kuhakikisha ardhi inapangwa na kupimwa. Programu hizo ni pamoja na Mradi wa Benki ya Dunia na ule mradi wa Korea unaofadhiliwa na Benki ya Exim.

Miradi hii yote siyo tu inaongeza kasi ya upangaji, upimaji na umilikishaji ardhi nchini bali itatoa fursa ya ujenzi wa miundombinu, Ofisi, Masijala za ardhi pamoja na ujenzi wa kituo cha kutoa mafunzo kwa wataalamu wa upimaji kitakachojulikana kama Geo-Innovation Center.

Pia, miradi inawezesha upatikanaji vifaa vya upimaji kama vile ndege isiyo na rubani (Drones) itakayochukua picha za Satellite zitakazotumika kuandaa ramani za msingi za upimaji ambazo zitatumika kwenye matumizi ya upangaji, utawala wa ardhi na uwekaji miundombinu ya reli, umeme na mabwawa.

Kupitia mradi wa Korea, Serikali ya Tanzania na Korea zimeingia makubaliano kwenye mradi wa upimaji ardhi (Road Show) kwa mfumo wa kisasa wa kidigitali wenye lengo la kuongeza miundombinu kwa kuwa takwimu zilizopo zinaonesha miundombinu iliyopo ni ya zamani na ipo kwenye mfumo wa analogia. ''Kwa kutumia teknolojia hiyo ya kisasa tutaweza kupata taarifa zote kwa

mfumo wa kisasa wa kidigitali ambapo itakuwa rahisi zaidi kupata taarifa yoyote kwenye mfumo huo na Tanzania baada ya kupata uzoefu tutaendelea kupima kwa kutumia mfumo huo wa teknolojia ya kisasa ya kidigiatali'', alisema Hamdouny Mansoor, Mkurugenzi wa Upimaji na Ramani Wizara ya Ardhi.

Kuhusu Mradi wa Benki ya Dunia, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa kushirikiana na Benki ya Dunia inaandaa mradi wa kuboresha milki ya ardhi nchini. Mradi huu unalenga kuongeza usalama wa haki za ardhi na ufanisi kwenye utawala wa ardhi kwenye maeneo ya ya Mijini na Vijijini na hivyo kukuza uwekezaji na pato la Taifa.

Sambamba na miradi hiyo, pia Serikali ya Awamu ya Sita katika kipindi cha mwaka mmoja imeendelea na zoezi la urasimishaji makazi holela kwa kasi ambapo takwimu zinaonesha kuwa hadi kufikia Desemba 2021 jumla ya viwanja 2,063,113 vimepangwa, 1,215,398 vimefanyiwa upimaji wa awali, 911,556 vimepimwa na kuidhinishwa huku Ankara 403, 957 zikiwa zimetolewa na hati 131, 018 kuandaliwa.

Juhudi hizi zinaifanya Serikali ya Awamu ya Sita chini ya Mhe. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupiga hatua ndani ya muda mfupi wa mwaka mmoja katika masuala mazima ya Sekta ya ardhi hususan upangaji na upimaji hasa ikizingatiwa tangu Tanzania kupata uhuru ni takriban asilimia 30 tu ardhi yote ndiyo imepangwa na kupimwa.

Akielezea kiasi cha shilingi bilioni 50 zilizotolewa kwa ajili ya kuzikopesha halmashauri kupitia programu ya kupanga na kupima ardhi nchini, Waziri wa Fedha na Mipango Mhe. Dkt Mwigulu Nchemba alisema, mpango huo wa kuzikopesha halmashauri utaipeleka Wizara yake katika hatua kubwa zaidi na kuimarisha shughuli za uzalishaji kwa kutumia ardhi.

"Mpango huu utatupeleka katika hatua kubwa zaidi, tutaimarisha shughuli za uzalishaji kwa kutumia ardhi pamoja na kutatua migogoro ya ardhi ambayo imekuwa kero kwa muda mrefu", alisema Dkt. Nchemba.

Fedha hizo zimetolewa kwa Halmashauri zilizokidhi vigezo ambapo katika awamu ya kwanza halmashauri 55 zilizokidhi vigezo kati ya 78 zilipatiwa fedha ambazo ni pamoja na Dodoma Jiji shilingi bilioni tatu, Ilemela shilingi bilioni 3.5, Chalinze shilingi bilioni mbili na Meru shilingi bilioni 6.5.

Aliyekuwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais – TAMISEMI, Mhe. Ummy Mwalimu alizielezea fedha zilizotolewa kuwa, zitatumika kutatua














kero na dhuluma kwa wananchi sambamba na kuwawezesha kiuchumi kutokana na maeneo yaliyopimwa na kupangwa ni rahisi kukopesha kuliko wanaomiliki maeneo yasiyo rasmi.

''Programu hiyo italeta matokeo chanya kwa kupunguza uendelezaji na ukuaji holela wa miji, kupendezesha mitaa na kuwa safi na salama pamoja na kuongeza maeneo ya ardhi kwa ajili ya miundombinu ya kijamii na kiuchumi'' alisema Mhe. Ummy Mwalimu

Akizungumza hivi karibuni alipotoka kuapishwa kushika wadhifa wa Waziri wa Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Mhe. Dkt Angeline Mabula alisema, moja ya mikakati yake ni kuhakikisha sehemu kubwa ya ardhi ya Tanzania inapangwa, inapimwa na kumilikishwa kwa wananchi.

Alisema, hatua hiyo ndiyo njia sahihi ya kuondoa migogoro ya ardhi sambamba na kuwawezesha wananchi kiuchumi kwa kuwa wanaweza kuitumia ardhi waliyomilikishwa katika shughuli za kiuchumi kwa kuwa wanaweza kuchukulia mikopo benki.

''Kazi yangu kubwa ni kuhakikisha natekeleza vipaumbele vya Mhe. Rais Samia Suluhu Hassan ambapo msisitizo wake mkubwa ni masuala mazima ya uwekezaji, matumizi ya mifumo katika utawala wa ardhi pamoja na kuhakikisha sehemu kubwa ya ardhi ya Tanzania inapangwa, kupimwa na kumilikishwa''. Alisema Mhe. Dkt Mabula

Aliongeza kuwa, utekelezaji wa maelekezo ya Rais na programu mbalimbali za wizara siyo tu unaleta usalama wa milki za ardhi kwa wananchi na kuondoa migogoro ya ardhi bali unaiwezesha serikali ya awamu ya sita kuongeza mapato yatokanayo na kodi ya pango la ardhi na hivyo kuleta ustawi wa maisha ya watanzania na Taifa kwa ujumla.

Kiujumla juhudi zilizofanyika na ule uwezeshwaji unaofanywa na serikali ya awamu ya sita chini ya Mhe. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ndani ya mwaka mmoja unatoa unatoa mwanga kuwa serikali yake siyo tu imedhamiria kuinua uchumi na ustawi wa wananchi pekee bali inataka kuhakikisha ardhi inapangwa, inapimwa na inamilikishwa huku migogoro ya ardhi ikiwemo ile ya wakulima na wafugaji inakoma.













# Awamu ya Sita: Mafanikio makubwa ujenzi wa uchumi shindani

Na **Mwandishi Wetu**
**Wizara ya Viwanda**

Ni dhahiri kuwa Sekta za Uwekezaji, Viwanda na Biashara zina mchango mkubwa katika ujenzi wa uchumi shindani na Viwanda kwa maendeleo ya watu. Uchumi shindani na viwanda unajumuisha kuchochea uchumi shindani na shirikishi na kuimarisha ukuaji wa uzalishaji wa ndani na utoaji huduma, kukuza uwekezaji na biashara, kuchochea maendeleo ya watu na kuendeleza rasilimali watu.

Kutokana na umuhimu huo, Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara ina jukumu la kuandaa na kusimamia Sera, Mikakati na Sheria mbalimbali za kisekta zenye malengo ya kuongeza ufanisi katika Sekta ya Viwanda na Biashara ikiwa ni pamoja na kuboresha mazingira ya kufanya biashara na kuvutia uwekezaji nchini yatakayochochea kasi ya maendeleo jumuishi na endelevu ya kiuchumi na maendeleo ya watu kwa kutumia malighafi za ndani kama vile: mafuta, gesi, makaa ya mawe, saruji, chuma, ngozi na malighafi za kilimo.

Katika kipindi cha mwaka mmoja wa Serikali ya awamu ya sita, Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara kwa kushirikiana na Taasisi zake imepata mafanikio makubwa katika ujenzi wa uchumi shindani na viwanda kwa maendeleo ya watu kwa kuzingatia miongozo mbali mbali inayotolewa ikiwa ni pamoja na Dira ya Taifa ya 2025, Agenda ya Dunia ya Malengo ya Maendeleo Endelevu 2030; Agenda ya Maendeleo ya Bara la Afrika Tuitakayo, 2063, Ilani za Uchaguzi za CCM katika vipindi mbali mbali vya uchaguzi ndani ya mfumo wa chama kimoja na vyama vingi pamoja, MKUKUTA I & II (2000 – 2010) na Mipango ya Taifa ya Maendeleo ya Miaka Mitano katika vipindi vitatu (2011 – 2026).

### Mafanikio ya Uwekezaji

Tangu kuanza kwa mageuzi ya kiuchumi katika miaka ya 1980, Tanzania imekuwa inahakikisha uwepo wa mazingira bora na miundombinu wezeshi ya kusaidia sekta binafsi kuwekeza katika uzalishaji na biashara nchini.

Baadhi ya jitihada hizo za kuvutia uwekezaji wa ndani na ule wa nje ni pamoja na kuundwa kwa Sera ya Taifa ya Uwekezaji ya Mwaka 1996 na Sheria ya Uwekezaji ya Mwaka 1997. Sheria hiyo ndiyo iliyoanzisha Kituo cha Uwekezaji cha Tanzania (TIC) ambayo ndiyo Wakala maalum wa Serikali wa kutangaza, kuvutia, kusaidia na kuratibu shughuli za wawekezaji wote nchini.

Kutokana na jitihada hizo, takwimu za uwekezaji wa ndani (Domestic Direct Investment - DDI) na ule wa kutoka nje (Foreign Direct Investment - FDI) umekuwa ukiongezeka mwaka hadi mwaka. Taarifa hii imeonesha mafanikio katika vigezo vitatu vinavyotumika kupima kiwango cha uwekezaji kwa nchi ambavyo ni Uwiano wa Uwekezaji na Pato la Taifa (Gross Capital Formation to GDP ratio), Kiwango cha Uwekezaji Kutoka Nje (Foreign Direct Investment inflows), kiwango cha Ukuzaji Rasilimali kwa kila mwaka (Fixed Capital Formation) na usajili wa miradi kupitia Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC) na Mamlaka ya Maeneo Maalum ya Uzalishaji kwa Mauzo Nje (EPZA).

### Uwekezaji Kutoka Nje ya Nchi

Uwekezaji wa mitaji kutoka nje umekuwa ukiongezeka kutoka Dola za Marekani milioni 0.99 mwaka 2016 hadi Dola za Marekani milioni 1.013 mwaka 2020 kwa mwaka. Viwango hivyo vimeiweka Tanzania katika nafasi ya kuendelea kuongoza kwa

kuvutia mitaji ya uwekezaji kutoka nje katika nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC).

**Mafanikio ya Uwekezaji Kupitia Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC)**

TIC imetekeleza majukumu iliyopewa ya uhamasishaji, uwekezaji na utoaji wa huduma ikiwepo utoaji wa huduma za vibali, leseni na usajili wa masuala ya uwekezaji mahali pamoja (One Stop Shop). Majukumu ya msingi ya Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC) ni pamoja na kuanzisha na kusaidia kuimarisha mazingira ya uwekezaji nchini kwa wawekezaji wa ndani na nje ya nchi; Kukusanya, kuchambua na kusambaza taarifa za fursa za uwekezaji zilizopo nchini; Kubainisha maeneo ya uwekezaji ikiwepo ardhi na miundombinu wezeshi kwa madhumuni ya uwekezaji kwa kushirikiana na taasisi na Wakala wa Serikali; na Kusaidia wawekezaji kuweza kupata vibali, leseni na idhini mbalimbali ambazo zinasaidia kufanikisha uwekezaji. Baadhi ya Miradi mikubwa iliyosajiliwa na TIC katika kipindi cha Serikali ya awamu ya sita ni pamoja na: -

**(i)** S. J. Sugar, kwa ajili ya kilimo cha miwa na ujenzi wa viwanda vya sukari mkoani Ruvuma;
**(ii)** Nile Perch Limited na Victoria Perch Limited kwa ajili ya usindikaji wa Samaki;
**(iii)** Nyanza Bottling Limited na SBC Limited kwa ajili ya viwanda vya vinywaji;
**(iv)** Sayona Steel Limited kwa ajili ya kiwanda cha kuchakata chuma na nondo, mkoani Mwanza;
**(v)** Busolwa Mining na Geita Gold Mine kwa ajili ya kuchakata madini;
**(vi)** Jambo Food Products kwa ajili ya utengenezaji wa juisi na maji mkoani Geita;
**(vii)** Kagera Sugar Limited kwa ajili ya kilimo na utengenezaji wa sukari;
**(viii)** Prime Catch Limited kwa ajili ya usindikaji wa samaki katika mkoa wa Mara; na
**(ix)** KEDS Tanzania Limited na Goodwill (T) Ltd Mkoa wa Pwani kwa ajili ya kiwanda cha kutengeneza vigae;

**Mafanikio ya Uwekezaji Kupitia Mamlaka ya Maeneo ya Uzalishaji kwa Mauzo Nje (EPZA)**

Kutokana na uanzishaji na uendelezaji wa viwanda katika maeneo ya EPZ/SEZ. Serikali imefanikiwa kupata Thamani ya Mitaji ya uwekezaji iliyosajiliwa chini ya EPZA ni USD 2.539 Bilioni, Ajira mpya za moja kwa moja 63,159; na Thamani ya mauzo ya bidhaa za Nje ya nchi USD 2.443 Bilioni. Serikali imeandaa Mwongozo wa Uwekezaji katika Mitaa ya Viwanda (Industrial Parks) nchini ambao utatoa taswira, mwongozo na Taasisi zinazohusika ili kurahisisha hatua za kuwekeza katika Mitaa ya Viwanda.

Serikali imefanikiwa kutenga maeneo matano kwa ajili ya kuanza ujenzi wa mitaa ya Viwanda katika mikoa ya Dar es salaam, Tanga, Arusha, Kilimanjaro na Mwanza. Aidha, Serikali ya Awamu ya Sita imetoa ridhaa ya kuendelea na majadiliano na wawekezaji ili kuendeleza eneo Maalum la Uwekezaji lililopo Bagamoyo ili kuvutia

**Miradi iliyosajiliwa na Mamlaka ya EPZ 2015 - Juni 2021**

| Mwaka | 2015/16 | 2016/17 | 2017/18 | 2018/19 | 2019/20 | 2020/21 |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Miradi Mipya Iliyosajiliwa | 10 | 20 | 09 | 11 | 5 | 17 |
| Mtaji (US$ Milioni) | 500 | 314.30 | 336.0 | 180.06 | 59.86 | 86.86 |



wawekezaji na kuendeleza eneo la Kurasini Logistics Centre lililopo Dar es Salaam ambapo kiasi cha shillingi bilioni 30 kimetolewa kwa ajili ya mradi huo. Katika kutatua changamoto za wawekezaji, Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara inaendelea na maandalizi ya Sera mpya ya Uwekezaji ambayo itaainisha vyema majukumu ya Wizara inayohusika na uwekezaji na mahusiano yake na wizara za kisekta.

Aidha, Wizara imeandaa rasimu ya Mwongozo wa Uwekezaji kwa lengo la kuimarisha uratibu wa kuwahudumia wakezaji nchini. Vilevile, Wizara imepanga kujumuisha mfumo wa kupokea na kuratibu utatuzi wa changamoto na malalamiko ya wawekezaji kupitia Mfumo wa Kieletroniki unaoandaliwa wa kuhudumia wawekezaji kupitia Dirisha Moja la Tanzania Investment Single Window System. Mfumo huo utaunganisha mifumo ya Taasisi zote zinazohudumia wawekezaji ili kuwa na Dirisha Moja la Kutoa Huduma za Vibali na Leseni kwa Wawekezaji Kimtandao.

Wataalam kutoka Taasisi mbalimbali za Serikali chini ya usimamizi wa Mamlaka ya Serikali Mtandao (eGA) wanaendelea na zoezi la kuunda mfumo huo ambao utawezesha Taasisi zote zinazotoa huduma kwa wawekezaji kuunganishwa ili mifumo yake iweze kuwasiliana.

Hadi sasa, kazi hiyo imekamilika kwa asilimia 50, na awamu ya kwanza ya kuunganisha mifumo ya kitaasisi inatarajiwa kukamilika mwisho wa mwezi Februari, 2022 ambapo Taasisi sita za NIDA, UHAMIAJI, Idara ya Kazi, BRELA, TIC na TRA zitakuwa zimeunganishwa. Vilevile, Wizara imeendelea na maandalizi ya Sera mpya ya Taifa ya Uwekezaji na Sheria mpya ya Uwekezaji ili iendane na mazingira ya sasa ikiwa ni pamoja na kujumuisha vipaumbele na Mipango ya Maendeleo ya Taifa na mabadiliko ya kikanda na kidunia. Kukamilika kwa Sera hiyo kutachochea katika kuvutia zaidi uwekezaji wa ndani na nje ya nchi.

Aidha, Wizara inaratibu maandalizi ya ujenzi wa Kongani ya Viwanda vya Mafuta ya Kula yanayotokana na mbegu za alizeti mkoani Singida. Kongani hiyo itakuwa na maeneo ya Viwanda (Industrial Parks), shughuli za kilimo (malighafi), ubunifu na maarifa. Ardhi ya uwekezaji yenye ukubwa wa ekari 45,000 imetengwa katika Wilaya ya Manyoni kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huo. Kongani nyingine ni ya sukari (Sugar Park) inayopang-





wa kutekelezwa katika Mkoa wa Morogoro katika Wilaya ya Kilosa eneo la Dakawa. Mradi utahusisha wawekezaji wadogo wa mashine ndogo zenye uwezo 200 – 500 TCD. Wizara pia inaratibu uanzishaji wa kongani ya viwanda eneo la Kwala katika Mkoa wa Pwani ambayo itaendelezwa na kampuni ya Sino Tan Kibaha Industrial Park Limited yenye ukubwa wa ekari 2,500 na unatarajia kuwekeza kiasi cha Dola za Marekani Bilioni 3, kuzalisha ajira za moja kwa moja 100,000 na zisizo za moja kwa moja 300,000.

Kutokana na jihudi mbalimba za kuvutia wawekezaji zinazofanywa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Samia Suluhu Hassan, Makampuni mbalimbali yanaendelea na taratibu za uwekezaji nchini ikiwemo Kampuni ya Elsewedy kutoka Misri inaendelea na taratibu za upatikanaji wa ardhi kwa ajili ya ujenzi wa kongani ya viwanda katika eneo la Kigamboni yenye ukubwa wa mita za mraba 2,000,000 ambapo uwekezaji wake unakadiriwa kuwa na thamani ya Dola za Marekani milioni 200. Takribani, viwanda 100 na ajira za moja kwa moja 10,000 zinatarajiwa kuzalishwa katika Mradi huo.

Serikali imefanya Marekebisho ya Sheria ya Kuratibu Ajira za Wageni ambapo kwa sasa sheria inaruhusu mwekezaji kuingiza wataalam 10 kutoka watano (5) ilivyokuwa kabla ya mwezi Oktoba, 2021 na kuondoa sharti la kupata idhibati ya vyeti vya elimu kutoka TCU na NACTE kwa wanaoomba vibali vya kazi.

Halikadhalika, Serikali imeunganisha mifumo ya kielektroniki ya utoaji wa vibali vya kazi kwa wageni (Online Work Permit Application and Issuance System-OWAIS) na kufungamanisha (integration) na Mfumo wa kielektroniki wa maombi ya vibali vya ukaazi (Online System for application of Residence Permit - e-Permit).

Serikali imefanikiwa kuchochea uanzishwaji wa shughuli za kiuchumi kwa kutoa mafunzo na kutumia mikopo inayotolewa na Shirika la kuhudumia viwanda vidogo (SIDO) chini ya Program ya SANVN inayojumuisha taasisi za SIDO, VETA, AZANIA BANK, NSSF na NEEC na Mfuko wa Wafanyabiashara na Wananchi (NEDF) ambao hadi 2020 una Bilioni 8.65 zinazotolewa kwa wajasiliamali.

Vilevile, Serikali imekamilisha ujenzi wa majengo viwanda 11 (industrial sheds) na kukarabati jengo kiwanda 1 (industrial shed) kwenye maeneo mbalimbali nchini kwa ajili ya mafunzo na uzalishaji wa bidhaa mbalimbali. Majengo hayo yamejengwa katika mikoa ya Kagera (1), Geita (4), Dodoma (3), Manyara (3) na Mtwara (1). Kwa upande wa Sekta ya Biashara, Serikali iliandaa Mpango wa Kuboresha Mfumo wa Udhibiti wa Mazingira ya Biashara nchini (Blue Print for Regulatory Reforms to Improve the Business Environment for Tanzania). Mpango huo umewezesha maboresho ya tozo 233 ambapo kati ya tozo hizo, tozo 163 zimefutwa na tozo kero 10 zimepunguzwa kiwango. Kati ya tozo zilizofutwa, 114 ni za Sekta ya Kilimo na Mifugo, 5 za OSHA, 44 za TBS, GCLA, Utalii, Maji, Uvuvi na iliyokuwa Mamlaka ya Chakula na Dawa-TFDA. Mpango huo umewezesha kuhamisha jukumu la usimamizi wa masuala ya chakula kutoka iliyokuwa TFDA kwenda TBS, ili kuondoa muingiliano wa majukumu. Maboresho hayo yamesaidia kuondoa urasimu na kupunguza gharama za kufanya biashara. Aidha, Tozo 60 zilizokuwa zinatozwa na Wizara, Idara na Taasisi zinazojitegemea zimefutwa.

Serikali pia imefanikiwa kuboresha Vituo vya Pamoja vya Mipakani (One Stop Border Posts - OSBP) kwa kuweka mifumo na kukamilisha ujenzi ili kurahisisha shughuli za Taasisi za usimamizi mipakani kutekeleza majukumu yao kwa pamoja kwa ufanisi, gharama nafuu na muda mfupi kwa kuwarahisishia wafanyabiashara, magari na bidhaa kukaguliwa mara moja wakati wa kuingia au kutoka katika mpaka wa nchi. Vituo hivyo ni pamoja na Holili/Taveta, Namanga/Namanga, Sirari/Isebania Horohoro/Lungalunga (Tanzania na Kenya), Kabanga/Kobero (Tanzania na Burundi), Rusumo/Rusumo (Tanzania na Rwanda), Mtukula/Mtukula (Tanzania na Uganda),Tunduma/Nakonde (Tanzania na Zambia) na Kasumulu/Songwe (Tanzania/Malawi).

Serikali imefanikiwa kuboresha mazingira ya biashara kwa kurahisisha shughuli za usajili wa majina ya biashara, usajili wa makampuni na alama za biashara na Huduma, na kutoa hataza, leseni za viwanda na leseni za biashara kwa njia ya mtandao (online kupitia www.brela.go.tz). Kampuni inayoshughulikia mfumo wa utambuzi wa bidhaa (Bar Codes) - GS 1 (TZ) National Limited imeanzishwa nchini.

Vilevile, kuanzishwa kwa mfumo wa stakabadhi za mazao ghalani mwaka 2007 kumetengeneza mazingira ya ushindani katika ununuzi wa mazao hali iliyosababisha wakulima kuwa na uhakika wa bei za mazao wanayozalisha. Halmashauri katika maeneo husika pia zimenufaika kupitia kodi kutokana na ongezeko la bei. Huku Wakala wa Vipimo imeendelea kumlinda mlaji kwa kuhakikisha anapata bidhaa kupitia matumizi ya vipimo sahihi katika ununuzi na uuzaji. Wakala umesogeza huduma karibu na wananchi kwa kufungua ofisi katika mikoa yote ya Tanzania bara na kwa Mkoa wa Dar es Salaam kila Wilaya. Kwa upande wa masoko ya ndani na nje, Serikali imefanikiwa kuwaunganisha wazalishaji wa ndani na fursa za masoko ya ndani na nje kupitia Maonyesho ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es Salaam (DITF) ambayo yanayofanyika mwezi Julai kila mwaka, Maonyesho ya Viwanda yanayofanyika mwezi Desemba kila mwaka, Maonyesho mbalimbali ya Biashara ya Kimataifa ya nje ya nchi yanayolenga kukuza biashara, misafara ya kibiashara inayoingia nchini na inayotoka nje na Maonyesho makubwa ya EXPO yanayolenga kukuza Biashara na kuvutia wawekezaji kama vile Expo Aichi, Expo Shanghai, Expo Zaragoza na mwaka huu 2021 Tanzania inashiriki katika maonyesho ya Dubai EXPO 2020.

Aidha, Serikali imefanikiwa kuhamasisha na kulinda ushindani wa shughuli za kibiashara na kumlinda mlaji wa bidhaa na huduma dhidi ya mwenendo usio wa haki, na upotoshaji, ukiukwaji wa mikataba, muonekano potofu wa bidhaa katika soko kupitia Tume ya Ushindani na Baraza la Ushindani. Aidha, Serikali imefanikiwa kujenga masoko yanayokidhi viwango vya Kimataifa yanayowawezesha wakulima kuuza mazao yao yakiwa katika ubora.

Sekta ya Biashara imewezesha uuzaji nje wa bidhaa zenye thamani ya Dola za Marekani Bilioni 6.06 kwa mwaka 2020. Ongezeko hilo limetokana na kuimarika kwa uzalishaji nchini na kutumika kwa fursa mbalimbali za masoko zinazotokana na uhusiano wa kibiashara baina ya Tanzania na nchi moja moja (bilateral), kikanda (regional) na kimataifa (multilateral) kwa madhumuni ya kutafuta fursa za masoko yenye masharti nafuu na kuboresha mazingira ya kufanya Biashara.

Mafanikio hayo yamepatikana kutokana na fursa mbalimbali za masoko ya upendeleo maalum (preferential market access) baina ya Tanzania na nchi za China, India, Japan, Kanada na Korea ya Kusini, Itifaki ya Umoja wa Forodha baina ya Tanzania na nchi zingine wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki; Jumuiya ya Uchumi ya Nchi za Afrika ya Kati (CEMAC), Jumuiya ya Uchumi ya Nchi za Afrika Magharibi (ECOWAS), Jumuiya ya Ulaya na Uswisi chini ya mpango wa Uza Kila Kitu Isipokuwa Silaha (Everything But Arms - EBA).

Mkataba wa Eneo Huru la Biashara barani Afrika (AfCFTA), Karibiani na Pasifiki (ACP) na Kutetea maslahi ya kibiashara ya Tanzania na ya nchi za kundi la LDCs katika majadilianao ya Biashara ya Kimataifa (multilateral trade negotiations).



# Rais Samia Afuata Nyayo za Nyerere, Karume Kuulinda Muungano

Na **Immaculate Makilika**
**Idara ya Habari - MAELEZO**

Tanzania ni lulu ya pekee kabisa katika historia ya Afrika huru. Nchi nyingine zote ni za kurithi kutoka katika ukoloni. Tuliokwisha kuunganisha nchi mbili zikawa nchi moja, sasa tukaunganisha vyama viwili vikawa chama kimoja. Hii haikuwa hatua ndogo hata kidogo katika kujenga nchi yetu. Kuna nchi gani nyingine zilizofanya hivyo? Vyama tunavyoviona katika bara letu siku hizi vinashindwa hata kuunganisha mbinu tu, ili viweze kushinda wapinzani wao katika uchaguzi.

Tumejenga nchi ambayo ilikuwa inaheshimiwa duniani kote, ndani na nje ya Afrika. Haya ni maneno hadhimu na adimu yaliyoandikwa na Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere katika kitabu chake cha Uongozi wetu na Hatima ya Tanzania.

Ni dhahiri kuwa Tanzania imebarikiwa kuanzia rasilimali hadi viongozi wake ambao wote kwa nyakati tofauti wameendelea kuwa viongozi mahiri wenye maono, uthubuti na nia ya dhati ya kuongoza na kuwalinda wananchi wao.

Utakubaliana nami kuwa Serikali ya Awamu ya Kwanza iliasisi Muungano wa Tanganyika na Zanzibar mwaka 1964 na hata baada ya miaka 60 bado Serikali ya Awamu ya Sita imeendelea kutekeleza maono na falsafa za wakati huo.

Hii inadhihirisha kuwa Tanzania ni lulu ya pekee kabisa katika historia ya Afrika huru na hata na duniani kote.

Kama ambavyo Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere na Rais wa Awamu ya Kwanza na Mwenyekiti wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, Abeid Aman Karume walivyoulinda Muungano hata sasa Rais wa Awamu ya Sita ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Samia Suluhu Hassan amekuwa akisisitiza kuongeza ushirikiano lakini na kubwa zaidi kutatua kero za Muungano zilizokuwa zikipigiwa kelele kwa miaka kadhaa.

Wakati huu ambapo Rais Samia anatimiza mwaka mmoja tangu aingie madarakani Machi 19, 2021, ameweza kufuta kero 11 kati ya 18 za Muungano pamoja na kuimarisha uhusiano uliopo kati ya Tanzania Bara na Visiwani.

Hivi karibuni, Mkurugenzi wa Idara ya Habari – MAELEZO na Msemaji Mkuu wa Serikali, Gerson Msigwa wakati akitoa taarifa yake kuhusu utekelezaji wa sera, miradi na utekelezaji wa shughuli mbalimbali za Serikali alisema kuwa licha ya kuwepo changamoto mbalimbali za Muungano Serikali imeendelea kutafuta maarifa na majawabu ya kukabiliana nazo.

Ambapo kumekuwepo na utaratibu wa kuwa na vikao vya pamoja vya kuzungumzia masuala ya Muungano ukiwemo utatuzi wa hoja za Muungano.

"Tulianza jukumu hili tangu mwaka 2006 tukiwa na hoja 25, tumefanya kazi kubwa ya kuzitafutia ufumbuzi, tukazipunguza hadi mwaka 2019 zikabaki hoja 18 na tarehe 24 Agosti mwaka jana 2021 tukaandika historia nyingine ya kuzifuta hoja 11 kati ya 18 katika vitabu vyetu kwa kuwa tayari zilikuwa zimeshapatiwa ufumbuzi", anasema Msigwa.

Alifafanua hoja zilizopatiwa ufumbuzi na kuondolewa kwenye orodha ya hoja na Muungano kuwa ni uingizaji wa maziwa Tanzania Bara kutoka Zanzibar ambapo waingizaji wa maziwa kutoka Zanzibar kwenda Tanzania Bara walikuwa wanatozwa shilingi 2,000/- kwa lita, lakini sasa tozo hii imepunguzwa hadi shilingi 250/- kwa lita.

Na waingizaji wa maziwa haya wamehimizwa kuzalisha maziwa kutoka Zanzibar badala ya kuingiza maziwa ya unga kutoka nje ya nchi na kisha kuyatengeneza kuwa ya maji na kuyaingiza Bara.

Hoja nyingine ni usimamizi wa ukokotoaji na ukusanyaji wa kodi kwenye Huduma za Simu unaofanywa na Mamlaka ya Mapato Zanzibar (ZRB).

Hoja zingine zilizopatiwa ufumbuzi "Mkataba wa mkopo wa fedha za ujenzi wa Barabara ya Chake chake hadi Wete – Pemba, hoja hii ilitokana na kuwepo kwa sharti la lililotaka mkopo upatikane kupitia Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, sharti hili liliondolewa", alisisitiza Msigwa.



Hoja nyingine ni pamoja na Mkataba wa mkopo wa fedha za Mradi wa Ukarabati wa Hospitali ya Mnazi Mmoja, Mkataba wa mkopo wa fedha za ujenzi wa Bandari ya Mpigaduri, Uvuvi kwenye Ukanda wa Uchumi wa Bahari Kuu.

Aidha, Ajira kwa Watumishi wa Zanzibar katika Taasisi za Muungano. Hoja hii imetatuliwa na Wazanzibar wanayo nafasi ya kuajiriwa Bara kupitia dirisha la ajira la sekretarieti ya ajira. Mgawanyo wa mapato yatokanayo na Misaada kutoka Nje ya Nchi.

Hivi sasa Zanzibar inapata mgao na inaweza kuomba msaada kutoka nje ya nchi hata bila kibali cha Waziri wa Fedha na Mipango kama ilivyokuwa awali pamoja na Mapato yanayokusanywa na Uhamiaji kwa upande wa Zanzibar. Hoja hii imeondolewa kwa sababu tayari maamuzi yamefanyika kwamba kila upande utakapokusanya mapato yatokanayo na visa yatabaki katika upande husika.

Aidha, mara kadhaa viongozi wa Serikali zote mbili wamekuwa wakisisitiza kuwa Muungano ni imara na hivyo wanaendelea kushirikiana katika masuala mbalimbali hususani masuala ya maendeleo.

Baadhi ya masuala ya maendeleo wanayoshirikiana ni kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Jamii nchini (TASAF) Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini Awamu ya Tatu Mzunguko wa Pili ambao ulizinduliwa mwezi Februari, 2020 ambapo jumla ya shilingi bilioni 112.9 zinatumika Zanzibar na kazi inaendelea.

Fedha za Kuchochea Maendeleo ya Jimbo kwa Majimbo yote ya Tanzania Bara na Zanzibar na fedha hizo hutumika kutekeleza miradi ya maendeleo kwenye Majimbo. Kwa majimbo ya Zanzibar kila mwaka hupokea shilingi bilioni 1.4 ambazo hutumika kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo katika Majimbo 50 yaliyopo Zanzibar.

Pamoja na mradi wa usogezaji wa huduma za mawasiliano katika maeneo ambayo yana mawasiliano hafifu au hayana mawasiliano kabisa. Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (Universal Communications Service Access Fund – UCSAF) na Kampuni ya Mawasiliano Zanzibar (Zantel) wameingia makubaliano mwezi Januari, 2022 ya kujenga minara ya simu 42 katika shehia 38 kwa lengo la kuboresha huduma ya mawasiliano Zanzibar.

Mradi huu ukikamilika Zanzibar mtu atapiga simu akiwa mahali popote labda kutokee kikwazo maalumu.


Matokeo ya ushirikiano wa Serikali hizi mbili yameleta mafanikio katika maeneo mbalimbali ambapo kuanzia mwezi Juni 2021 hadi sasa Mamlaka ya Uvuvi wa Bahari Kuu inayosimamia (DSFA) imekusanya Shilingi bilioni 2.4 na kutoa gawio kwa serikali (SMT na SMZ) ya asilimia 50 ya mapato hayo ikilinganishwa na kushindwa kukusanya kabisa mwaka 2019 na 2020.

Mafanikio haya yametokana na kutungwa kwa sheria ya Kusimamia na Kuendeleza Uvuvi wa Bahari Kuu, Sura ya 388 ya mwaka 2020 ambayo imeridhiwa na Baraza la Wawakilishi.

Kanuni zake zimeanza kutumika mwaka 2021. 1Sheria na Kanuni hizi zimechohea uwekezaji katika uvuvi wa Bahari Kuu.

Aidha, kufadhili mradi wa Kutambua Maeneo yenye Samaki wengi Baharini (Potential Fishing Zone - PFZ), jumla ya wavuvi wadogo 3,360 wamefaidika na mradi huu.

Rais Samia ameendelea kudhihirisha kuwa tunu ya Watanzania ni Muungano na hawana budi kuulinda kwani licha ya kuwa ni Muungano wa kipekee duniani bado una sifa nyingine za kiuchumi na kihistoria na hivyo wakati wengine wakifikiria kupigana na kutengana Watanzania wafikirie kuungana na kuiimarisha zaidi.






# Mwaka Mmoja wa Rais Samia Madarakani: Wawekezaji Madini Wampongeza

## Wafurahishwa na mazingira mazuri

## ● Wakiri, haijawahi kutokea

Na **Georgina Misama**
**Idara ya Habari - MAELEZO**



Siku 365 tangu Serikali ya Awamu ya Sita iingie madarakani Machi 2021 Watanzania wanaangazia sekta mbalimbali kama vile kilimo, elimu, afya, madini na hata shughuli mbali mbali za kijamii katika kujitathimi walipotoka na wanapoelekea.

Wawekezaji katika Sekta ya Madini wameuzungumzia mwaka mmoja wa Rais Samia Suluhu Hassan madarani kuwa ni mwaka wenye mafanikio na wenye kuleta matumaini kwa wawekezaji walipo hapa nchini na hata waliopo nchi zilizoendelea ambao wapo tayari kuja kuwekeza.

Akizungumza katika mahojiano maalumu na mwandishi wa makala haya, Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya uchimbaji madini ya Nickel nchini (Tembo Nickel), Benedict Busunzu alisema wawekezaji katika sekta ya madini wameshuhudia mabadiliko makubwa katika mazingira ya uwekezaji na hivyo wanamatumaini makubwa kwa siku zijazo.



"Wakati Rais Samia Suluhu Hassan anaingia madarakani, kitu cha kwanza alichozungumzia ni kuifungua nchi yetu, watu wengi hawakumwelewa lakini sisi tuliopo kwenye sekta hii tulimwelewa na katika huu mwaka mmoja wa uongozi wake tunaweza kusimama na kumwelezea ni kwa namna gani ameifungua nchi yetu", alisema Busunzu.

Alifafanua kwamba hivi sasa kampuni ya Tembo Nickel imefanikiwa kuivutia kampuni kubwa ya uchimbaji madini duniani ya BHP kujiunga pamoja katika mradi wa uchimbaji madini ya Nickel unaotarajiwa kuanza kuvuna na kuchimba madini hayo kwa mara ya kwanza ifikapo 2024.

"Si kitu kidogo kuweza kuivutia kampuni kubwa kama hiyo ya kuchimba madini ambayo iliondoka Afrika zaidi ya miaka 10 iliyopita, na sasa inarudi Afrika tena kupitia nchi yetu. Jambo hili linatoa picha kubwa Duniani kwamba Tanzania ni sehemu salama na ya muhimu kuwekeza katika sekta ya madini" aliongeza.

Akiongelea masuala ya upatikanaji wa leseni kwa wachimbaji wakubwa na wa kati, Bosunzu alisema kwamba mwishoni mwa mwaka jana, 2021 wawekezaji watano (5) walikabidhiwa leseni kubwa na za kati za uchimbaji madini ikiwa ni mara ya kwanza katika historia ya Tanzania.

"Unaweza kufikiri leseni tano (5) ni idadi ndogo au ya kawaida, lakini kwa sekta ya madini sikumbuki ni wakati gani idadi kama hiyo ya leseni kubwa na za kati zimewahi kutolewa kwa wakati mmoja.

Hii inatuonyesha ni kwa namna gani Rais Samia ameweka mkazo na msukumo mkubwa kuhakikisha sekta yetu ya madini inanyanyuka na kuweza kuchangia kwa kiasi kikubwa katika uchumi wan chi yetu", alisema. Busunzu alitoa rai kwa Watanzania kujiweka tayari ili kunufaika moja kwa moja na fursa zinazoletwa na wawekezaji katika sekta ya madini ambapo anasema takribani Watanzania elfu 13 wanatarajiwa kupata ajira mara mradi wa Tembo Nickel utakapoanza, kati yao ajira elfu 6 zitatokana na kuajiriwa na wakandarasi na nyingine kwa watoa huduma mbalimbali katika shughuli za uchimbaji.







# Mama Samia Umetufaa Sana Kiuchumi, Kijamii - Mchambuzi

Na **Lillian Shirima**
**Idara ya Habari - MAELEZO**

Ni mwaka mmoja sasa umetimia tangu Rais Samia Suluhu Hassan ambaye pia ni Amiri Jeshi Mkuu wa Majeshi ya Tanzania alipoapishwa na kutangazwa rasmi kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Machi 19, 2021 kufuatia kifo cha aliyekuwa Rais wa Awamu ya Tano, Hayati John Pombe Magufuli Machi 17, 2021.

Rais Samia Suluhu Hassan anawaongoza Watanzania kupitia Awamu ya Sita yenye Kauli mbiu isemayo "Kazii endelee" ikiwa na maana mambo mazuri yaliyoachwa na viongozi waliomtangulia ambayo ni tunu za amani, umoja, mshikamano, kuenzi Mapinduzi ya Zanzibar na kujenga uchumi wa nchi yataendelea kudumishwa na kuimarishwa.

Katika mahojiano maalum na Idara ya Habari-MAELEZO, Mchambuzi wa masuala ya siasa na uchumi kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Severine Kapinga amesema, katika kipindi kifupi cha mwaka mmoja watanzania wanashuhudia namna ambavyo Rais Samia akipeperusha vema bendera ya Tanzania kitaifa na kimataifa.

Ametaja baadhi ya maeneo ambayo mafanikio yake yanaonekana wazi kuwa ni amani, umoja na mshikamano wa kimataifa umeendelea kuimarika na kwamba wananchi wanafanya shughuli zao kwa tija na hivyo kuongeza pato la mtu mmoja mmoja na taifa kwa ujumla.

"Nchi yetu inapoendelea kuimarisha amani na utulivu, hivyo watu wananafanya kazi za uzalishaji mali bila hofu, wanakuwa huru kutoka sehemu moja kwenda sehemu nyingine na mzunguko wa fedha unaonekana", amesema Kapinga.

Aidha, amefafanua kwamba tangu alipoingia madarakani amekuwa akihimiza wasaidizi wake kufanya kazi kwa bidii na maarifa huku akisisitiza kushughulikia changamoto zinazikwamisha maendeleo nchini. Katika kipindi cha mwaka mmoja Rais Samia mbali na kupitia sekta zote kiutendaji, ameweka mkazo kwenye sekta za kimkakati zenye mchango mkubwa katika maendeleo ya nchi kama vile utalii, kilimo, madini na kuimarisha maeneo mengine mengi ambayo ni chanzo cha ajira kwa watanzania.

Kwa kutambua umuhimu wa kufungua fursa za ajira kwa watanzania, mara kadhaa Rais Samia amehimiza sekta binafsi zinazomilikiwa na watanzania wenyewe kupewa kipaumbele kwenye zabuni mbalimbali ili kuruhusu sekta hizo kukua na kutoa ajira zaidi kwa watanzania wenyewe.

Mbali na hayo, Kapinga anamwelezea Rais Samia kama kiongozi mpambanaji katika kuhakikisha kuwa milango ya biashara inafunguka kwa kuweka mazingira wezeshi ya kuvutia kufanya biashara na hata wawekezaji kuwekeza nchini.

Amesifu juhudi na uwezo mkubwa alionao Rais Samia katika ushawishi wa kidiplomasia unayoiletea nchi yetu heshima katika mataifa ya ukanda wa Afrika Mashariki na pia kimataifa.

Akitoa mifano ya ziara yake ya Ufaransa na Ubelgiji aliyofanya Mhe. Rais Samia hivi karibuni amesema, mbali na kujifunza kutoka kwa mataifa mengine yaliyoendelea ziara hiyo imefanikiwa kuimarisha uhusiano wa kidiplomasia na kufungua fursa za ushirikiano wa biashara na kiuchumi kwa Tanzania na Ufaransa.

"Magazeti mengi yaliandika na kumpongeza Rais Samia kwa kazi anayoifanya,akiwa Ufaransa Rais ameshuhudia utiaji saini wa msaada wa mkopo wa kusaidia ujenzi wa awamu ya tano ya mabasi yaendayo kazi (BRT) Euro milioni 178, Mkataba wa ukarabati wa uwanja wa ndege wa Mwalimu Nyerere Terminal 2 na mikataba mingine haya yote ni kuhakikisha nchi inaendelea", amesema Mtaalamu huyo wa Masuala ya Siasa na Uchumi.

Ametaja mkopo mwingine ambao nchi ilipata kutokana na ziara za kidiplomasia za Rais Samia ni ule wa Shilingi za Kitanzania trilioni 1.3 kutoka IMF ambapo fedha hizo



zililenga kushughulikia na UVUKO-19 kama vile ununuzi wa vifaa vya hospitali kwa ajili ya kusaidia wagonjwa, ujenzi wa vyumba vya ICU, ujenzi wa vituo vya dharura, vyumba vya madarasa, usambazaji wa maji hasa maeneo ya vijijini na mahitaji mengine mengi ambayo yalilenga afya ya jamii.

Kama hiyo haitoshi amesema, Rais Samia ni kiongozi msikivu anayezingatia sheria na utawala bora katika mipango yake kwani amekuwa na utaratibu wa kukutana na makundi tofauti ya watanzania bila kujali itikadi za kisiasa, kidini au kikabila hatua anayosema inakuza demokrasia, umoja na ushirikiano katika kuunganisha nchi na kukuza maendeleo.

Amempongeza Rais kwa hutua anazochukua za kukutana na makundi tofauti kama vile wazee, wanawake, wamachinga, viongozi wa dini jambo linalokuza ushirikiano na kutoa hamasa katika ujenzi wa nchi.Kadhalika, Kapinga amesema, ushirikishwaji wa vijana katika masuala ya uongozi unadhihirisha kwamba Rais Samia ni kiongozi msikivu anayethamini na kutambua uwezo walionao vijana katika kuleta mabadiliko chanya na pengine jambo hilo ndilo linalochagiza vijana kuteuliwa katika ngazi za uongozi.

"Taifa lolote duniani hujengwa na nguvu ya vijana kwa kuwa vijana ni kundi pana katika shughuli za kila siku na pia ni kundi lenye uthubutu, ubunifu na msukumo wa kuleta mageuzi kiuchumi, kisiasa na kijamii tusipotumia maarifa waliyonayo kasi ya maendeleo katika jamii yoyote inapungua.

Amesifu uteuzi wa wakuu wa wilaya nchini uliofanywa na Rais Samia Juni, 2021 na kusema kwamba, ingawa amewaridisha waliowahi kushika nafasi hizo za uongozi awali, ameingiza sura mpya katika uongozi wa wilaya wengi wao wakiwa vijana kitendo kinachoamsha ari ya vijana kufanya kazi kwa bidii na kukuza moyo wa uzalendo.

Amewataja baadhi ya vijana walioteuliwa kuwa ni Simon Simalenga (Songwe), Joshua Nassari (Bunda), Fatma Nyangasa (Kigamboni), Gabriel Zakaria (Busega) na Albert Msando (Morogoro) ambaye kwenye sakata la wamachinga alionyesha umahiri wa juu kwa kuwapanga vizuri wafanyabiashara hao kwenye maeneo stahiki bila kuamsha taharuki dalili inayoonesha uwezo wa kukabiliana na changamoto.


Hata hivyo, Kapinga amesema ni muhimu kufahamu kuwa, tunapozungumza habari ya mabadiliko ya kijamii tunazungumzia ushirikishwaji wa makundi ya jamii na hasa kundi la vijana ambao ni nguzo katika ujenzi wa taifa na hivyo anachofanya Rais ni kuwaandaa vijana kulitumikia taifa lao.

"Unapoona kiongozi kijana ameteuliwa kwenye nafasi, tafsiri yake sio ameenda kupewa madaraka, ameenda kupewa kazi ya kusimama na kuhakisha jamii na uchumi wa nchi unaimarika na kuweza kujifuza siasa ya nchi na kutengeneza uzalendo", amesema Kapinga.

Hongera Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Samia Suluhu Hassan kwa kutambua kiu ya wananchi wako katika katafuta maendeleo yao na nchi kwa ujumla lakini pia kwa kutukumbusha wajibu wetu kama watanzania wazalendo kufanya kazi kwa bidii na kuitunza amani tuliyonayo.







# Tanzania Kichocheo cha Utengenezaji Betri za Umeme za Magari Duniani

Na **Immaculate Makilika - MAELEZO**
na **Natasha Liddell - Kabanga Nickel**

Hivi karibuni Serikali imeboresha mazingira ya uwekezaji nchini ambapo katika eneo la uchimbaji madini na uwekezaji kumekuwepo na mabadiliko ya mazingira ya uwekezaji kwa njia za udhibiti na zinazohimiza uwazi na ushirikiano katika sekta hii.

Mafanikio haya ya Serikali yamekuwa pia ni mafanikio ya Kampuni ya Kabanga Nickel, ambapo inaelezwa kuwa kiwango kikubwa cha madini ya nikeli yanapatikana nchini Tanzania katika eneo la kabanga wilayani Ngara mkoani Kagera.

Ndani ya siku 365 za Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Samia Suluhu Hassan anafanya ziara yake ya pili wilayani Ngara mkoani Kagera  Februari 23, 2022 ambapo anaeleza msimamo wa Serikali katika kuhakikisha madini hayo yanachimbwa na kuleta faida kwa wawekezaji na kuinua uchumi wa  Tanzania.

Ambapo Mhe. Rais alioneshwa kukerwa na changamoto zilizojitokeza katika utekelezaji wa mradi huo uliocheleweshwa kwa zaidi ya miaka nane kwa kwasababu ya wananchi wasiowaaminifu kuweka 'tegesha' kwa matarajio ya kufidiwa.

"Machimbo ya Nikeli tutahakikisha watu wa Ngara wananufaika kwanza, na tumeamua kuweka mitambo ya uchenjuaji kule Kahama kwasababu ardhi ipo na miundombinu ipo, lakini ujanja ujanja wa baadhi yenu ndio unafanya mnajichelewesha wanaopaswa kulipwa fidia wapo lakini mnaweka tegesha sasa hatuendi hivyo," anasema Rais Samia.

Hifadhi ya Kabanga yenye madini ya aina tatu muhimu ya nikeli, shaba na kobalti ambayo yana uwezo wa kujaza mahitaji yanayoongezeka ya betri zinazotumika katika magari ya umeme. Baraza la Uchumi la Dunia linakadiria kuwa mahitaji ya Nikeli kwa daraja la kwanza kwa kiwango cha juu yataongezeka kwa mara 24 kati ya mwaka 2018 na 2030.

Serikali ya Tanzania ni mshirika muhimu katika maendeleo ya mradi jumuishi wa Kabanga ili kujenga thamani ya pamoja. Katika hotuba yake kwenye Mkutano wa COP26 mjini Glasgow uliofanyika Novemba mwaka 2022, Rais Samia anasisitiza haja ya nchi zilizoendelea kulisaidia bara la Afrika katika kukabiliana na changamoto za mabadiliko ya tabianchi.

Ushirikiano wa Kabanga na Serikali, na kuungwa mkono na BHP ni mfano wa jinsi hii inaweza kuafikiwa. Licha ya Rais Samia kuonesha utayari huo wa Serikali yake katika kuhakikisha shughuli za uchimbaji madini zinafanywa kama inavyokusudiwa nayo Kampuni ya Ubia ya Tembo Nickel Corporation inayomiliki Leseni Maalum ya Uchimbaji madini (SML) Katika kipindi cha mwaka mmoja tu imefanikiwa kuunda Mkataba wa Mfumo unaoainisha muundo wa utawala wa mradi wa Kabanga.

Serikali ambayo inamiliki asilimia 16 ya mradi huo kupitia kampuni ya ubia ya Tembo Nickel Corporation kwa kutumia mtindo wa biashara wa manufaa kamili ya ndani ya nchi kuzalisha nikeli ya daraja la kwanza ya betri iliyosafishwa yenye bidhaa za ziada za shaba na kobalti, thamani iliyoongezeka itabaki ndani ya Tanzania.

Aidha, Kabanga Nickel pia inavutia uwekezaji kutoka katika kampuni inayoongoza duniani ya madini, BHP kwa kuzingatia kuwa Tanzania imekua nchi yenye mazingira tulivu ya uwekezaji na kuhamasisha uwekezaji kutoka nje ili kusaidia nchi kuwa katika nafasi muhimu katika uchumi wa dunia.

Sambamba na hilo, kupitia mradi huu Tanzania inaisaidia dunia kupata madini muhimu ambayo yatasaidia mabadiliko ya nishati duniani.

Machimbo ya Nikeli ya Kabanga yanakadiriwa kuwa na hazina ya tani milioni 58 za











madini yenye tani milioni 1.52 za nikeli, pamoja na kiasi kikubwa cha shaba na kobalti ambayo pia yanaweza kuchimbwa kwa zaidi ya miaka 30.

Aidha, ubora wa mwamba wa madini na jiolojia yake inamaanisha kuwa mradi huo utakuwa wa uchimbaji wa madini ya nikeli, shaba na kobalti daraja la kwanza kutoka nchini na tayari kwa matumizi ya wateja na watengeneza betri bila uchakataji wowote. Kama tunavyofahamu kuwa dunia inakumbwa na changamoto ya hewa ya ukaa, hivyo nikeli inayochimbwa Kabanga pia inakusudia kupunguza kiwango cha uzalishaji wa hewa chafu katika maendeleo kwa kutumia teknolojia ya hydrometallurgy kuchakata ore iliyokolea, badala ya kuyeyusha kwa kiasili.

Faida za kuwa na uchimbaji wa madini ya Nikeli nchini ni utasaidia kuondoa hitaji la kusafirisha makinikia kwenda katika viwanda vya kuyeyusha na kusafishia madini ya nje ya nchi, hivyo kupunguza mtaji na gharama za uendeshaji kwa athari ndogo za kimazingira, kuzalisha chuma ndani ya nchi, vilevile Watanzania watanufaika kutokana na mradi huu kiuchumi na kijamii kutokana na mradi wa kiwango cha kimataifa wa uchimbaji madini na uchenjuaji.

Aidha, mradi huu ambao utazalisha metali kwa ajili ya mpito wa nishati kama mojawapo ya vitoa kaboni duni zaidi kati ya shughuli zozote za usindikaji wa nikeli duniani.



# Sekta Binafsi Yampongeza Rais Samia Kuweka Mazingira Mazuri ya Biashara, Uwekezaji

Na **Jonas Kamaleki**
**Idara ya Habari - MAELEZO**

Sekta binafsi imempongeza Mhe. Samia Suluhu Hassan, Rais wa jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuweka mazingira mazuri ya biashara na uwekezaji na kwa ushirikiano mkubwa kati ya Serikali na sekta hiyo.

Tangu Serikali ya Awamu ya Sita iingie madarakani mwaka mmoja uliopita, imeonesha dhahiri ushirikiano na Sekta binafsi katika kukuza biashara na kuweka mazingira wezeshi ya uwekezaji.

Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Rais Samia Suluhu Hassan imesimama kidete kuhakikisha inakuza biashara na uwekezaji ili kuzalisha ajira pamoja na kukuza ustawi wa jamii na uchumi wa watu.

Ili kutimiza azma yake adhimu, Rais Samia amekutana na wafanyabiashara wa jijini Nairobi, Kenya ambapo amewaeleza mageuzi yanayoendelea kufanywa na Serikali yake kwa lengo la kuboresha mazingira ya sekta hizo. Mabadiliko hayo ni kushughulikia vibali kwa wataalamu wa kigeni, utendaji wa kituo cha pamoja cha uwekezaji, kuondoa kero katika kodi na ushuru, ada ya mtumiaji na tozo nyingine, na kuweka busara katika usimamizi wa kodi.

Mengine ni mapambano dhidi ya rushwa na urasimu katika sekta ya umma, kutambua na kutenga ardhi kwa ajili ya uwekezaji, kujenga 'industrial parks' na kunyoosha kazi za mamlaka za udhibiti.

“Na ili kuhakikisha biashara na uwekezaji unakuwa endelevu na wenye manufaa, Tanzania imewekeza miradi mikubwa kwenye miundombinu zikiwamo barabara, bandari, reli, viwanja vya ndege na uzalishaji wa nishati,” anasema Rais Samia.

Jitihada za Rais Samia zinatoa matumaini kwamba zitarudisha imani kwa wawekezaji na kutoa vivutio kwa wawekezaji mahiri (Strategic Investors), ikiwa ni pamoja na kuwezesha uwekezaji kufanyika kwa haraka. Katika kipindi hiki cha uongozi wake, Rais Samia amekutana na wafanyabiashara, ametatua baadhi ya changamoto zao na kuongeza ujazo wa mzunguko wa fedha kwa kuwalipa wakandarasi mbalimbali.

Sambamba na hayo, Mhe. Rais amefurahishwa kuona wafanyabiashara wazawa wanapata zabuni katika miradi mbalimbali pamoja na kupunguza kero mbalimbali zinazowakabili wawekezaji na wafanyabiashara wa sekta binafsi.

Mwenyekiti wa Taasisi ya Sekta Binafsi Tanzania (TPSF), Bi. Angelina Ngalula amezungumzia namna ambavyo Serikali ya Awamu ya Sita imeweka mazingira mazuri yanayostawisha sekta binafsi.

“Tozo zaidi ya 200 zimefutwa katika kipindi mwaka mmoja wa Uongozi wa Mhe. Rais Samia Suluhu Hassan, uwezeshaji sekta binafsi kupitia ushirikishwaji katika miradi mikubwa ni kipaumbele cha Serikali ya Awamu ya Sita kwa sasa,” alisisitiza Bi Ngalula.

Bi. Ngalula amesema urasimishaji biashara umepewa mkazo katika kipindi hiki ili kukuza sekta binafsi na kwamba Serikali imeanzisha maeneo maalum ya uwekezaji wa viwanda. Hivi karibuni katika Maonesho ya Dubai (Dubai Expo 2020) Bi. Angelina amesikika akimsifia Rais Samia akisema, “Kwa niaba ya TPSF tunakushukuru kwa ushiriki wako katika Kongomano hili muhimu, tangu umekuwa madarakani mwaka takribani mwaka mmoja umekuwa ukisisitiza ushirikiano kati ya Serikali na Sekta Binafsi kuwaendeleza wananchi kiuchumi”. Aliongeza kuwa

ushirikiano huo ni matokeo ya juhudi za makusudi za kuendeleza biashara na uwekezaji zinazofanywa na Kiongozi Mkuu wa Nchi.

"Mhe. Rais, mwaka wako mmoja madarakani tumeshuhudia mabadiliko makubwa katika kuweka mazingira wezeshi katika uwekezaji na biashara kwa ujumla. Katika Kongamano hili tunao zaidi ya wafanyabiashara 100 wakubwa wanaotaka kuwekeza Tanzania na wengine wameshaanza kuwekeza nchini tayari", alidhihirisha Bi. Ngalula.

Ni ukweli usiopingika kuwa Rais Samia ameonesha juhudi kubwa za kukuza uchumi kwa kuthamini mchango wa Sekta Binafsi katika kutengeneza ajira kwa vijana. Si hilo bali Mhe. Rais amejikita katika kuimarisha Diplomasia ya Uchumi. Ziara zake za hivi karibuni nchini Ufaransa, Ubelgiji na hatimaye kwenye Dubai Expo 2020 zimekuwa na manufaa makubwa kwa Tanzania hasa kwenye kuvutia wawekezaji kama ilivyoshudiwa hati za makubaliano zikisainiwa Dubai kati ya wafanyabiashara wakubwa na Tanzania. Katika Kongamano la Biashara na Uwekezaji jijini Dubai zimesainiwa hati za makubaliano 37 jambo ambalo si kawaida kufanyika kwa kipindi kifupi katika nchi moja.

Mwaka mmoja wa Rais Samia Madarakani, Kazi Inaendelea. Heko Rais Samia kwa kuinua uchumi wa Watanzania.






Maelezo
2022.MAELEZO PODCASTS.
SIKILIZA PODCASTS
ZA KISWAHILI KUTOKA
IDARA YA HABARI
MAELEZO.
2022.MAELEZO PODCASTS.
MAELEZO PODCASTS
Tunapatikana: Spotify, Apple Podcasts, Google Podcasts, Amazon music, Stitcher
iHeartRadio, Pandora, TuneIn + Alexa, Podcast Addict, Podchaser, Pocket Casts,
Overcast, Castro, Castbox, Podfriend, Deezer, Listen Notes, Player FM, Podcast Index
Podcast Index, AudioMack, Soundcloud
MSEMAJIMKUUWASERIKALI/MAELEZONEWS/
WWW.MAELEZO.GO.TZ


Maelezo
2022.MAELEZO PODCASTS.
SIKILIZA PODCASTS
ZA KISWAHILI KUTOKA
IDARA YA HABARI
MAELEZO.
2022.MAELEZO PODCASTS.
MAELEZO PODCASTS
Tunapatikana: Spotify, Apple Podcasts, Google Podcasts, Amazon music, Stitcher
iHeartRadio, Pandora, TuneIn + Alexa, Podcast Addict, Podchaser, Pocket Casts,
Overcast, Castro, Castbox, Podfriend, Deezer, Listen Notes, Player FM, Podcast Index
Podcast Index, AudioMack, Soundcloud
MSEMAJIMKUUWASERIKALI/MAELEZONEWS/
WWW.MAELEZO.GO.TZ



Maelezo
2022.MAELEZO PODCASTS.
SIKILIZA PODCASTS ZA KISWAHILI KUTOKA IDARA YA HABARI MAELEZO.
2022.MAELEZO PODCASTS.
MAELEZO PODCASTS
Tunapatikana: Spotify, Apple Podcasts, Google Podcasts, Amazon music, Stitcher iHeartRadio, Pandora, TuneIn + Alexa, Podcast Addict, Podchaser, Pocket Casts, Overcast, Castro, Castbox, Podfriend, Deezer, Listen Notes, Player FM, Podcast Index Podcast Index, AudioMack, Soundcloud
MSEMAJIMKUUWASERIKALI/MAELEZONEWS/
WWW.MAELEZO.GO.TZ